Ijumaa Juni 21, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579950

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Auawa kwa tuhuma za wizi mboga mafungu 6

UKURASA 3


Baada ya korosho kukwama, Kibiti yahamishia mtego wa mapato ufuta
Ukurasa 19
UCHUMI
BUFE
Ijumaa Juni 21, 2019
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Tanzania katika mageuzi makubwa utalii duniani ikibeba sura ya kinara
Ukurasa 14
MAGEUZI BANDARI ZA VICTORIA
Walichokikosa miaka 61, leo mashuhuda kuingia 'chomboni' bila kukanyaga maji
Ukurasa 16
UCHUMI
Ukurasa 18
Biashara katika picha
Ukurasa 17

UKURASA 13

**TISHIO LA UGAIDI:**

# Balozi Marekani aitwa kujieleza

**AKIRI** kufanya makosa, Waziri Lugola awatoa hofu Watanzania, asema vyombo vya ulinzi viko imara... *Endelea ukurasa wa 2*



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akipita karibu na rundo la ngozi zilizotelekezwa katika eneo la Mbagala Rangi Tatu, jana na kusababisha kero kwa wakazi wa eneo hilo, kutokana na harufu mbaya. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Muhimbili kupandikiza uloto wagonjwa selimundo, saratani

UKURASA 2

## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**

**ASASI 28 KUTOA ELIMU DAFTARI WAPIGAKURA**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imetoa vibali kwa asasi za kiraia 28 nchini kutoa elimu ya mpigakura wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura...

**UKURASA WA 3**

**WASIRA AFUNGUKA KUDAIWA HAZINA**

ALIYEWAHI kuwa waziri katika utawala uliopita, Stephen Wasira, amefunguka kudaiwa kwake na Wizara ya Fedha na Mipango, akidai ameshamaliza kulipa deni hilo muda mrefu na anashangaa kuwamo katika orodha ya wadaiwa sugu...

**UKURASA WA 4**

**AFARIKI KWA KUANGUKIWA KIFUSI AKICHIMBA DHAHABU**

MKAZI wa kitongoji cha Mutukura, kijiji na kata ya Nsirorisimba, Butiama mkoani Mara, Nyamhanga Kanyonyi, amekufa papo...

## Makato posho za wabunge gumzo

UKURASA 3

**MICHEZO** WAKUTEMWA YANGA SASA MGUU SAWA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Balozi Marekani aitwa kujieleza

**Na Romana Mallya**

SERIKALI kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imemwita Kaimu Balozi wa Marekani nchini, kutoa ufafanuzi kuhusu taarifa ambayo ubalozi huo, uliitoa juu ya angalizo la kiusalama la uwezekano wa kutokea shambulio la kigaidi.

Wakati balozi huyo akiitwa, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amewaondoa hofu Watanzania kuwa vyombo vya ulinzi na usalama viko imara kukabiliana na hatari zozote zinazoweza kujitokeza.

Juzi, Ubalozi wa Marekani nchini ulitoa taarifa katika mtandao wa kijamii wa "Twitter" ya angalizo la kiusalama kuhusu shambulio la kigaidi katika baadhi ya maeneo ya Jiji la Dar es Salaam.

Kutokana na mwito huo, taarifa iliyotolewa jana na wizara ilisema ubalozi huo ulimtuma mwakilishi wa Kaimu Balozi wa Marekani, Ann Marie Warmenhoven - Tilias, ambaye aliutambua na kukiri kuwa ujumbe huo umetumwa na ubalozi wa Marekani nchini.

Katika ufafanuzi wake, kwa mujibu wa taarifa hiyo, mwakilishi huyo alikiri kuwa, "ubalozi wake umefanya makosa ya kutoa tetesi ambazo hazikuwalenga raia wa Marekani pekee bali raia wote wakitambua kuwa ubalozi hauna mamlaka ya kufanya hivyo, jambo lililosababisha taharuki kwa wananchi na wageni wanaotarajia kuitembelea Tanzania."

"Kutokana na kukiri huko, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeukumbusha Ubalozi wa Marekani umuhimu wa kuzingatia sheria za nchi na taratibu za kidiplomasia zinazokubalika duniani kote katika utoaji wa taarifa za aina hii," iliongeza taarifa hiyo.

Aidha, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Faraji Mnyepe, alikaririwa katika taarifa hiyo akiwataka wananchi na jumuiya za kimataifa pamoja na wageni walioko nchini na wanaotarajia kuitembelea Tanzania, kuendelea na shughuli zao kama kawaida kwa kuwa mpaka sasa hakuna taarifa yoyote iliyothibitishwa ya kuwapo kwa tishio la aina hiyo.

Pia Katibu Mkuu alisisitiza kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vimejizatiti kukabiliana na matishio yoyote.

**LUGOLA AWATOA HOFU**

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amewaondoa hofu wananchi kuhusu tahadhari iliyotolewa na Ubalozi wa Marekani nchini juu ya kuwapo kwa taarifa za tishio la kigaidi, akieleza kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vipo imara na havitishiki.

Lugola alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam jana ikiwa ni siku moja baada ya taarifa ya ubalozi huo kutahadharisha kuwapo kwa mipango ya mashambulizi ya kigaidi eneo la Masaki jijini Dar es Salaam likidaiwa kulengwa.

Katika ufafanuzi wake kuhusu suala hilo jana, Waziri Lugola alisema kuwa baada ya kupata taarifa za tahadhari hiyo, Jeshi la Polisi limefanya mawasiliano na ubalozi huo kujua ulikopata taarifa hizo.

"Serikali ya Rais John Magufuli na vyombo vyake vya ulinzi na usalama vipo imara, havitikisiki, vimejipanga vizuri kwa jambo au tishio lolote la usalama ambalo linaweza kutokea. "Nataka niwahakikishie Watanzania kwamba hizi ni sehemu za taarifa za kawaida ambazo wenzetu wameweza kuzipata na tumewasiliana nao kupitia Jeshi la Polisi," Lugola alisema.

Waziri huyo aliwataka wananchi kutokuwa na hofu kwa kuwa nchi ipo imara na ina usalama wa hali ya juu.

"Vyombo vya usalama vinaendelea kufanya kazi yake na tuviache viendelee kufanya kazi na Watanzania waendelee na shughuli zao. Kama taarifa hizi zipo na kama ni za kweli, nchi ipo imara na tunaendelea, hakuna sababu ya Watanzania

INAENDELEA UK.8

## Asasi 28 zapewa rungu NEC

**Na Enock Charles**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imetoa vibali kwa asasi za kiraia 28 nchini kutoa elimu ya mpigakura ili kutoa elimu hiyo, wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Akizungumza na wawakilishi wa asasi 24 za Tanzania Bara jijini Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti wa NEC, Jaji Mbarouk Mbarouk, alizitaka kufuata sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia utoaji wa elimu hiyo na kutojihusisha na itikadi za kisiasa, udini, ukanda na ukabila.

"Mnapaswa kufahamu kuwa lengo la tume la kuwapatia vibali pamoja na miongozo ni kuhakikisha mnafuata yale tu mnayotakiwa kutekeleza," Jaji Mbarouk alisema.

Asasi zilizoruhusiwa kutoa elimu hiyo ni pamoja na Chama cha Wenye Ualbino, Muungano wa Wapigakura Tanzania, Buguruni Development Organization, Kikundi cha Ujirani Mwema Kigoma, Mulika Tanzania, Kijogoo Group for Community Development, Tanzania Youth Vision Association na Rukwa Legal Aid Organization.

Zingine ni Morogoro Saving the Poor Organization, Green Belt Schools Trust Fund, Safina Women Association, Kigoma Paralegal Aid Centre, People Development Forum, Organization For Youth Community Rights and Development, Rukwa Legal Aid Organization, Grace Community Development and Education na Social Mainstreaming for Gender Equality Organization.

Kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi kinaipa tume jukumu la kutoa elimu ya mpigakura nchi nzima.

Sheria hiyo pia inatoa nafasi kwa tume kukasimisha utoaji wa elimu ya mpigakura kwa taasisi na asasi zenye nia ya kutoa elimu hiyo.




Mkurugenzi wa Huduma za Tiba katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Hedwiga Swai, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Damu wa MNH, Dk. Stella Rwezaura. **PICHA: JOHN STEPHEN**

# Muhimbili kupandikiza uloto wagonjwa selimundo, saratani

**Na Beatrice Shayo**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa mara ya kwanza itaanza upandikizaji wa uloto (Bone Marrow Transplant), kwa wagonjwa wanasumbuliwa na selimundo na saratani ya damu.

Tanzania itakuwa nchi ya kwanza kupandikiza uloto katika Ukanda wa Afrika Mashariki na pia nchi ya sita katika Bara la Afrika. Kwa sasa huduma hiyo Afrika inatolewa Afrika Kusini, Tunisia, Misri, Komoro na Nigeria

Wagonjwa wenye tatizo hilo walikuwa wakipelekwa nje ya nchi kwa gharama ya Sh. milioni 200, hivyo MNH mgonjwa atagharimia chini ya asilimia 50.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Huduma za Tiba, Dk. Hedwiga Swai, alisema wagonjwa hao walikuwa wanapelekwa nje ya nchi kutokana na ukosefu wa wataalamu na vifaa.

"Muhimbili tunatekeleza azma ya serikali ya kupunguza idadi ya wagonjwa wanaokwenda kutibiwa nje ambao mara nyingi walikuwa wakifuata matibabu yasiyopatikana hapa nchini ama kutokana na kutokuwapo wataalamu au ukosefu wa vifaa vya kutolea huduma husika," alisema.

Aidha, alisema hospitali sasa inapeleka wataalamu 11 nchini India katika Hospitali ya Apollo iliyopo Chennai kwa kipindi cha mwezi mmoja ili kujifunza kwa njia ya vitendo jinsi ya kufanya upandikizaji wa uloto.

Alisema huduma hiyo hufanyika kwa kupandikiza chembechembe mama za kuzalisha damu ambazo hupatikana kwenye uloto, (Pluripotent Haemopoietic Stem Cells) au chembechembe mama kutoka kwenye kitovu cha mtoto mchanga (umbilical cord blood) au kondo la nyuma la mama.

"Upandikizaji huu huanza kwa kumwandaa mgonjwa ambaye chembechembe zake za damu zina tatizo kama saratani, selimundu au wale ambao mifupa yao inashindwa kuzalisha damu," alisema.

Aliongeza: "Hii hufanyika kwa kuwapa tiba maalum ili kuua chembechembe zote zenye matatizo kisha kupandikiza chembechembe mpya zilizopo kwenye uloto kutoka kwa ndugu yake mwenye vinasaba vinavyofanana au chembechembe mpya zilizozalishwa kutoka kwa mgonjwa mwenyewe baada ya kupata tiba maalum," alisema.

Aidha, alisema huduma hii inakadiriwa kuwa ni Sh. milioni 200 kwa mgonjwa mmoja ambaye anapandikizwa uloto kutoka kwa ndugu yake wakati akipandikizwa uloto wake mwenyewe si chini ya Sh. milioni 150.

"Takwimu za Hospitali ya Muhimbili zinaonyesha kuwa wagonjwa

INAENDELEA UK.8

## HABARI KITAIFA

# Auawa kwa tuhuma za wizi mafungu 6 spinachi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Ndembezi Shinyanga Mjini, Ester Samwel (35), ameuawa kwa kupigwa na wananchi baada ya kutuhumiwa kuiba mboga aina ya spinachi mafungu sita, nyanya debe moja na mahindi mabichi matatu.

Tukio hilo lilitokea juzi maeneo ya Kitangili, Shinyanga Mjini, wakati Ester alipodaiwa kuiba kwenye sokoni na wananchi kupiga kelele za mwizi na kumshambulia kwa kipigo hadi kusababisha kifo chake.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Richard Abwao, alisema wananchi hao baada ya kumshambulia Ester, alikosa nguvu na hatimaye kukimbizwa hospitali ya rufani ya mkoa na kufariki dunia.

"Chanzo cha mauaji ya mwanamke huyu ni wananchi kujichukulia sheria mkononi baada ya kumtuhumu marehemu kuiba mboga aina ya chinese mafungu sita, nyanya debe moja pamoja na mahindi mabichi matatu," alisema Abwao na kuongeza:

"Mwili wa marehemu umehifadhiwa kwenye chumba cha maiti katika hospitali ya rufani ya mkoa wa Shinyanga, na juhudi za kuwasaka watu waliohusika na mauaji hayo zinaendelea."



Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola (wa tatu kulia), akiongoza maandamano ya kuadhimisha Siku ya Wakimbizi Duniani, jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Meja Jenerali Jacob Kingu, Mwakilishi wa Shirika la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) nchini, Chansa Kapaya (katikati) na (kulia) ni Kamishna Jenerali wa Magereza, Phaustine Kasike. **PICHA: WMN**

# Wasira afunguka kudaiwa Hazina

**Na Gwamaka Alipipi**

ALIYEWAHI kuwa waziri katika utawala uliopita, Stephen Wasira, amefunguka kudaiwa kwake na Wizara ya Fedha na Mipango, akidai ameshamaliza kulipa deni hilo muda mrefu na anashangaa kuwamo katika orodha ya wadaiwa sugu.

Wasira ambaye pia amewahi kuwa Mbunge wa Bunda Mjini kwa muda mrefu kabla ya kushindwa katika Uchaguzi Mkuu uliopita, amelazimika kutoa ufafanuzi kuhusu deni hilo baada ya juzi Wizara ya Fedha na Mipango kutaja jina lake katika orodha ya wadaiwa sugu 15 wa serikali kupitia mpango wa 'Commodity Import Support (CSI)'.

Katika tangazo hilo lililotolewa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Doto James, ilielezwa kuwa madeni hayo ni mkopo wenye masharti nafuu uliotolewa kwa taasisi, kampuni, viwanda na wafanyabiashara kupitia mpango huo.

Katika tangazo hilo, Wasira alitajwa kuwa miongoni mwa wanufaika hao akijipatia mkopo kupitia kampuni za Siza Cold Storage Co.Ltd na 21st Century Afritex Ltd.

Akizungumza na Nipashe jana, Wasira ambaye amewahi kushika nafasi mbalimbali katika serikali ya awamu ya kwanza hadi ya nne, alisema deni alilokuwa akidaiwa lilikuwa limebaki Sh. milioni 26, lakini ameshamaliza kulipa.

"Tulishamalizana na TIB (Benki ya Uwekezaji) na tunajua tumeshalipa deni lote lililokuwa Sh. milioni 26, tunashangaa kusikia bado tunadaiwa," Wasira alisema.

INAENDELEA UK.8

# Mbunge alalamikia makato ya posho

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBUNGE wa Konde, Zanzibar, Khatibu Said Haji (CUF), jana aliomba mwongozo wa kiti cha Spika, akidai kuwa wabunge wanakatwa fedha za vikao kiholela.

Wakati anaomba mwongozo huo, Mbunge huyo alisema: "Mheshimiwa Naibu Spika (Dk. Tulia Ackson), nimesimama kwa Kanuni ya 68 (7), jana tulilipwa malipo ya 'sitting allowance' (posho za kikao) na katika malipo hayo, kumeonekana kuna makato na wengi wetu hatuna taarifa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na utaratibu ambao si mzuri katika jambo hili, na inavyoonekana hili jambo linakuwa endelevu. Watu huko watakuja na mambo yao kama ni malalamiko... kuna watu wana shida kule majimboni kwetu na kama kila mbunge akichukua shida za wapigakura wake zikiletwa humu, ukumbi huu hautatosha."

Aliongeza, "Kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Spika,

INAENDELEA UK.8


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
14 - 06 - 2019

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe 22-06-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar Port kuelekea Kinyerezi ,** gari hizo zenye namba za usajili:
   **T 324 CZS / T 387 DHQ T 628 DFA / T 887 DJB**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **23** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.4** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.4** |

3. Njia itakayotumika: **Dar Port hadi Kinyerezi** Kupitia Tabata, gari zitasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

XXXXXXX

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 19/06/2019

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATATU tarehe 24/06/2019** kampuni ya **S.S.F Co.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR kuelekea KAGERA** gari hilo lenye namba za usajili:
   **T 487 DPY /T166ADN.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita21.40** |
| **Upana** | - | **mita 5.00** |
| **Kimo** | - | **mita 5.10** |

3. Njia itakayotumika **DAR hadi KAGERA kupitia MWENDAKULIMA** gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

215287402

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

## Wakurugenzi kampuni za ujenzi waburuzwa kortini

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Iringa, imewafikisha mahakamani watuhumiwa wawili kwa mashtaka matano yanayohusiana na rushwa.

Mashtaka hayo ni kughushi nyaraka, kuwasilisha nyaraka zilizoghushiwa, kujipatia mali kwa njia ya udanganyifu, kuisababishia hasara mamlaka na kula njama kinyume cha makosa ya kanuni ya adhabu.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Iringa, Mweli Kilimali, alisema jana kuwa waliofikishwa mahakamani ni Edmund Johnson Kileo ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Siha Enterprises Co. Ltd ya Dar es Salaam na Iddy Zorawanga, Mkurugenzi wa Mavonda's Co. Ltd ya Dar es Salaam, kwa tuhuma za kuunda ubia wa uongo.

Alisema Julai, 2017 Kileo, Siha ilitengeneza ubia wa uongo na Mavonda's ili waombe zabuni ya ujenzi wa mradi wa maji wa Sawala, Mtwango, Lufuna na Kibao iliyotangazwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi Julai, 2017 kwa kughushi baadhi ya nyaraka za maombi ya ubia na kuziwasilisha kwa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) ili wapatiwe barua ya utambulisho wa ubia huo.

Kilimali alidai kuwa watuhumiwa hao walitumia barua ya utambulisho wa uongo

INAENDELEA UK. 8

# Afariki kwa kuangukiwa kifusi akichimba dhahabu

**Na Ahmed Makongo,** BUTIAMA

MKAZI wa kitongoji cha Mutukura, kijiji na kata ya Nsirorisimba, Butiama mkoani Mara, Nyamhanga Kanyonyi, amekufa papo hapo baada ya kuangukiwa na kifusi cha udongo wakati akichimba dhahabu.

Wakati Kanyonyi (43) akipoteza maisha, mke wake Kadogo Nyamhanga (23), ambaye alikuwa naye kwenye tukio hilo kijijini hapo, amenusurika kifo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Kamishna Msaidizi (ACP) Juma Ndaki, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo lililotokea usiku wa kuamkia juzi.

"Ni kweli nimempigia simu OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) wa Butiama amesema tukio hilo limetokea usiku majira ya saa sita. Kwa hiyo ni kweli kabisa hilo tukio lipo," alisema Ndaki.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Julius Matiko, na Diwani wa Nsirorisimba, Alexander Makolele, walisema wanandoa hao walikumbwa na tukio hilo wakati wakichimba dhahabu katika eneo la jirani na nyumbani kwao.

Walisema mwanamume huyo alikufa papo hapo na kwamba mke wake aliokolewa na wananchi waliokuwa katika eneo la tukio.

"Huyo mwanaume alikufa baada ya kufunikwa na kifusi wakati wakichimba dhahabu na mke wake. Lakini mwanamke aliokolewa na amepelekwa hospitalini," alisema Makolele.

Alisema mwanamke huyo alipelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mara, mjini Musoma na kisha akahamishiwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando jijini Mwanza baada ya hali yake kuendelea kuwa mbaya.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akizungumza na viongozi wa Chuo cha Mafunzo ya Kigeni na Utalii cha nchini China, kijulikanacho kwa jina la JXCFFS, baada ya kuwatambulisha wageni hao, bungeni jijini Dodoma jana. Viongozi hao wamekuja kwa lengo la kuwajengea uwezo wa mafunzo watumishi na wadau wa utalii hapa nchini. **PICHA: WMU**

# Watumishi, wadau kujifunza Kichina kuteka soko la utalii

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, imesema kwa sasa mwelekeo wa soko la utalii nchini limelenga kupata watalii wengi kutoka China.

Kutokana na dhamira hiyo, wizara hiyo ikiwa na dhamana ya kusimamia sekta ya utalii, imeweka mkazo kwa watumishi na wadau kujifunza lugha ya Kichina.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alisema jana alipokuwa akizungumza na viongozi wa Chuo cha Mafunzo ya Lugha za Kigeni na Utalii cha China kijulikanacho kwa jina la JXCFFS.

"Nguvu nyingi kwa sasa zinaelekezwa nchini China, hivyo ni muda mwafaka wa kuandaa timu ya wataalamu mbalimbali, wakiwamo waongoza watalii watakaoweza kuzungumza lugha ya Kichina ili kulimudu soko hilo," alisema. Kanyasu alisema lengo la mkutano huo ni kuimarisha ushirikiano kati ya China na Tanzania katika kuwajengea uwezo watumishi na wadau wa utalii nchini.

Mkutano huo ulihudhuriwa na ujumbe kutoka China ukiongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Xiong Nanyong, Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Lucius Mwenda, na viongozi waandamizi wa wizara.

Alisema ni muhimu kwa watumishi wa wizara na wadau wa utalii kujiandaa ili kuzungumza lugha ya Kichina badala ya vifaa maalum vya kutafsiri lugha ilhali kuna uwezekano kwa Watanzania kujifunza. Naye Prof. Xiong alisema wamejipanga kutoa mafunzo mbalimbali yakiwamo ya lugha ya Kichina na utalii ili kuwajengea uwezo watumishi hao.

Aliongeza kuwa wameshaomba kibali kutoka Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kutoa mafunzo hayo nchini.

Kwa upande wake, Mwenda aliahidi kutoa ushirikiano kwa uongozi wa chuo hicho ili kujengeana uwezo baina ya serikali ya Tanzania na China.


**Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-**

- **Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=**
- **Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=**
- **Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima**
- **Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku**

215227501



## HABARI KITAIFA

# Waliokata watu koromeo kunyongwa hadi kufa

**Na Mwandishi Wetu,** BUKOBA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Bukoba imewahukumu kunyongwa hadi kufa washtakiwa watatu waliokuwa wanakabiliwa na kesi ya mauaji ya kikatili kwa kuwakata watu wanne koromeo katika Kijiji cha Kashenge Kata ya Katoma Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera.

Matukio hayo ya kikatili yalitendeka Novemba mwaka 2015.

Akisoma hukumu ya kesi hiyo namba 66 ya mwaka 2017 juzi jioni, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma ambaye alikuwa akisikiliza kesi hiyo tangu ifunguliwe akiwa Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu kanda ya Bukoba, Lameck Mlacha, alisema mahakama imejiridhisha bila kuacha shaka kutokana na hoja zilizotolewa na mashahidi 18 kwa upande wa Jamuhuri na zilizotolewa na mashahidi wanne wa utetezi.

Jaji Mlacha alisema mashahidi upande wa Jamhuri waliwasilisha ushahidi wa mawasiliano ya simu ya mara kwa mara yaliyokuwa yakifanywa na washtakiwa na mshtakiwa namba mbili, Rashid Athuman kukutwa na simu ya marehemu aliyeuawa na washtakiwa.

Upande wa Jamuhuri pia umeeleza kuwa vipimo vya vinasaba (DNA) vilivyofanyika kwa kuchunguza miili ya marehemu na vitu vyenye ncha kali (mapanga) yaliyotumika yaliondoa wasiwasi katika mahakama hiyo juu ya makosa hayo.

Baada ya hukumu hiyo, Wakili wa Serikali Mkuu, Hashimu Ngole, ambaye alikuwa kiongozi wa mawakili kwa upande wa Jamhuri, alieleza alivyopokea kesi 12 za mauaji zilizokuwa zikiwakabili watuhumiwa hao.

Alisema watuhumiwa hao walikiri makosa na mahakama kuona wana hatia, hivyo kuwapa adhabu hiyo, ambayo alisema waliistahili.

Wakili aliyeongoza jopo la utetezi, Mathias Rweyemamu, alieleza kutoridhishwa na hukumu hiyo, licha ya utetezi uliotolewa mahakamani.

Watuhumiwa waliohukumiwa kunyongwa hadi kufa ni Njeleka Joseph, Rashid Athuman na Aliyu Daudi, ambapo waliwaua watu wanne kwa kuwakata koromeo.

Watuhumiwa hao walitenda ukatili huo katika Wilaya za Bukoba, Missenyi na Muleba pamoja na uchomaji makanisa mwaka 2015.

# Mabula aahidi kumaliza mgogoro bonde la Buswelu

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

BAADHI ya wananchi wanaomiliki mashamba katika bonde la kilimo Buswelu, Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza, wameiomba serikali kuingilia kati mgogoro baina yao na halmashauri kufuatia upimaji wa maeneo unaendelea bila kushirikishwa.

Viongozi wa mitaa pamoja na baadhi ya wananchi wanaomiliki mashamba katika eneo hilo, walisema wameshtushwa na uamuzi huo wa kutaka kugeuza eneo hilo kutoka bonde la kilimo kuwa makazi, ambalo awali walisema halifai kwa makazi kutokana na uwapo wa mkondo wa maji.

Nipashe ilifika katika bonde hilo na kushuhudia bikoni za upimaji huku baadhi ya wananchi wakiendelea na shughuli za kupalilia mpunga na wengine wakimwagilia katika bustani za mboga.

Charles Renatus, mkulima wa mboga za majani katika bonde hilo, alisema jiji la Mwanza linategemea bonde hilo kwa huduma ya mboga za majani na matunda na wakulima wananufaika kwa chakula na kipato.

Alisema awali serikali ilitenga eneo hilo kuwa bonde la kilimo kutokana na kuwa hatarishi kwa sababu ya kujaa maji na kuhoji inakuwaje serikali igeuze kuwa makazi.

"Watu wa Buswelu hatukuwa na taarifa, tukaambiwa kule kuna upimaji unaendelea pasipo hata sisi wananchi kushirikishwa kwamba kuna nini kinachoendelea, lakini tumejaribu kuwauliza wakadai kwamba hapa tayari tumeshabadilisha mchoro tuweke mji wa kisasa kwenye bonde hili mvua ikikubali hapa panakuwa kama ziwa, hili bonde likifungwa mboga zinazotumika kwa chakula itakuwa hamna," alisema Renatus.

Agnes Simiyu mkazi wa Buswelu A, alisema mageuzi yanayofanywa katika bonde hilo yatawaathiri wenye mashamba kwa kuwa licha ya kupata chakula pia anasomesha watoto.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Buswelu A, Shedrack Shindano na mwenyekiti wa mtaa wa Buswelu B, Yega Martine, walikiri kuwapo kwa sintofahamu hiyo baina ya wananchi na halmashauri ya manispaa na kwamba suala ni kutokuwapo kwa mawasiliano na maelewano upimaji maeneo ya watu yaliyogeuzwa matumizi.

"Watu wanaofanya shughuli ya kupima maeneo hayo wanaharibu mazao ya wamiliki wa mashamba kwa kukanyaga mpunga ambao haujakomaa na kama sehemu wanapotaka kuweka bikoni kuna mazao ya watu wanachofanya wanachimba viazi ambavyo havijakomaa wanaweka bikoni, hali hii inasikitisha, wangesubiri kwanza watu watoe kwanza mazao yao shambani ndipo zoezi lao liendelee," alisema Shedrack.

Naibu Waziri wa Ardhi ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Angelina Mabula, alipozungumza na Nipashe kwa njia ya simu, alisema taratibu za uthamini zimefanyika baada ya kukaa vikao zaidi ya vitatu vya halmashauri na kabla ya zoezi hilo kuanza kamati za maendeleo za kata ya Buswelu na Nyamongolo mahali ambapo mradi upo zilikaa ili kukubaliana.

"Taratibu za uthamini baada ya vikao kukubaliana zilifanyika na tayari wananchi 300 wameshathaminiwa na wanachosubiri ni kulipwa pesa zao," alisema Mabula.

Mabula alisema ombi la kusitishwa kwa zoezi la upimaji amelipokea baada ya kupigiwa simu na baadhi ya walalamikaji na amewahakikishia kuwa atakapomaliza vikao vya Bunge la Bajeti 2019/2020 vinavyoendelea jijini Dodoma, atakwenda katika eneo la mradi huo na kuzungumza na wananchi kumaliza mgogoro huo.






## NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Sisi **Yono Auction Mart and Company Ltd** Kwa idhini tuliyopewa na **AMANA BANK LTD** na mamlaka tulionayo kisheria tunatoa notisi ya siku 14 kuanzia siku ya tangazo hili kwa wadaiwa wote na wadhamini mlipe madeni yenu yote kinyume cha hapo tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wake. Mnada utafanyika mahali ilipo dhamana.

### MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA NA MAHALI ILIPO

| NA | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | JINA LA MMILIKI | DHAMANA INAYOUZWA | MAHALI DHAMANA ILIKO | TAREHE YA MNADA NA MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ELIAMANI SHABANI MGALLAH | ELIAMAN SHABANI | C.T No. 24342 LR Moshi, L.O No. 311187 | Plot No 29, Block 'W' Area 'F' Arusha Municipality | Tarehe 13.07.2019 Saa Nne (10:00 A.M) asubuhi na kuendelea |
| 2 | FALAHI INDUSTRIES LIMITED | MOHAMED IQBAL ARBI | C.T No. 13137-MBYLR, L.O No. 342563 | Plot No 205, Block 'Industrial area' Industrial Area Kibwabwa Iringa Municipality | Tarehe 14.07.2019 Saa Nne(10:00 A.M) asubuhi na kuendelea |
| | | MOHAMED IQBAL ARBI | C.T No. 20009-MBYLR, L.O No. 434302 | Plot No 206, Block 'Industrial area' Industrial Area Kibwabwa Iringa Municipality | Tarehe 14.07.2019 Saa Nne(10:00 A.M) asubuhi na kuendelea |
| | | IQBAL ARABI | C.T No. 5908-MBYLR L.O No. 149139 | Plot No 53, Block 'IB' Wilolesi area Iringa Municipality | Tarehe 14.07.2019 Saa Nane(02:00 P.M) mchana na kuendelea |
| | | THADEI FRANCIS MOSHY | C.T No. 131577 L.O No. 492988 | Plot No 2207, Block 'C' Goba Kunguru Area, Kinondoni Municipality | Tarehe 12.07.2019 Saa Nne(10:00 A.M) asubuhi na kuendelea |
| 3 | TWAIBA AHMED ALLY | TWAIBA AHMED ALLY | C.T No. 80526 L.O No. 282824 | Plot No 66, Block 'D' Temeke area, Dar es salaam City | Tarehe 12.07.2019 Saa Nane(02:00 P.M) mchana na kuendelea |
| | | ATWIYE SWALEH KARAMA | C.T No. 27382 LR Moshi, L.O No. 170792 | Plot No 18, Block 'E' Kana area, Tanga City Council | Tarehe 16.07.2019 Saa Nane (02:00 P.M) Mchana na kuendelea |
| 4 | WAHIDA HASSAN SAID | | C.T No. 37583/1, L.O No. 170792 | Plot No 25, Block 'M' Kariakoo area, Dar es salaam City | Tarehe 12.07.2019 Saa Nne(10:00 A.M) asubuhi na kuendelea |

**Yono Auction mart Mawasiliano simu No 0767 675 168**

**MASHARTI YA MNADA**

1) Mnunuzi anatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki atakilipa ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
2) Ukaguzi wa dhamana utafanyika siku nne kabla ya mnada kuanzia saa Nne(10:00 A.M) asubuhi hadi saa Nane (02:00 P.M) mchana.
3) Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine zikiwemo usafiri ni za mnunuzi.
4) Dhamana itauzwa "kama ilivyo"

*215288002*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bravo NEC ushirikishaji wa wadau uboreshaji daftari

**MAANDALIZI** ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Oktoba mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani, yameanza baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuanza mchakato wa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Maboresho ya daftari hilo yanatarajiwa kuanza mwezi ujao katika mikoa yote nchini, ambapo walengwa watakuwa ni wale waliopoteza kadi zao za kupigia kura, wapigakura wapya na waliohama maeneo yao. Uboreshaji wa daftari ni takwa la kisheria, ndio maana NEC imeanzisha mchakato huo.

Kumekuwapo na malalamiko mengi tangu daftari hilo lilipoanza kutumika mengi yakihusu wapigakura kutokukuta majina yao katika orodha ya wapigakura siku ya uchaguzi, hivyo wengi kukosa haki yao ya kupiga kura.

Hali hiyo imekuwa ikilalamikiwa na wagombea, wapigakura, vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi, hivyo kutoa taswira mbaya ya NEC; kwamba inashindwa kutekeleza wajibu wake wa msingi wa kuratibu na kusimamia uchaguzi.

Lingine ambalo limekuwa likilalamikiwa ni uteuzi wa waandikishaji wa daftari na wasimamizi wa uchaguzi, kubwa likiwa ni kukosa imani na baadhi yao; kuwa wanapewa nafasi hizo kwa kuzingatia itikadi za vyama.

Hata hivyo, katika maandalizi ya uboreshaji wa daftari hilo, Tume imechukua hatua kadhaa, lengo likiwa kuepusha malalamiko na changamoto zingine.

Kikubwa ambacho NEC imekifanya, na ambacho kinastahili pongezi ni kushirikishaji wa makundi yote ya jamii kwa kuandaa semina na kujadiliana nayo kuhusiana na mambo mbalimbali, yakiwamo kueleza sheria, kanuni, taratibu na maelekezo ya tume kuhusiana na mchakato wa uboreshaji wa daftari hilo. Kwa kufanya hivyo, itapata mawazo na maoni tofauti yatakayoisaidia kuboresha utendaji.

Kwa kipindi cha wiki mbili hadi jana NEC ilikutana na kila kundi kwa siku moja jijini Dar es Salaam. Makundi yaliyohusishwa ni ya wadau kutoka vyama vya siasa; viongozi wa dini; wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; vyombo vya habari na asasi za kiraia. Utaratibu huo ni mzuri kwa kuwa umewawezesha wadau kutoa maoni na mapendekezo yao pamoja na NEC kuwapa ufafanuzi wa sheria, kanuni na taratibu za uandikishaji na uboreshaji wa daftari hilo.

Miongoni mwa mambo ya msingi na ambayo yatasaidia kuufanya mchakato wa uboreshaji kuwa na ufanisi na kupunguza malalamiko ya wadau ni NEC kuwa na ushirikiano wa karibu na wadau hususan vyama vya siasa. Hii inatokana na kusisitiza kwamba itakahikisha vyama vyote vinapewa nakala ya daftari hilo baada ya kuhakikiwa pamoja na utaratibu wa kuvipatia nafasi ya kutoa maoni kuhusu majina ya maofisa wa uandikishaji baada ya kuteuliwa kwao.

Tunaamini pamoja na taratibu nyingine ambazo tume imeainisha kuzitumia kufanikisha mchakato huo ikiwamo kutumia vyombo vya habari, matangazo kupitia gari lake maalum litakalokuwa likipita maeneo mbalimbali nchini, semina na burudani, wananchi wengi watapata elimu na bila shaka lengo litafanikiwa. Tunaamini kuwa asasi zilizopewa jukumu la kutoa elimu wakati huu wa uboreshaji daftari zitatekeleza jukumu hilo hilo kwa kufuata sheria, kanuni, taratibu na maelekezo yatakayotolewa na tume, huku tukitarajia vyama vya siasa ambavyo ni wadau wakuu wa uchaguzi kuwahimiza na kuwahamasisha wanachama wao wenye sifa za kuandikishwa wanachangamkia fursa hiyo.


Bila shaka walengwa ambao ni wenye akili timamu, uraia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18, watajitokeza kwa wingi ili watumie haki yao ya kushiriki katika uchaguzi Oktoba mwakani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Ongezeko la kodi kwenye taulo tuwasikie wadau

**BAADA** ya kusikika kuwa kodi ya taulo za kike inaongezwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), kuna wadau wametoa maoni yao kuhusiana na ongezeko hilo.

Taulo za kike ni mkombozi, pale mwanamke au mtoto wa kike aliyefikia umri wa kuanza kujisitiri, zinamwezesha kutumia na kuwa huru katika hali ya usafi.

Imeshabainika kwamba, kutokuwapo taulo hizo za kike katika baadhi ya shule, watoto wanapojichafua wanapata changamoto na kuamua kurudi nyumbani, mpaka hapo hali yake itakapokuwa salama.

Wapo watoto ambao wanakaa nyumbani hadi siku tano hawahudhurii masomo, kwasababu kubwa ni kutokuwapo uwezo wa kupata taulo hizo.

Taulo zimekuwa zikiuzwa gharama kubwa. Kutokana na ukweli, baadhi ya wazazi hawana uwezo wa kumudu gharama hizo, hawazipati.

Kuna baadhi ya wafadhili wamekuwa wakitoa elimu ya kutumia taulo hizo na kuwapatia watoto taulo, ili waweze kuzitumia kwa ajili ya kuendelea na masomo.

Mbali na wafadhili, pia baadhi ya shule kupitia mafungu yake ya mapato zimekuwa zikitenga fedha kwa ajili ya kununua taulo za kike, lengo ni kumwezesha bintipale anapoharibikiwa, aweze kujisitiri na kuendelea na masomo kama kawaida.

Pamoja na kutengwa pesa hizo, changamoto iliyopo ni uhaba wa taulo hizo. Mtoto anpoharibikiwa, anapewa taulo moja na anaweza kukaa nayo muda mrefu. Kiafya, hiyo haitakiwa mtu kukaa nayo kwa saa nyingi.

Hivi karibuni katika semina za Jinsia na Maendeleo (GDSS) ambazo hufanyika kila wiki, baadhi ya washiriki waliweza kuzungumzia kurudishwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika taulo za kike.

Washiriki walitoa maoni yao, kuendana na kila mmoja aliyekuwa anavyotathmini kwa maono na mazingira yake.

Mwajuma Ally, ni mama anayesema kuwa taulo hizo ni mkombozi kwa wanawake na watoto waliofikia umri wa kuanza kuzitumia.

Anasema ongezeko hilo, linaweza kuwafaa zaidi wanafunzi na kinamama, mama lishe na wengine ambao wanakaa muda mrefu wakihudumia wateja katika mihangaiko yao ya kila siku, kulingana na shughuli zao.

Anasema kama ongezeko likipitishwa, uwezekano wa kinamama kurudia miaka ya nyuma kujisitiri kwa tabu itarudiwa tena.

Amina Mwinyiheri anasema, serikali iliangalie hilo, kwamba kuna shule ambazo wanapata taulo kupitia wafadhili na hali hiyo imesaidia hata mahudhurio ya watoto katika masomo, kutokana na kupata taulo za kike.

Mama huyo anasema, kuwa bei ikiongezeka wafadhili waliojitolea katika shule nao huenda wanaweza kuacha na hali hiyo ikarudisha nyuma maendeleo ya watoto shuleni, hata afya zao.

Anasema hakuna anayepinga maendeleo, lakini katika suala la taulo, kuna kila sababu ya hitaji la kungaliwa upya.

Pia, Hamis Juma, anasema ongezeko la bei litawanufaisha wazalishaji, lakini litawaumiza watumiaji, huku Zuwena Hamis, akisema kuwa taulo zikiwa za bei kunwa, changamoto itatokea kwa walio na vipato vidogo.

Anasema wapo walio na watoto wenye matatizo ya akili wanapoharibikiwa hawataki kukaa na taulo muda mrefu na kila baada ya muda anataka abadilishwe na kwa siku anaweza kubadilisha hata mara 20.

Faustina John anasema, serikali ifanye jitihada za taulo za zifike vijijini, kutokana na maduka mengi kukosa baadhi na wanakijiji hawajui umuhimu wa taulo na bado wanatumia njia zisizo salama kujisitiri.

## *Wanafunzi nidhamu yao mtihani*

**Mhariri,**

*NAOMBA niseme jambo kuhusu tabia ya mavazi ya watoto wanafunzi katika shule mbalimbali, kwamba yako katika namna inayonishangaza sana.*

*Kila nikipata wasaa wa kuwatathmini vijana hawa, wako katika mazingira ya kushangaza na wengi ni wa shule za sekondari zilizoko mijini.*

*Moja ya hayo kutoka ninayoshuhudia ni wanafunzi wengi hawavai soksi na viatu vya aina mbalimbali, hata kwa walioko katika shule moja, jambo linalonipa ujumbe kuwapo ukiukwaji mkubwa wa kanuni za sare.*

*Hilo linatokea, huku ikifahamika sare ni kipengele muhimu kwa nidhamu ya mwanafunzi awe msichana au mvulana.*

*Pili, ni kwamba hata unapokuta wamevaa soksi, hapo ndipo kuna kichekesho au mshangao inategemea fikra zako zinakoangukia.*

*Jambo la lingine mbali na hilo ninaloshuhudia kila siku ni kwamba wengi wao wanaelekea shule wakiwa wamechelewa sana, jambo ambalo nalo linaangukia tafsiri ya tatizo katika mtazamo wa nidhamu.*

*Kingine, hata mashati ya shule, wanafunzi wanayakata au wanayaunguza kwa namna ambayo haiwezi kuchomekewa, huwa najiuliza, kwa nidhamu ya namna hiyo, usafi unatokea wapi katika ulingo wa taaluma?*

*Hapo sijaingilia kati mfumo wa maisha yao, tukisikia yanatawaliwa na mengi ya kinidhamu, ikielezwa hata kutoka ushuhuda wa walimu, vijana katika sehemu kubwa ya maisha yao wanatawaliwa na mizíki na mambo yasiyohusiana na taaluma.*

*Sote kama jumuiya, wazazi, wanafunzi na walimu pia shule kwa jumla na mamlaka za kiserikali, tunakoelekea ni wapi kitaaluma?*

**Ahmed Kajundi.**
**Kibaha.**

### WASILIANA NASI:

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Jamii inavyopaswa kujiongeza katika malezi ya watoto wao




**Na Beatrice Moses**

MALEZI ya kimwili, kimaadili, kiroho na kisaikolojia yanayopaswa kutolewa kwa watoto, sasa yamegeuka mtihani mkubwa kwa wazazi, walezi, walimu na jamii kwa ujumla.

Ni hali inayochangiwa kwa kiasi kikubwa na kukosekana uelewa wa malezi ya watoto, yanayozungukwa na haki zao zinazosimamiwa na vyombo husika, pia na mwongozo wa vitabu vya kiimani.

Tunapoadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika, iliyokuwa Juni 16 ikiwa na lengo la kutambua thamani, utu na umuhimu wa mtoto duniani, tumeendelea kusikia au kushuhudia mengi kuhusu watoto, ikiwamo kushamiri ukatili dhidi yao.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) nchini, katika ripoti yake mpya iliyozinduliwa Mei 14, mwaka huu, imebainisha matukio 6,000 ya ama ukatili au unyanyasaji dhidi ya watoto, zikiwamo vinavyohusu ngono na viliripotiwa katika kipindi cha mwaka 2018.

Miongoni mwa matukio hayo ya kikatili, ni pamoja na mauaji ya watoto katika baadhi ya maeneo nchini, hasa mkoani huko mkoani Njombe hivi karibuni, hata kutoa jamii hofu.

Katika ripoti hiyo iitwayo "Ukatili wa Kingono: Tishio kwa Haki na Ustawi wa Mtoto Tanzania imebainishwa kuwa imani za kishirikina ni miongoni mwa vichocheo vya ukatili kwa watoto.

Jarida la Ulinzi na Usalama wa Mtoto, kilichoandaliwa na Shirika la World Vision Tanzania kwa ajili ya kuelimisha jamii juu ya haki, ustawi wa mtoto na wajibu wa mzazi/mlezi katika kumlea na kumlinda mtoto, linajulisha ni wajibu wetu sote.

Kuna haki za watoto zinazoainishwa katika jarida hilo, ikisema kuna watoto wengi wanaofanyiwa ukatili na unyanyasaji, hivyo kusababisha washindwe kufurahia utoto wao.

Ni hali inayotajwa kuchangia madhara makubwa kiakili, kihisia na kimwili, hivyo yasipokomeshwa, yataendeleza mzunguko wa umaskini na ukatili katika jamii na kuharibu maadili na ustawi wa jamii kwa ujumla.

Kupitia vyombo vya habari kadhaa ikiwamo mitandao ya kijamii, mwaka huu kumekuwapo kesi za ulawiti, unajisi, mauaji yanayohusu watoto.

Shirika la World Vision Tanzania linasema kuwa, kesi zote za jinai nchini zinapaswa kuripotiwa kwa Ofisa wa Polisi aliyepo katika eneo husika mara moja, ili hatua za kisheria zichukue mkondo wake.

Ni wastani wa miezi mitatu iliyopita, kuna matukio ya ukatili unaowahusu watoto, kesi zake zipo mahakamani na baadhi zimekwishapatiwa hukumu kali. Zote kwa ujumla, mtazamo mkuu ni umuhimu wa sheria kuchukua mkondo wake.

Mikasa ya kesi za namna hiyo, zimeripotiwa katika Mahakama Kuu huko Bukoba na Arusha.

Naamini kwamba, adhabu hizo ni miongoni mwa mafunzo yenye kumbukumbu mbaya kwa jamii, hivyo zinaweza kutumika kuwa kuwakumbusha kuwa umakini katika malezi ikiwamo kuhakikisha haki za watoto zinalindwa.

Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, inabainisha kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto ambapo, ikianza na ufafanuzi mtoto ni nani?

Tafsiri kuu, ni kwamba mtoto ni mtu aliye na umri chini ya miaka 18. Ustawi wa maisha yake yanapaswa kutawaliwa na furaha na amani.

Hiyo ndio kipaumbele katika kutathmini mambo yote yanayomhusu, yawe yamefanywa na taasisi ya Ustawi wa Jamii ya serikali au binafsi, Mahakama au vyombo vya utawala.

Katika kipengele cha 12 kinaelezea jinsi ya kulinda mtoto asiteswe na kudhalilishwa.

Mtu yeyote hataruhusiwa kumfanya mtoto apate mateso, au adhabu ya kikatili, ya kinyama au afanyiwe matendo yenye kumshushia hadhi.

Hii ni pamoja na desturi zozote za mila zenye kudhalilisha utu wa mtoto au zinazosababisha athari za maumivu ya mwili au akili ya mtoto.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**



# Mbunge alalamikia makato ya posho

INATOKA UK. 3

utaratibu unatumika wa kuchangisha pesa pasipo idhini yetu, naomba Mheshimiwa Naibu Spika, na naomba utoe maelekezo ya jambo hili lisifanyike tena kwa kukata pesa zetu."

Akijibu mwongozo huo, Naibu Spika Dk. Ackson, alisema hamna namna ambayo ofisi inaweza ikakata fedha bila ya wabunge kuhojiwa na hakuna utaratibu holela wa kukata fedha za wabunge.

"Waheshimiwa wabunge, Mheshimiwa Hatibu amesimama hapa akisema wabunge wamekatwa fedha, ama niseme wote tumekatwa fedha maana huwa tunakatwa wote kwa pamoja, lakini kuna utaratibu ambao umekuwa ni holela hivi kwa waheshimiwa wabunge kukatwa fedha zao.

"Jambo la msingi tufahamu kuwa hakuna fedha ambayo imewahi kukatwa bila wale watu kuwapo humu ndani wakatangaziwa, hoja ikatoka na wabunge wakahojiwa."

Kwa maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Hatibu, maelezo ambayo sisi wenyewe tukiwa tumekaa humu ndani, hamna namna ambayo ofisi inaweza ikakata fedha bila ya wabunge kuhojiwa, hakuna utaratibu holela wa kukata fedha za wabunge."

"Kwa hiyo hakuna namna ambayo ofisi inaweza ikakata fedha pasipo ridhaa ya wabunge kuhojiwa kwa hiyo, mazingira ambayo Bunge hili tangu lianze limewahi kuchangia ni pale ambapo yupo mbunge ambaye ametoa hoja na bunge likahojiwa na watu waliosema ndiyo wakawa wengi," alisema Dk. Tulia.

# Muhimbili kupandikiza uloto

INATOKA UK. 2


takribani 130 hadi 140 wanahitaji huduma ya kupandikizwa uloto kwa mwaka na zaidi ya theluthi mbili ya wagonjwa hao hufariki dunia kwa kukosa huduma hiyo," alisema Dk. Swai.

Alisema uwepo wa huduma hiyo utasaidia wananchi wengi kutibiwa hapa nchini, kujenga uwezo kwa wataalamu wa ndani na kupunguza mzigo kwa serikali kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwa kuwa gharama zitashuka kufikia kiasi cha chini ya asilimia 50 kwa mgonjwa mmoja.

Dk. Swai alisema wataalamu hao wanatarajia kurejea nchini mwishoni mwa Julai, 2019 tayari kuanza maandalizi ya mwisho ya kutoa huduma hiyo mwishoni mwa mwaka huu (2019).

Aidha, alisema gharama za kupeleka wataalamu hao kwenye mafunzo ni Sh. milioni 91 zikijumlisha gharama za mafunzo, nauli, fedha za kujikimu pamoja na gharama nyingine za mafunzo. Fedha hizi zote zitalipwa na Hospitali ya Taifa Muhimbili ili kujenga uwezo wa wataalamu wake.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Magonjwa ya Damu MNH, Dk. Stella Rwezaure, alisema kuna wagonjwa ambao wana tatizo la mifupa yao kushindwa kutengeneza chembechembe za damu, hivyo inabidi asaidiwe kwa kupatiwa tiba ya saratani na baada ya hapo kumuoteshea uloto kutoka kwa ndugu yake.



Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Faraji Kasidi Mnyepe, akimsikiliza Mwakilishi wa Kaimu Balozi wa Marekani hapa nchini Ann Marie Warmenhoven – Tilias alipomwita wizarani jijini Dar es Salaam jana, kutoa ufafanuzi kuhusu angalizo la kiusalama lilitolewa na ubalozi huo, kupitia tovuti ya Ubalozi wa Marekani hapa Nchini. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

# Wakurugenzi waburuzwa kortini

INATOKA UK. 4

na kuutumia kununua kitabu cha zabuni na kukirejesha kikiwa kimeambatanishwa nyaraka za kughushi, hivyo kuwezesha kampuni hizo kushinda zabuni hiyo na kutia saini mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi Januari, 2018.

Kutokana na mkataba huo, alidai kuwa halmashauri ilizilipa kampuni hizo malipo ya awali ya asilimia 15 ambayo ni Sh. 270,687,141.45.

Alidai kuwa watuhumiwa hao baada ya kulipwa kiasi hicho cha fedha, walitekeleza kazi ya mradi huo kwa kusuasua hali iliyosababisha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mufindi kuvunja mkataba huo Aprili, mwaka huu. Mkuu huyo wa Takukuru alidai kuwa watuhumiwa hao walisomewa mashtaka hayo juzi katika Mahakama ya Wilaya ya Mufindi na Mwendesha Mashtaka wa Takururu, Maria Mwakatobe.

Sambamba na kushtakiwa huko, alidai kuwa uchunguzi unaendelea dhidi ya watumishi waliohusika kufanikisha watuhumiwa hao kupata zabuni na kutia saini mkataba kwa kutumia nyaraka za kughushi.

# Balozi Marekani aitwa kujieleza

INATOKA UK. 2

kuwa na hofu, hizi ni tahadhari za kawaida ambazo zinatokea.

"Hizi ni tahadhari za kawaida kama ambavyo tunavyotoa tahadhari za Tsunami, mvua nyingi... hii ni tahadhari ya kiusalama ya kawaida ambayo Watanzania hawapaswi kuwa na wasiwasi, serikali yao chini ya Rais Magufuli ipo imara," Lugola alisisitiza.

Alisema wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Rais Magufuli aliwaahidi Watanzania kwamba serikali itahakikisha nchi inaendelea kuwa na amani, usalama wa wananchi na mali zao na ahadi hiyo inatekelezwa.

Nipashe ilipita katika maeneo ya Masaki yaliyotajwa kulengwa katika tishio hilo la ugaidi na kukuta wananchi wakiendelea na shughuli zao, huku baadhi yao wakiwa hawana hata taarifa za tahadhari hiyo.

Athuman Mohamed, mkazi wa Masaki, alipoulizwa na mwandishi kuhusu tahadhari hiyo, alisema hakuwa na taarifa za tishio hilo, lakini akasisitiza atachukua tahadhari ya kuepuka mikusanyiko ambayo mara nyingi hulengwa katika matukio ya kigaidi.

Katika taarifa yake, Ubalozi wa Marekani nchini umeyataja maeneo yanayolengwa kuwa ni pamoja na hoteli na migahawa ambayo hutembelewa na watalii likiwamo eneo maarufu la maduka ya Slipway.

"Ubalozi hauna ushahidi wa moja kwa moja wa tishio hilo ama taarifa za muda gani mashambulizi yatatokea. Hata hivyo, unawaonya wananchi kuchukua tahadhari," ilielezwa katika taarifa hiyo ya ubalozi huo.

Ubalozi huo pia uliwataka wananchi kujiepusha na makundi na kufuatilia taarifa kupitia vyombo vya habari.

Mwaka 1998, ikiwa ni miaka 21 sasa, wapiganaji wa Jihadi walishambulia kwa pamoja Balozi za Marekani za Kenya na Tanzania.

Agosti 7, mwaka huo, saa 4:30 asubuhi, wakati magaidi wawili walilipua lori moja lililokuwa limejaa mabomu mbele ya Ubalozi wa Marekani mjini Nairobi nchini Kenya, dakika tisa baadaye bomu lingine lililipuka katika Ubalozi wa Marekani mjini Dar es Salaam.

Takriban watu 242 waliuawa katika mashambulizi hayo mawili yalioharibu kwa kiwango kikubwa balozi hizo za Marekani na kusababisha kuporomoka kwa nyumba zilizokuwa karibu.

# Wasira afunguka kudaiwa Hazina

INATOKA UK. 3

**JINSI AVYOLIPA**

Wasira ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Sera, Uratibu na Bunge, alisema awali walikuwa wamempangisha Mzindakaya kwenye moja ya majengo yao na mteja wao huyo hakuweza kulipa kodi kwa kipindi cha miaka mitano, hivyo wakawa wanamdai Sh. milioni 186.

Alisema walipotaka kumfukuza, TIB ilimkingia kifua na kuwaeleza kuwa itamlipia deni hilo kwa sababu alikuwa ni mteja wake.

Waziri huyo wa zamani wa maji aliongeza kuwa baadaye kampuni yake ilifanya kikao na Mkurugenzi Mkuu wa TIB aliyekuwapo kwa wakati huo, Peter Noni, ambaye aliwaeleza kuwa endapo watahitaji kulipwa fedha wanazomdai Mzindakaya, wanatakiwa kuandika barua ili TIB nao wakate deni lao walilokuwa wakiwadai.

"Mteja tuliyekuwa tukimdai alikuwa ni Mzindakaya, na tulikuwa tumempangisha na hakulipa kodi kwa miaka mitano. Tulipotaka kumfukuza, TIB wakamkingia kifua wakisema watalipa kwa sababu alikuwa ni mtejaa wao.

"Baadaye tulifanya kikao na Managing Director wa TIB aliyekuwapo, anaitwa Peter Noni, akatuambia 'condition' ya sisi kulipwa deni la Mzindakaya kupitia TIB ni sisi kuandika barua ili wakate sehemu ya deni lililobakia," alisema.

Wasira ambaye pia aliwahi kuwa Waziri wa Kilimo na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), alisema walilazimika kuandika barua ambayo iliiruhusu TIB kukata deni walilokuwa wakidai na walilipwa Sh. milioni 160.

"Hiyo Sh. milioni 26 iliyobaki, ndiyo ilikuwa ni 'balance', tukaandika barua tukawaruhusu wakate, matarajio yetu ni benki ikate deni lake kwa sababu deni tulilokuwa tunamdai Mzindakaya lilikuwa ni Sh. milioni 186, 'balance' waliyotulipa benki ilikuwa ni milioni 160. Kwa hiyo, tulijua walikata Sh. milioni 26 walizokuwa wakitudai," Wasira alisema.

Aliongeza kuwa alipokuwa akifuatilia benki kuhusu kumaliza deni hilo, alikuwa anaelezwa kuwa kwenye rekodi zao hazionyeshi kama deni limelipwa.

"Lakini wenyewe tena wanasema haziko kwenye rekodi za benki, nilipokwenda kuzungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa sasa, alikiri kwamba huku nyuma kulikuwa na wizi wizi.

"Kwa hiyo, madeni yenyewe ni ya miaka ya nyuma, yawezekana walipokata deni lao la Sh. milioni 26 badala ya kuingiza kwenye rekodi zao, wakaweka kwenye mifuko yao," Wasira alisema.

Wasira alisema aliwaeleza TIB kuwa kama nyaraka zinazoonyesha deni kulipwa hawazitambui, basi suala hilo lifikishwe katika mahakama ili likaamuliwe huko.

Alisema wanazo nyaraka zote zinazoonyesha deni hilo kulipwa pamoja na mawasiliano ya email waliokuwa wanayafanya na benki husika.

HABARI KITAIFA

# Watumishi TRA kortini, wakosa dhamana

**Na Alphonce Kabilondo,**
GEITA

WATUMISHI wawili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Geita, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita, wakikabiliwa na makosa ya kuomba na kupokea rushwa.

Wanashtakiwa chini ya sheria na kifungu cha 15 (1) (a na b) namba (2) cha sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa namba 11 mwaka 2017, huku mshtakiwa Amza Rugemalira akiendelea kutafutwa.

Washtakiwa waliofikishwa mahakamani juzi ni Sadick Kassim Lutenga na Elias Samwel Msula.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri, alidai mshtakiwa wa kwanza na wa pili wakiwa katika utekelezaji kwa pamoja walimuomba rushwa mfanyabiashara, Alphonce John Maringo, ya Sh. milioni 30 ili waweze kumfanyia makadirio ya chini ya kodi.

Mwendesha mashtaka huyo aliendelea kudai kuwa washtakiwa hao wa kwanza na wa tatu waliomba Sh. milioni 75 kutoka kwa Bertha Charles Magadula na Makoye Athumani Shiyunga ambao ni wakurugenzi wa Makoye Hospitali, na kwamba mnamo Aprili 8, mwaka huu, washtakiwa hao kwa pamoja walipokea Sh. milioni 50.

Alidai kuwa mshtakiwa wa kwanza Juni 14, mwaka huu, anadaiwa kupokea Sh. milioni 10 kutoka kwa Alphonce John Maringo ikiwa ni sehemu ya rushwa ya Sh. milioni 30.

Hata hivyo, kutokana na mvutano wa kisheria kati ya wakili wa Takukuru na upande wa utetezi ukiongozwa na wakili wa utetezi, John Rwabuhanga, aliomba ufafanuzi wa marekebisho ya Sheria ya Uhujumu Uchumi namba 3 ya mwaka 2016 inayofafanua kuwa makosa ya rushwa yanaangukia katika uhujumu uchumi.

Hali hiyo iliibua mabishano, huku wakili huyo wa utetezi akiomba mahakama iwape dhamana wateja wake, lakini ombi hilo likapingwa na wakili wa Takukuru Murusuri, ambaye aliiomba mahakama washtakiwa waendelee kukaa mahabusu kwa kuwa ushahidi wa shauri hilo haujakamilika. Murusuri aliieleza mahakama kuwa kutokana na uzito wa shauri hilo mahakama hiyo haina mamlaka ya kutoa dhamana kwa washtakiwa, kwa kuwa Mahakama Kuu ndiyo yenye mamlaka hayo.

Hakimu wa Makama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita, Jovit Kato, aliiahirisha kesi hiyo kwa muda saa 6:55 mchana kupitia vipengele vya kisheria na baadaye kuendelea tena na shauri hilo saa 8:35 mchana.

Wakili Rwabuhanga baada ya mahakama kuahirishwa kwa muda na kurejea kuendelea, aliendelea kuomba dhamana kwa wateja wake kwa madai kuwa wanashtakiwa kwa makosa ya uhalifu.

Wakili mwingine wa utetezi, Renatus Malecha, alidai kutokana na kifungu cha 148 (1) ibara ya 3 kifungu cha 6 sheria ya mwaka 2016 inaonyesha kuwa makosa hayo yameondolewa kwenye makosa yasiyo nadhamana.

Washtakiwa hao wamekana mashtaka yao na wamerudishwa mahabusu.

Hakimu Katto baada ya mtifuano mkali wa hoja za kisheria, aliaahirisha kesi hiyo hadi Julai 2, mwaka huu, ambapo hatima ya dhamana itajulikana.




Baadhi ya wananchi wenye mashamba katika bonde la kilimo la Buswelu, wilaya Ilemela jijini Mwanza, wakionyesha kwa waandishi wa habari alama za mipaka 'beacon' zilizowekwa ili kutenganisha eneo la makazi na kilimo. Upimaji wa kugeuza eneo hilo kutoka bonde la kilimo kuwa makazi unaendelea. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Kampuni 384 za mawakala forodha zapewa siku saba

**Na Beatrice Moses**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imetoa onyo na kutoa siku saba kwa kampuni 384 za mawakala wa forodha wanaoshughulikia mizigo inayopita Tanzania kwenda nchi jirani, kujisalimisha kwa kutoa maelezo yenye ushahidi wa kuvuka kwa mizigo waliyoishughulikia.

Agizo hilo lilitolewa na Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa, Usaje Asubisye, katika taarifa kwa umma kupitia vyombo vya habari.

Alieleza kuwa mawakala hao wa forodha ambao majina ya makampuni yao yameorodheshwa kwenye taarifa walitakiwa kutoa maelezo na ushahidi wa kuvuka kwa mizigo inayowahusu kwenda nchi jirani.

"Mnakumbushwa kulipa uzito jambo hili kwani kushindwa kufika kwa mizigo inayopitia nchi jirani itakuwa ni kuhujumu mfumo wetu wa kodi na ukwepaji kodi," alieleza Asubisye katika taarifa yake hiyo.

Mawakala hao wameonywa kuwa kushindwa kutimiza maagizo hayo, watasababisha kampuni zitakazothibitika kuhusika na hujuma hizo zitachukuliwa hatua kali za kisheria.

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, alisema mizigo hiyo iliingizwa kwa kipindi tofauti tofauti, wahusika wamepewa nafasi ya kuwasilisha vielelezo vyao. "Hatuwezi kuwachukulia hatua bila kuwapa nafasi ya kujieleza, ndiyo maana TRA tumewaita ili wajieleze ndipo uamuzi utatolewa kwa mujibu wa sheria kwa wale watakaobainika kufanya hujuma mojawapo ya adhabu ni kufungwa kwa kampuni husika," alisema Kayombo.

Baadhi ya taratibu zinazopaswa kufuatwa wakati wa kuingiza bidhaa nchini ni mwingizaji bidhaa kutakiwa kumteua wakala wa kupokea na kusafirisha mizigo mwenye leseni ili aweze kupokea/kukomboa bidhaa zake.

Orodha ya wakala wa kupokea na kusafirisha mizigo mchakato wa kuandikisha unafanyika mtandaoni kupitia Mfumo wa Pamoja wa Forodha Tanzania (TANCIS) kwa upande wa Tanzania Bara na mfumo wa ASYCUDA ++ kwa upande wa Zanzibar.

# Onyo kali la NEMC kwa kumbi starehe, nyumba ibada

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeagiza wamiliki wote wa kumbi za starehe, baa pamoja na nyumba za ibada kuhakikisha wanadhibiti uchafuzi wa kelele katika maeneo ambayo ni makazi ya watu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema NEMC imepokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi sehemu mbalimbali nchini kutokana na kushimili kwa kelele na mitetemo chafuzi.

"Tumepokea malalamiko kutoka kwa wananchi mbalimbali juu ya kelele na mitetemo chafuzi zinazotoka katika maeneo ya kumbi za starehe, baa pamoja na nyumba za ibada," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na kanuni zake zinakataza uwapo wa kelele na mitetemo chafuzi.

Sheria na kanuni hizo zinakataza uwepo wa kelele na mitetemo chafuzi, hivyo ni vyema shughuli hizo zikaendeshwa katika maeneo yaliyorasimishwa au katika majengo yaliyojengwa katika muundo wa kudhibiti sauti zisitoke nje na kuwa kero kwa wananchi wa eneo husika, alisisitiza Dk. Gwamaka.

Hata hivyo, NEMC imebaini kuwa tatizo hilo limechangiwa na kumbi hizo, baa pamoja na nyumba za ibada kujengwa kwenye makazi ya watu

Agizo hilo liliungwa mkono na baadhi ya wananchi waliozungumza kwa nyakati tofauti kuonyesha kukerwa na uchafuzi huo wa kelele katika maeneo ya makazi hususani kwa nyakati za usiku.

"Binafsi naunga mkono tamko hili la NEMC kwa kuwa limekuja katika wakati ambao linauhitaji kwa wananchi kwani tumekuwa tukiathirika na uchafuzi wa kelele hususani kwa mikesha ya miziki na ibada zinazofanyika katika maeneo ya wazi ambayo pia ni makazi ya watu, alisema Yasini Mbalami, mkazi wa Mbagala Kuu.

Mohammed Twaha, mkazi wa Kigamboni, licha ya kupongeza tamko hilo la NEMC, alisema limechelewa kutolewa kwa kuwa maeneo mengi yamekuwa yakiathirika na kelele hizo zinazotokana na ala za muziki kutoka kwenye kumbi za starehe.

"Huku mitaani hali ni mbaya, kumbi za starehe na wakati mwingine ni maeneo ya wazi imekuwa ni wazalishaji wakubwa wa uchafuzi wa kelele, hali inayotufanya tushindwe kulala vizuri hasa kwa wakati wa usiku," alisema Twaha.

NEMC imefanunua kuwa tamko hilo halihusu ibada fupi kama vile adhana misikitini, kengele za kanisani ambazo huita waumini kwenda kufanya ibada za muda mfupi.

# Sababu za kuchelewa uwekezaji miradi mikubwa zawekwa wazi

SERIKALI imetoa sababu za kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa miradi mikubwa ya uchimbaji wa makaa ya mawe wa Mchuchuma na uchimbaji wa chuma wa Liganga.

Serikali imesema hali hiyo imetokana na mwekezaji kutaka kupewa vivutio vya ziada ambavyo havipo kisheria.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya, amesema changamoto iliyojitokeza ni majadiliano kati ya mwekezaji na serikali kuhusu vivutio vya uwekezaji kuchukua muda mrefu. Mhandisi Manyanya alikuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Lucia Mlowe, aliyehoji serikali imekuwa ikitoa ahadi juu ya uanzishwaji wa mradi wa Mchuchuma na Liganga wakati ambapo wananchi wamekuwa na hamu sana na mradi huo, je, ni lini sasa mradi huo utaanza?

"Hivyo serikali inaangalia njia bora ya kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kwa tija ili kuleta manufaa mapana kwa wananchi wa eneo hilo na taifa kwa ujumla," akisema na kuendelea:

"Serikali inafahamu umuhimu wa mradi huu katika ujenzi wa uchumi, hatua za awali za ujenzi wa mradi zimekwishaanza kutekelezwa. Hatua hizo ni pamoja na kufanya upembuzi yakinifu, kupata cheti cha mazingira kwa miradi inayotekelezwa, kujenga barabara kuu ya lami, ili kurahisisha usafirishaji wa mitambo na huduma nyingine katika eneo la mradi, kufanya uthamini wa mali na maeneo ya wananchi watakopisha mradi."

Baada ya majibu hayo, Mlowe aliuliza swali la nyongeza akihoji kama haiwezekani serikali ikambadilisha mwekezaji huyo ili miradi hiyo iweze kuanza kwa kasi, ambapo Manyanya alieleza kuwa serikali itamwondoa mwekezaji huyo kama hawataafikiana.


Kuhusu wananchi wa Ludewa na Mkomang'ombe ambao waliondolewa katika eneo hilo kupisha mradi huo, Manyanya alifafanua kuwa wizara hiyo inaendelea kufuatilia madai hayo na italipa fidia wananchi hao kulingana na mafungu ya kibajeti.

Mei 14 mwaka huu, aliyekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda, aliliambia Bunge kuwa mipango yote ikiwamo ulipaji wa fidia kwa wananchi utafanyika kabla ya mwaka wa fedha 2018/19 kumalizika Juni 30. Hata hivyo, Waziri wa Viwanda na Biashara kwa sasa ni Innocent Bashungwa. Kwa mujibu wa wizara hiyo, mkataba wa mwekezaji ulikuwa na vipengele ambavyo vingeitia hasara kubwa serikali kama ingepitishwa kama ilivyo ikiwamo hasara ya dola milioni 19.88 kwa Liganga pekee.



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akipokea zawadi toka kwa Balozi wa Tanzania nchini Misri, Meja Jenerali, Issa Suleiman Nassor, wakati alipotembelea jana Ubalozi wa Tanzania nchini Misri. **PICHA: BUNGE**

# Soko mbadala la mbaazi latafutwa




**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

KUTOKANA na kutokamilika kwa mkataba wa makubaliano kati ya Tanzania na India kuhusiana na soko la mbaazi, serikali imesema inaendelea kutafuta masoko mbadala ambayo mazao jamii ya mikunde yatauzwa.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya alisema tayari nchi ya Malawi imeonyesha uhitaji wa tani 7,000 za mbaazi.

Alikuwa akijibu swali la Mbunge wa Liwale (CCM), Zuberi Kuchauka, aliyesema kwa kuwa kumekuwa na tatizo la muda mrefu la ukosefu wa soko kwa mazao ya jamii ya kunde kama mbaazi na choroko, ni nini kauli ya serikali juu ya kutatua tatizo hilo.

"Mwezi Machi 2019, serikali ilifanya ziara ya kutafuta soko la mazao jamii ya mikunde katika nchi jirani za Malawi, Burundi, DRC na Zambia. Kutokana na ziara hiyo, Malawi kwa mwaka 2019 imeonyesha uhitaji na taratibu za kuhakikisha oda hiyo inatekelezwa zinaendelea kufanyiwa kazi," alisema Manyanya.

Katika majibu yake kuhusu nini mkakati wa serikali juu ya kuongeza thamani kwa mazao hayo ili kuimarisha masoko, Naibu Waziri huyo alisema mkakati wa serikali uliopo ni kuendelea kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kukoboa na kuongeza thamani kwa mazao jamii ya mikunde nchini.

Kutokana na jitihada za serikali za kushawishi uwekezaji katika viwanda vya kuchakata na kusindika mazao jamii ya mikunde nchini, Kampuni ya Mahashree Agro Processing Limited kutoka India inajenga kiwanda mkoani Morogoro.

Kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuchakata na kusindika tani 700,000 za mazao jamii ya mikunde kwa mwaka.

Kwa mujibu wa Mhandisi Manyanya, kiwanda hicho kinatarajia kuanza uzalishaji mwezi Julai mwaka 2019.

Vile vile, viwanda vingine vilivyojengwa na vinavyofanya kazi ni pamoja na kiwanda cha Quality Pulse Exporters Limited kilichopo Dar es Salaam (SEZ) na kiwanda cha Samon Agro Export Limited (SEZ industrial Park).

## Makandarasi wabanwa zaidi

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, imepigilia msumari uamuzi wa halmashauri za wilaya nchini kutoa adhabu ya kuwakata fedha za fidia makandarasi wanaochelewesha miradi, huku ikitaka pia zisitishe mikataba ya kazi kwa makandarasi hao.

Wito wa kutaka kufanya hivyo, ulitolewa jana na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Elias Kuandikwa.

Kuandikwa alikuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Kilolo (CCM), Venance Mwamoto, aliyetaka kujua ni adhabu gani anastahili kupewa mkandarasi anaposhindwa kumaliza mradi wowote kwa wakati kwenye halmashauri.


"Inapobainika kuwa mkandarasi ameshindwa kumaliza kazi yake kwa wakati bila sababu za msingi, mwajiri (zikiwamo halmashauri), huchukua hatua za kimkataba ikiwa ni pamoja na mkandarasi kukatwa fedha za fidia ya kuchelewesha mradi yaani liquidated damages.

"Mkataba kusitishwa au mkandarasi kunyang'anywa sehemu ya kazi, aidha Bodi ya Usajili wa Makandarasi pia kuchukua hatua la kumshusha daraja la usajili au kampuni kufutiwa kabisa usajili." Kwa mujibu wa Kuandikwa, adhabu nyingine ni kusitishwa kupewa kazi za ujenzi kwa muda fulani kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA).

Zaidi alieleza kuwa, miradi ya ujenzi nchini inafanywa na makandarasi waliosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), kwa mujibu wa sheria na taratibu za usajili kwenye madaraja mbalimbali. Mikataba ya kazi kwa makandarasi hutolewa kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake za Mwaka 2011, ambapo baada ya kushinda zabuni mkandarasi husaini mkataba tayari kwa hatua ya kutekeleza kazi hiyo.

CRB imeshaweka wazi kwamba itawafutia usajii wao, makandarasi wasiokuwa na sifa.

Mei 24, 2019, Msajili wa CRB, Rhoben Nkori, alisema wameona ni wakati mwafaka wa kuchukua hatua hiyo ili kubaini makandarasi waliopoteza sifa, kutokana na kukithiri kwa malalamiko ya kutofanya kazi zao kwa viwango stahiki.






Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, akimkabidhi Mwenge wa Uhuru Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, baada ya kukamilisha mbio zake kwenye halmashauri saba za Mkoa wa Manyara, jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Barabara Bagamoyo, Mombasa yapewa kipaumbele cha EAC

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TANZANIA imewasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Jumuiya Afrika Mashariki (EAC), na kuitangaza Barabara ya Bagamoyo Mombasa kuwa ni kipaumbele.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiao wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, jana aliwasilisha bajeti hiyo ya Dola milioni 111 takribani Sh.bilioni 249 kwa ajili ya mwaka 2019/2020 katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA), jijini Arusha.

Akisoma bajeti hiyo Dk. Ndumbaro, alisema kipaumbele kikubwa katika bajeti hiyo ni kuimarisha miundombinu ya barabara akitaja ile ya Bagamoyo hadi Mombasa nchini Kenya, itakayoambaa kandokando ya Bahari ya Hindi.

Aidha, vipaumbele vingine ni ujenzi wa barabara na reli kati ya Tanzania, Burundi na Uganda, kwa mujibu wa maelezo yake.

Alisema lengo la kuboresha miundombinu ni kuwezesha wafanyabiashara wa nchi za Afrika Mashariki (EAC) kusafirisha bidhaa bila usumbufu.

Aidha, alisema katika eneo la kilimo kwa mara ya kwanza bajeti hiyo, imetenga fedha za sekta hiyo ili kuhakikisha nchi hizo zinakuwa na chakula cha kutosha na kuondokana na njaa.

"Tunafahamu miundombinu imara hujenga uchumi imara, wanachama wanapokuwa na chakula cha kutosha hawawezi kupata changamoto za njaa."

Alisema ujenzi wa miundombinu na suala la kilimo limepewa kipaumbele katika makadirio ya bajeti ya mwaka huu.

Naibu Waziri, alisema bajeti hiyo haijasahau usalama, amani na utawala bora kwani wanachama wamesisitiza kujenga uwezo wa kila nchi mwanachama wa jumuiya hiyo ili aweze kujisimamia kikamilifu katika uchaguzi wake mwenyewe. "Katika jumuiya tunapenda uchaguzi uwe na waangalizi wa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na katika kutekeleza hili tutaanza na mwakani katika uchaguzi wa Burundi na utafuata wa Tanzania," alisema Naibu Waziri. Alidha, alisema kwenye usafiri wa anga, bajeti imegusia eneo la usafirishaji wa ndege kwa nia ya kupunguza gharama za tiketi za ndege na kuondoa urasimu wa nchi moja kutoza nchi nyingine, ili abiria wasafiri kwa urahisi ndani ya EAC.

Aliongeza kuwa bajeti hiyo ni ongezeko la asilimia 10 ya ile ya mwaka uliopita na inatokana na michango ya nchi wanachama wa Burundi, Rwanda, Tanzania, Kenya, Uganda na Sudan Kusini, ambapo wanachama watachangia asilimia 52 na wafadhili asilimia 48. Aidha, Mbunge wa Afrika Mashariki kutokea Tanzania, Adam Kimbisa, aliisifu kwa kutoa kipaumbele kwenye miundombinu ya barabara ambayo ni muhimu kwa uchumi wa taifa lolote duniani.

"Kama hatuwezi kuunganisha reli au bababarabara na kuwa na umeme unaopatikana kwa uhakika na bei nafuu tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu, hivyo hili kwetu limepewa kipaumbele," alisema.

Aliongeza kuwa ujenzi huo utarahisisha ufanyaji biashara, zinazoingia au zinazotoka, kwa sababu miundombinu itakuwa imekamilika.

Kwa upande wake, Fatuma Ally, mbunge kutoka Kenya alisema anapata hofu ya wafadhili kutochangia bajeti hiyo kama wanavyotarajia.

Aidha, alisema baadhi ya nchi wanachama hawajawasilisha michango au wanafanya hivyo kwa kusuasua. Alisema Sudan Kusini haijawasilisha michango yoyote tangu ijiunge na jumuiya hiyo Katika bajeti hiyo Jumuiya ya Afrika Mashariki imetengewa Sh. bilioni 117.7, Mahakama ya Afrika Mashariki (EACLA) bilioni 9.3, Bunge bilioni 43, Bonde la Ziwa Victoria (LVB) bilioni 30 na Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki (EASTECO) itapata bilioni 4.3. Tume ya Kiswahili ya Afrika Mashariki yenye makao yake makuu Zanzibar imetengewa bilioni tatu.

# Mamlaka yaongeza bei ya maji Babati

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Babati (Bawasa), imepandisha bei ya maji na kufikia Sh. 2,175 kwa uniti moja ili kukarabati miundombinu chakavu.

Hatua hiyo inachukuliwa kwa sababu licha ya miundombinu hiyo kutumika, haijawahi kukarabatiwa tangu wakati wa uhuru, hali inayoathiri utendaji kazi wa mamlaka.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Bawasa, Mhandisi Iddy Msuya, wakati akizungumza na wanahabari ofsini kwake, kuhusu bei mpya ya maji. Alisema bei ya maji haiongezeki kiholela, ila inabadilishwa kwa maelekezo ya serikali na kwamba Bawasa walifuata taratibu.

"Wakala wa Usimamizi wa Nishati na Maji (Ewura), uliongeza bei kwa asilimia 36, ambapo kwa uniti moja (lita 1,000), wateja wanatakiwa kulipia Sh. 2,175 ila sisi tulitaka tuongeze zaidi ya hapo," alisema Msuya.

Bei iliyoongezeka ina nia ya kuwafikishia maji wakazi wa Babati kwa muda wa zaidi ya saa 20 kwa kila siku, kwa mujibu wa maelezo yake.

"Kuongezeka kwa bei ya maji kunatuwezesha kukarabati miundombinu chakavu, iliyojengwa tangu uhuru kama iliyoko Kitintale na pale Maisaka. Pia tunakimbizana ili tufikie asilimia 95 za upatikanaji wa maji, ifikapo mwaka 2020 kwa mijini kama ilani inavyosema," alifafanua mhandisi huyo. Alisema licha ya kujitokeza malalamiko juu ya bei ya maji ongezeko la Sh. 475 lilihitajika ili kuboresha huduma kama umeme kukatika wanatakiwa maji yaendelee kutoka kwa saa sita. Wateja wa maji waliozungumza na Nipashe, walisema upatikanaji wa maji ni wa kuridhisha kwa sasa, tofauti na zamani kipindi cha mgao na kuwa Bawasa wasife moyo na malalamiko ya binadamu, wachape kazi maana wananchi wote hawawezi kuridhika.

Mkazi wa Negamsi Laurian Godfrey alisema wakati mwingine watu wanalaumu Bawasa ila hawajui gharama wanazotoa kukarabati miundombinu, huku akiirushia lawama Tanesco kwa kukata umeme na Bawasa kushindwa kutoa huduma.

## TCRA Arusha yawataka wananchi kusajili simu

**Allan Isack,** ARUSHA

MAMLAKA ya Mawasiliano nchini (TCRA), imewataka wakazi wa Arusha, kujitokeza kwa wingi kusajili laini za simu, kwa mfumo wa kielektroniki unaotumia dole gumba.

Akizungumza na wanahabari, Kaimu Mkuu wa TCRA, Kanda ya Kaskazini, Imelda Salum, alisema kutokana na umuhimu wa usajili wa laini za simu kwa mfumo huo, ni vema kila mwananchi kutumia fursa hiyo na kwa wakati.

Alisema katika kuelekea maadhimisho ya Siku ya Utumishi wa Umma, mamlaka hiyo kwa kushirikiana na kampuni za simu nchini, itatoa huduma hiyo kwa siku tano kwa wakazi wa Jiji la Arusha.

Alisema awali huduma hiyo ilitolewa kwa muda wa siku mbili, kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Uhasibu Arusha (IAA), na siku tatu kwa wateja wa Jiji la Arusha.

Aliongeza kuwa usajili huo waliufanya kwa pamoja na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) na Idara ya Uhamiaji.

Alisema mwitikio wa wananchi ni mkubwa na uongozi wa mamlaka ya mawasiliano hiyo, ulitumia vyombo vya habari kuwaelimisha wananchi kujitokeza kwenye usajili.

Aidha, alitoa rai kwa Wanaarusha, kutumia fursa hiyo ili kukamilisha usajili huo ambao hauna gharama yoyote.

"Niwaombe wananchi kutokusubiri hadi kufikia karibu na mwisho wa usajili kwa sababu huenda kwa kipindi hicho watu wengi wakajitokeza hata wengine wakakumbana na changamoto zitokanazo na kuwapo kwa idadi kubwa ya watu," alisema Salum.

Aliitaja changamoto iliyojitokeza kwa upande wa Nida, kuwa ni kundi kubwa la watu ambao bado hawajaandikishwa na kupata namba za vitambulisho, hivyo aliwashauri kuongeza vitendea kazi na mashine, ili kuendana na kasi ya watu watakaojitokeza.

Ofisa Usajili wa Vitambulisho vya Taifa, kutoka Mamlaka ya Nida, Julieth Raymond, alisema kuwa ili wananchi waweze kukamilisha usajili huo lazima wawe na vitambulisho vya taifa au namba ya kitambulisho cha taifa.

Alisema mamlaka hiyo, katika kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Utumishi wa Umma, walifika kwenye maeneo hayo kutoa huduma kwa wananchi ambao hawakubahatika kufikiwa na huduma hiyo.





# 150 wajifungua maeneo yaliyopigwa marufuku

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

WANANCHI wa vijiji vya Mowo na Lyakombila katika kata ya Kimochi wilayani Moshi Vijijini, wameeleza kuwa wako hatarini kiafya kutokana na zahanati yao ya kijiji kutokuwa na uwezo wa kuhudumia wagonjwa.

Imeelezwa kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2014 hadi sasa, takriban wajawazito 150 katika vijiji hivyo wamejifungua wakiwa kwenye maeneo yasiyo rasmi, ikiwa ni pamoja na nyumbani, kwenye magari na mashamba ya kahawa baada ya kupata uchungu.

Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imeshapiga marufuku wajawazito kujifungua nje ya vituo vya afya ikiwa ni sehemu ya mikakati yake ya kupunguza vifo vya uzazi ambavyo bado ni changamoto kubwa nchini.

Mariam Mchomvu na Maria Machenje, wakazi wa kijiji cha Mowo, kwa nyakati tofauti jana, waliiambia Nipashe kuwa waliomba serikali kuhakikisha zahanati hiyo inatoa huduma zilizokusudiwa ili kuepusha vifo visivyo vya lazima.

"Zahanati yetu imejengwa kisasa, lakini tangu kufunguliwa mwaka 2014, haina uwezo wa kumsaidia mwanamke kujifungua wala kutoa chanjo za mara kwa mara, tunaomba serikali itusaidie katika hili," Mchomvu alisema.

Nipashe ilifika katika zahanati hiyo na kuzungumza na mmoja wa watoa huduma ambaye aliomba hifadhi ya jina lake, akikiri haina vifaa muhimu.

Alisema zahanati haitoi chanjo muhimu kutokana na kutokuwa na hifadhi nzuri ya chanjo, hivyo chanjo inazopokea kuharibika mara kwa mara.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Elikana Malisa, pia alikiri kuwapo kwa changamoto ya wajawazito kujifungua nje ya vituo vya afya na kuhatarisha maisha yao na watoto.

Alisema zahanati hiyo inayotegemewa na wananchi 3,609, licha ya kuwa na miundombinu ya kisasa, haina huduma ya umeme ambayo waliomba tangu mwaka 2012.

Akizungumza na Nipashe kuhusu changamoto za zahanati hiyo, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Moshi Vijijini, Dk. Alex Kazura, alisema zinachagizwa na upungufu wa watumishi wilayani humo.

Alibainisha kuwa kwa sasa, sekta ya afya wilayani mwake inakabiliwa na upungufu wa watumishi 804, akieleza kuwa mahitaji ni watumishi 1,119 na waliopo ni 315.

Alisema mikakati ya kutatua changamoto hiyo inaendelea kwa kuikumbusha serikali kupeleka watumishi.

Dk. Kazura alisema atafuatilia kwa karibu kutatua changamoto zinazoikabili Zahanati ya Mowo kwa kuwa hajapewa taarifa za kina juu ya zahanati hiyo.

Alisema zahanati hiyo ina friji kwa ajili ya kuhifadhi chanjo za watoto na wajawazito. Hata hivyo, Nipashe ilielezwa katika zahanati hiyo kuwa friji hilo linaharibika mara kwa mara na kusababisha kuharibika pia kwa chanjo zinazohifadhiwa.



Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson (mwenye suti ya kijivu), akiwa katika picha ya pamoja na kamati ya kutetea na kupinga ukatili dhidi ya watoto wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyofanyika katika wilaya yake. **PICHA: JAMES LANKA**

# Waiangukia Hazina ujenzi wa barabara

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) Mkoa wa Kilimanjaro umeiomba Hazina kuipa Sh. bilioni 3.7, ili kufanya matengenezo ya barabara ya Chome inayoviunganisha vijiji vilivyoko katika milima ya Upare.

Mratibu wa Tarura mkoani hapa, Meleck Silaa, alisema juzi kuwa wamelazimika kuomba kiasi hicho cha fedha ili kufanya matengenezo ya barabara hiyo yenye urefu wa Km 25.

Silaa alitoa taarifa hiyo kwa Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Staki, alipokabidhi mradi wa ujenzi wa barabara hiyo kwa Kampuni ya Checotec Tanzania Limited iliyoshinda zabuni ya ujenzi huo kwa kiwango cha changarawe.

"Mpaka sasa, tumeshapokea Sh. milioni 600 tu ambazo zimo katika bajeti ya matengenezo ya barabara hii. Imeelekezwa kwamba hizo zilizopatikana zigharamie matengenezo ya barabara yenye urefu wa Km nane katika muda wa miezi mitano.

"Naomba wananchi wawe wavumilivu wakati serikali inaangalia uwezekano wa kupata fedha za kutengeneza barabara hii ambayo tunaamini itafungua milango zaidi ya kiuchumi.

"Lakini pia mkandarasi hakikisha unafanya kazi kwa muda uliopo katika mkataba na uwatumie vijana wa maeneo husika na msisahau kutunza mazingira," Silaa alisema.

Baada ya makabidhiano hayo, mkandarasi aliyeshinda zabuni hiyo ya ujenzi kutoka Kampuni ya Chacotec Tanzania Ltd, Herieli Mgonja, aliahidi kumaliza kazi hiyo kulingana na masharti ya mkataba na kuahidi kuwa vijana kutoka katika Kata ya Chome ndiyo watakaopewa kipaumbele katika mradi huo.

Mkuu wa Wilaya hiyo (Staki), alimtaka mkandarasi huyo kutengeneza barabara hiyo kwa ufanisi na kwa viwango vinavyokubalika.

"Nia ya serikali kuunda Tarura ni kuona kwamba changamoto ya usafiri nchini hususani maeneo ya vijijini zinabaki kuwa historia. Wakala umepewa jukumu zito la kusaidia kuimarisha mtandao wa barabara za vijijini na kuwezesha wananchi wengi kusafiri na kusafirisha bidhaa zao kwa urahisi," alisema.

# Akumbusha ahadi ya Rais Magufuli

**Na Mary Mosha,** MOSHI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro imetoa zaidi ya Sh. milioni 20 kwa ajili ya matengenezo ya barabara yenye urefu wa Km 12 kwa kiwango cha moramu kutoka Mamboleo hadi Uru Shimbwe.

Diwani wa Kata ya Uru Shimbwe wilayani Moshi, Bertin Mkami, aliyasema hayo jana alipotembelea mradi huo baada ya kuapishwa kuongoza kata hiyo.

Alisema ameanza kazi ya kumtembelea mkandarasi wa ujenzi wa barabara hiyo na ameahidiwa ujenzi huo utaendelea baada ya kumalizika kwa msimu wa mvua.

Alisema mkandarasi yupo tayari eneo la mradi na kwamba alikuwa anasubiri hali ya hewa kuwa nzuri ili kuendelea na kazi yake baada ya mvua kunyesha kwa kiwango kikubwa.

Alisema barabara hiyo iko kwenye mkakati wa kujengwa kwa kiwango cha lami kutokana na Rais John Magufuli kutoa ahadi hiyo mwaka 2015 wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu.

Diwani huyo pia alisema kwa sasa, kata yake ina kitongoji kimoja tu ambacho hakijaunganishwa na umeme wa REA na wako katika mkakati wa kuikarabati Shule ya Msingi Shimbwe.

Alisema amepata ufadhili wa Sh. milioni 12 kwa ajili ya ujenzi wa choo cha wanafunzi wa kike na kiume katika shule hiyo na kwamba ujenzi huo utakamilika hivi karibuni.



Baada ya korosho kukwama, Kibiti yahamishia mtego wa mapato ufuta

Ukurasa 19

UCHUMI



Tanzania katika mageuzi makubwa utalii duniani ikibeba sura ya kinara

Ukurasa 14


# BUFE

Ijumaa Juni 21, 2019


Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


MAGEUZI BANDARI ZA VICTORIA

# Walichokikosa miaka 61, leo mashuhuda kuingia ‘chomboni’ bila kukanyaga maji

Ukurasa 16



UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UCHUMI

Na Nimi Mweta

# Tanzania katika mageu utalii duniani ikibeba s

## • Tuzo ya Russia imeidhinisha kimataifa

JUHUDI za kubadili mwonekano wa Tanzania katika biashara ya utalii duniani, zinaanza kuzaa matunda.

Hiyo ni baada ya matukio ya kimataifa kuipa hadhi kubwa kwa ubora wa kinachoweza kumwonyesha mgeni, upana wa vivutio na ubora wa maskani wanakofikia watalii, hasa hoteli katika miji mikubwa, mbugani na ufukweni.

Ni eneo ambako mtu anaweza kusema, Tanzania inaelezwa ilikuwa imechelewa kuonyesha ilicho nacho na inachoweza kuwapa au kuwaonyesha watalii.

Siyo rahisi kusema, ni nguvu zipi zimefanya kazi kuanza kubadili hali hiyo. Kuna msukumo wa wazi na wakati wote kutoka kwa mamlaka zinazohusika na utalii, ila kuna soko lenye nafasi ya kimataifa.

Ni katika eneo hilo la pili, ambako inawezekana mabadiliko yamekuwa ya haraka zaidi kuliko upande wa kwanza, yaani juhudi za kitaasisi au za kidiplomasia kukuza biasharaya utalii kwa maana ya kupata wageni wengi zaidi kutoka nje.

Ni sehemu iliyochukua muda mrefu kubadilika, kwa maana ya kuwa na sura mpya inayoendana na hali halisi, pia kubadilika mazingira ya ndani, kuendana na kinachohitajiwa katika soko la kimataifa.

Hapo ni kuboresha taswira ambayo mgeni au mtalii tarajiwa anakutana nayo kwa haraka akisikia jina au nchi Tanzania ikitajwa. Ni taswira kongwe (zinaitwa stereotypes) zinazochukua muda mrefu kubadilika, zikishajengwa kwa miongo kadhaa.

Mtu anaweza kusema, taswira ya kawaida iliyodumu miaka mingi kuhusu utalii na mazingira yake, imetokana na ukinzani uliokuwapo kati ya Tanzania na nchi za Magharibi, tangu kutangazwa Azimio la Arusha, mwaka 1967.

Ni hatua iliyobadili sura ya Afrika Mashariki kuwa na pande mbili kimsingi, Kenya ilikuwa na mwonekano wa ki-Magharibi na Tanzania, iliyokuwa na mwonekano wa ki-Mashariki, licha ya kwamba haifungamani na nchi za Kijamaa.

Uhusiano kati yake na nchi za Scandinavia au taasisi kadhaa za kimataifa kama Benki ya Dunia, kwa miaka mingi ulikuwa mzuri tu. Ila walikosana tena katika urekebishaji uchumi.

### Tanzania kivutio

Kwa miaka zaidi ya 10, Tanzania imekuwa ikitajwa kushika nafasi ya pili kwa vivutio duniani nyuma ya Brazil, ambako kwa ama njia moja au nyingine, inafanana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa ukubwa wa nchi na upana wa vivutio vyake.

Hapo ina maana, DRC ikijtahidi katika miaka inayokuja hasa kujenga miundombinu ya kurahisisha usafiri kati ya majimbo ya nchi, inaweza kutoa changamoto kubwa ya vivutio vya utalii katika eneo la Afrika Mashariki na Kati, ambako hadi sasa inatawaliwa na Kenya na Tanzania, huku Rwanda ikikua kwa kasi.

Utalii nchini Uganda hausikiki sana, kama ilivyo Kenya, kutokana na maeneo ya utalii mkubwa kuwa




Tembo wakiwa katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

> “Tusipoangalia, bidhaa zinazozalishwa nchini huenda vikashindwa hata kushindana na bidhaa zinazotoka nje. VAT ni somo gumu na pana, nchi kama Ufaransa wana utaratibu ambao bahati kwao ni ‘very smart’, lakini kwa nchi zetu hizi ni ‘very complicated’.

upande wa Mashariki.

Licha ya umuhimu wa Tanzania na wingi wa vivutio vyake unafahamika duniani kote, haikuwa rahisi kuoanisha wingi wa vivutio na wasafiri, kwani usafiri unaohusu nchi hizo unajengwa na vizazi.

Taswira ya nchi inapokaa kichwani inachukua muda kubadili mazingira yake, kwani hisia kuhusu nchi zinategemea ushuhuda, kama ilivyo kwa watu binafsi kijamii, kuwa na shuhuda zinazotolewa zinamejengea taswira.

### Kongamano Russia

Ni sababu ambayo Tanzania inabeba nafasi ya kuwashukuru waandaaji wa kongamano na utoaji zawadi kimataifa nchini Russia mapema mwaka huu.

Tanzania ilipewa nafasi ya kwanza kwa wingi wa vivutio duniani na hata ubora wake, kwa maana ya mtawanyiko na upana wa maeneo yenye vivutio.

Siyo rahisi kulinganisha kila kitu, lakini itakuwa vigumu kwa Brazil, ambayo ina mto mkubwa ambao misitu yake inachukua sehemu kubwa ya nchi, kuwa na eneo pana kama hifadhi moja ya Selous, ambayo taarifa zinaifafanua ukubwa wake ni sawa na nchi yote ya Ujerumani.

Ni aina ya muujiza kuwa na mbuga kama hiyo. Hata hivyo, ziko nyingine. Kuna aina ya ushindani kati ya Selous na Hifadhi ya Ruaha, moja ikisifiwa kwa tembo na nyingine ikisifiwa kwa samba.

Hapo, ni sawa na Hifadhi ya Serengeti inayosifiwa kwa idadi kubwa ya nyumbu na pundamilia wanaohama, huku zikitajwa nyingine Mahale na Sokwe.

Tumesikia karibuni kuwa katika Bonde la Kilombero, kwamba lina



Watalii wakizuru hifadhini Selous. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

# uzi makubwa sura ya kinara



Simba wakiwa mtini kwenye Hifadhi ya Taifa Selous.

labda nusu ya mamba walioko nchini, ni mazingira yanayoweza kuvutia utalii wa kuwinda, kwani ngozi yake inapendeza.

Kutokana na vivutio vya



nchini, vinaweza kutoa habari nyingi za utalii, hasa mawasiliano mapya duniani yanapowezesha watu kujua kiini, kutokana na ufuatiliaji wa vitu tofauti, hivyo vinaanza kufahamika na kutajwa muhimu wake katika utalii wa duniani.

Mtazamo mmojawapo, ni simba wanaopanda mitini kule hifadhini Manyara. Nyingine ni Bonde la Olduvai na Mlima Kilimanjaro.

**Utalii wa kisiasa**

Haja nyingine iliyoko ni ya kuongeza kitu kingine; utalii wa kisiasa. Huo hauhusu kusafiri, bali kutambua kipya kinachotokea Afrika na mahsusi kinapatikana nchini Tanzania.

Inaelezwa, ina nafasi ya kubadili taswira ya nchi, kupitia msisimiko, pale makundi tofauti ya wadau wa kimataifa wanaporidhika na mtazamo kwamba kinachofanywa si cha kawaida.

Picha au taswira, huwa na michanganyiko na michanganuo tofauti, lakini baadhi yake zinaanza kujitokeza, sifa zake zikienea duniani, ambako kuna mifano miwili.

Kwanza, kampeni ya 'kutumbua majibu' iliyosisimua wasomi barani kote, halafu 'hoja ya makinikia' nayo ilitingisha dunia.

Iko pia mikondo mipana zaidi ya uchumi wa kimataifa ambayo inajieleza, yenyewe na matokeo yanayonekana, pasipo kuhitaji nguvu kubwa kutoka kwa taasisi za nchini.

Kwa lugha nyingine, ni kuwezesha juhudi za kitaasisi kuzaa matunda kwa tija kubwa zaidi, kuliko ilivyokuwa mtazamo wa awali.

Ni dhana nzima ya kukua Bara la Afrika, ambalo ni soko muhimu duniani katika miongo inayokuja, halafu kukua kwa nchi za Mashariki ya Mbali, ambazo ni tegemeo jipya katika usafiri wa kitalii. Hapo kuna kukua katika uwezo wa nchi za Ulaya Mashariki, zikiwamo Russia na Uturuki, kuwa karibu zaidi na Afrika kiuchumi.

Katika hatua hiyo, picha inayojitokeza ndio hiyo ya kuitishwa kongamano la kimataifa na kutolewa tuzo na zawadi ambako ubora wa Tanzania katika utalii duniani umeanza kukubalika.

Hapo kuna utambulisho wa ubora unaotokana na juhudi za kitaasisi, zikizaa kiwango kilichofikiwa. Ni kielelezo kuwa hali inabadilika kimsingi, kuwa njema zaidi.

# Unajua waliokata tamaa mahali wanakokimbilia?

**Na Mwandishi Wetu**

WATU huenda wapi maisha yao yanapotishiwa na mapigano, mateso au njaa? Inaelezwa takribani asilimia 80 ya watu hawaondoki nchini mwao na wale wanaoondoka, takribani asilimia 80 huenda nchi jirani, si zaidi ya hapo.

Katika maadhimisho ya Siku ya Wakimbizi Duniani mwaka jana, waliangalia nchi sita ambazo zilikuwa na idadi kubwa ya wakimbizi mwaka 2018

Uturuki; inahifadhi wakimbizi wengi kuliko nchi nyingine yoyote. Matokeo ya vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Syria, tangu mwaka 2011.

Idadi kubwa pia inasafiri kutoka Afghanistan. Uturuki inahifadhi karibu mmoja kati ya wakimbizi watano chini ya Shirika la Wakimbizi Duniani UNHCR.

Peru; ni ya pili kupokea wakimbizi mwaka 2018 wengi kutoka Venezuela, kutokana na kuporomoka kwa uchumi.

Watu milioni nne wamekimbia huko mwaka 2015, wengi wakienda nchi jirani, kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa.

Juma lililopita Peru iliweka sheria kali za uhamiaji kudhibiti kasi ya wakimbizi kuingia nchini humo.

Sudan; huko ambako si salama hivi sasa, wakimbizi wengi waliowasili mwaka jana walikuwa wakikimbia vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Sudani Kusini.

Wengine wengi waliingia wakitoka mbali zaidi- Sudan ni ya tatu kwa kupokea wakimbizi kutoka Syria nje ya Mashariki ya Kati.

Lakini Sudan yenyewe ni chanzo cha wakimbizi, watu 724,800 waliondoka nchini humo mwishoni mwa mwaka 2018

Uganda; Uganda ilipokea wakimbizi kutoka nchi mbili za jirani waliokimbia nchi zao kutokana na migogoro ya ndani: Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo wakimbizi karibu 120,000 na Sudani Kusini.

Pia ilipokea idadi kubwa ya watoto waliokimbia wenyewe bila wazazi na waliotenganishwa mwaka 2018.

Lakini wakimbizi 83,600 walikuwa wamerejea nchini Sudani Kusini wakitokea Uganda ilipofika mwishoni mwa mwaka 2018.

Marekani; Imeweka msimamo kuhusu masuala ya uhamiaji tangu Rais Donald Trump kuingia madarakani. Ilikuwa na idadi kubwa ya watu wanaotafuta hifadhi mwaka 2018, na maombi mengi ya wanaotafuta hifadhi kuliko nchi nyingine yeyote mwaka huo.

Wakimbizi wa Marekani walitoka katika nchi 166, lakini zaidi ya nusu walitoka Mexico.

Idadi ya watu walioomba uhifadhi ilikuwa ndogo kuliko idadi ya 331,700 miaka ya nyuma.

Ujerumani; inahifadhi wakimbizi zaidi ya milioni moja zaidi ya nusu yao kutoka Syria (532,000 mwishoni mwa mwaka 2018).

Nchi hiyo bado ilikuwa chanzo cha idadi kubwa ya wakimbizi kuingia nchini Ujerumani mwaka 2018, lakini idadi nyingine kubwa iliingia kutoka nchini Iraq

Lakini ingawa Ujerumani inashika nafasi ya tatu duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya maombi ya uhamiaji, idadi imepungua kutoka 722,000 mwaka 2016.

Idadi ya watu wanaoomba hifadhi ilishuka kwa asilimia 14 mwaka 2018 pekee.

Makala haya yanatoka kwenye ripoti ya Shirika la Wakimbizi Duniani.

**Kwa mujibu wa mtandao.**



Wakimbizi kutoka nchini Mexico, katika misafara wakitaka kuingia nchini Marekani. **PICHA: MTANDAO.**

BIASHARA

MAGEUZI BANDARI ZA VICTORIA

# Walichokikosa miaka 61, leo mashuhuda kuingia 'chomboni' bila kukanyaga maji

- Wenyeji washangilia 'haijapata kutokea'
- Wafutiwa sharti la vua nguo upande boti
- TPA yaingiza mabilioni kwenye ujenzi wa gati visiwani

**Na Mary Geofrey, MWANZA**

MIRADI ya ujenzi wa gati za kisasa na ukarabati wa zile za zamani inayotekelezwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), kwa kutumia fedha za ndani za mamlaka hiyo, inaonekana kuwa mkombozi wa kupaisha uchumi wa Taifa na kurahisisha maisha ya Watanzania wanaoishi Visiwani.

Ziwa Tanganyika ni miongoni mwa maziwa makuu, ambayo TPA imewekeza miradi mbalimbali ya usafiri wa majini na kutoa huduma za usafirishaji mizigo.

Miradi hiyo kwa asilimia 100, inatekelezwa na fedha za walipa kodi nchini, inatajwa kuwa mkombozi kwa wananchi na yenye manufaa kiuchumi kwa Taifa.

Tangu Rais John Magufuli, aingie madarakani takribani mwaka wa nne sasa, TPA ilianzisha na inaendeleza miradi ya bandari zote nchini kwa lengo la kuimarisha uchumi wa mamlaka na kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

Mbali na ujenzi na ukarabati wa gati unaofanywa na TPA katika bandari zote, pia wanajenga maghala ya kuhifadhia shehena za mizigo, ofisi za watumishi wa mamlaka za serikali zinazofanya kazi bandari.

Hapo inamaanisha maofisa Uhamiaji, Mamlaka ya Mapato (TRA), Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Pia, wanajenga nyumba za watumishi uzio wa kuimarisha usalama wa bandari na majengo ya kusubiria abiria na vyumba vya kuhifadhia mashine za umeme.

**MIRADI VICTORIA**

Bandari ya Mwanza, ni makao makuu ya bandari zilizopo katika Ziwa Victoria, wanatekeleza miradi mbalimbali.

Kaimu Meneja wa Bandari ya Mwanza, Geofrey Lwesya, anasema katika mkoa wa Mwanza wanatekeleza miradi ya maendeleo katika bandari za Ntama na Sengerema.

Mtendaji huyo anasema, katika Bandari ya Ntama wanajenga gati ambalo ujenzi wake umefikia asilimia 80, kazi iliyobaki ni kuezeka jengo la abiria na umaliziaji wa ujenzi wa vyoo na mnara wa tangi la maji, gharama yake ni Sh. bilioni 2.224 na unategemewa kukamilika Agosti 4, mwaka huu.

Pia, anataja mradi mwingine ni gati la kisasa katika bandari za Lushamba na Sengerema unaogharimu Sh. bilioni 1.265.

"Mradi huu sasa umefikia asilimia 90 ya utekelezaji wake na unatarajia kukamilika Julai 9, mwaka huu," anasema Lwesya.

Anaeleza kuwa sehemu ya kazi zilizobaki kwenye mradi huo ni kumalizia jengo la abiria na mizigo, uzio, vyoo, mnara wa tangi la maji na ujenzi wa chumba cha kuhifadhi mashine ya umeme.

Lwesya anasema, pia katika Bandari ya Fela, wamechukua eneo la ujenzi wa bandari kavu, lenye ukubwa wa ekari 117,869 kwa sasa limepata mzabuni mshauri kwa ajili ya upangaji wa matumizi ya bandari.

> **"Mradi huu katika Wilaya ya Musoma umekamilika na watumiaji wa bandari hiyo watanufaika na huduma zinazotolewa, kwa sababu awali walikuwa wanakumbuna na changamoto za kukanyaga maji wanapopanda boti na mitumbwi," anasema Lwesya.**



Sehemu ya Bandari ya Musoma, ikifanyiwa upanuzi. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

"Mbali na kuwa tunamiliki bandari katika maeneo ya Ziwa Victoria pia tuna eneo la bandari kavu ambalo litapangiwa matumizi yake na linagharimu Sh. bilioni 5.604," anaeleza Lwesya.

Kuhusu miundombinu wanayomiliki katika Bandari ya Mwanza Kusini, Lwesya anaeleza wana gati tatu zenye urefu wa mita 280, maghala matatu, mizani moja yenye uwezo wa tani 100.

Anasema, pia wana karakana ya kutengeneza meli moja yenye urefu wa mita 110, upana mita 17 na yenye uwezo wa kubeba tani 2,100.

Katika Bandari ya Mwanza Kaskazini, anasema wana gati tatu moja yenye urefu wa mita 212.5 na jengo la kupumzikia abiria moja, vitendea kazi na mzani moja wenye uwezo wa kubeba tani 100.

**BANDARI MUSOMA**

Ziwa Victoria katika mkoa wa Mara, pia Lwesya anasema wana mradi wa ujenzi wa gati la Mwigobero katika Bandari ya Musoma, ambako

umegharimu Sh. milioni 605, kazi ikiwa imeshakamilika.

"Mradi huu katika Wilaya ya Musoma umekamilika na watumiaji wa bandari hiyo watanufaika na huduma zinazotolewa, kwa sababu awali walikuwa wanakumbuna na changamoto za kukanyaga maji wanapopanda boti na mitumbwi," anasema Lwesya.

Anasema katika bandari hiyo wana bandari kuu yenye gati tatu kila moja lenye urefu wa mita 160 na jengo la abiria.

**BANDARINI GEITA**

Kiongozi anayesimamia bandari ya Nyamirembe, wilayani Chato, Mkoa wa Geita, anasema wanaendelea na mradi wa kujenga gati kwa gharama ya Sh. bilioni 4.128. Hadi sasa maendeleo yake yamefika asilimia 40.

Anataja kilichobaki ni kumalizia ujenzi wa gati, majengo ya abiria, mizigo, uzio, vyoo, mnara wa tangi la maji na chumba cha mashine ya umeme.

Lwesya anataja kazi nyingine, ni ujenzi wa chumba cha walinzi, mradi unaotarajiwa kukamilika mwezi Agosti.

**MKOA KAGERA**

Mkoani Kagera nako hakujaachwa nyuma katika miradi ya maendeleo, ambako kuna ukarabati wa jengo la ofisi na abiria katika awamu ya pili.

Lwesya anasema, mradio kwa sasa umefikia asilimia 95 ya utekelezaji wake na unagharimu Sh. milioni 143. Inategemewa kufanyiwa ukaguzi wa mwisho mwezi Juni huu.

Anataja mradi mwingine ni kujenga gati la Magarini wilayani Muleba, utakaogharimu Sh. bilioni 1.730, na kwamba hadi sasa umeshafika asilimia 62 ya utekelezaji wake.

Lwesya anataja sehemu ya kazi iliyobaki ni kujenga gati, jengo la abiria, mizigo, vyoo, mnara wa tangi la maji na chumba cha mashine ya umeme na chumba cha walinzi.

Anasema mradi huo unatarajiwa kukamilika mwisho wa mwezi Juni mwaka huu, huku akitaja miundombinu inayomilikiwa na Bandari Bukoba ni gati tatu zenye urefu wa mita 202.5 na jengo moja la kupumzikia abiria.

Kwa mujibu wa Lwesya, pia katika mwalo wa Bukoba wana gati yenye urefu mita 48 na katika Bandari ya Nansio (Ukerewe) wana gati tatu ndogo yenye urefu wa mita 100 na jengo la kupumzikia abiria.

Lwesya anasema katika Bandari ya Kyamkwikwi wilayani Muleba, wana gati moja, ghala la mizigo na chelezo.

**MIKAKATI ILIYOPO**

Lwesya anasema wameweka mikakati ya kuwawezesha kufikia malengo waliyojiwekea kama bandari, ikiwamo kuendelea na wateja wanaowahudumia, kutafuta wateja wapya, kurudisha waliondoka sokoni na kuzidisha wateja wakubwa.

Anasema pia wanarekebisha miundombinu iliyopo na ujenzi mpya magati na kununua vifaa vipya kwa ajili ubebaji wa mizigo.

Pia, kupitia mkakati hiyo, anasema wanaimarisha na kuongeza ushirikiano na wadau kama Kampuni ya Kuhudumia Meli (MSCL), Mamlaka ya Mapato (TRA) na sekta za serikali na wadau binafsi.

**WANANCHI KUNUFAIKA**

Mhandisi wa TPA Mwanza, Abraham Msena, anasema kuwa wananchi wa kijiji cha Nanyara, katika Halmashauri ya Buchosa, iliyoko Sengerema Mwanza, wanaelekeza pongezi kwa Rais Dk. John Magufuli, kupitiaTPA kwa kuwajengea gati katika Bandari ya Lushamba, ambayo inawarahisishia usafiri.

Tangu mwaka 1958, wakazi wa kijiji cha Buchosa na vitongoji vya Mwibale, Msikitini, Kisarazi na Gembale, waliunganishwa na usafiri wa mitumbwi iliyokuwa ikiishia majini, hivyo gati hilo ni unafuu unaowaondoa katika adha hiyo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Lazaro Ngonzo, anasema kwa miaka 61 tangu kuanzishwa bandari hiyo hakukuwapo gati, sasa jumla yao wakiwa 8,000 wamekuwa wakisafiri katika mazingira yasiyo salama.

Anataja baadhi ya adha hizo ni kupanda boti ndani ya maji hali inayosababisha kupoteza mali zao na kulazimika kuvua nguo wakati wa kupanda na kushuka.

Ngonzo anatoa ufafanuzi: "Hakika tumekumbukwa kwa sababu bandari hii itarahisisha usafiri wa kwenda visiwani kwa urahisi tofauti na sasa tunapata shida."

Anasema kila siku kuna jumla ya boti 13 zinazotoa huduma za kwenda na kurudi katika visiwa vinavyozunguka kijiji hicho.

"Tunaishukuru serikali. Ujenzi wa bandari hii ni msaada mkubwa kwetu, tunaamini serikali imetuona na imetufikia, matatizo yetu yanakwenda kumalizika sasa," anasema.

Mkazi wa Musoma, Anna Joseph, anasema awali kabla ya ujenzi wa gati ya Mwigobero, wakilazimika kupandisha nguo hadi wanapokanyaga maji wakati wa kupanda au kushuka kwenye meli hali ambayo ilikuwa ikiwadhalilisha wanawake na wakati mwingine walipoteza mali zao kama simu.

"Tunashukuru kwa ajili ya ujenzi wa gati hii, itasaidia sana wananchi wa Musoma na watumiaji wa bandari hii, tutaondokana na adha ya kuvua nguo wakati wa kupanda na kushuka kwenye meli na wakati mwingine watu walikuwa wakipoteza maisha wakidondoka kwenye mali, tunaishukuru sana serikali kwa kutujengea mradi huu," anasema Anna.



Bandari ya Lushamba, mkoani Mwanza katika mandhari yake mpya inayopendeza na kisasa.

## BIASHARA KATIKA PICHA



George Bajuta Mwenyekiti wa Wafugaji nchini, akiwa na mifugo yake, mkoani Songwe. **PICHA: IBRAHIM YASINI**



Mkuu wa Masoko na Uhusiano wa Benki ya KCB, Christine Manyenye (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam wikiendi, katika uzinduzi wa awamu ya pili ya programu ya tujiajiri inayotarajia kutoa jumla ya Sh. milioni 85 kama ruzuku kwa kinamama wajasiriamali 17, ambao wamekamilisha na kufuzu awamu ya kwanza ya mafunzo ya kinadharia na vitendo ya kurasimisha biashara, usimamizi wa fedha na mafunzo ya kuongeza mauzo na kukuza soko la biashara zao. Wengine ni Mkuu wa Kitengo cha Biashara Barry Chale (kulia), Mkuu wa Uendeshaji na Teknohama Rojas Mdo, (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Shule ya Sekondari ya East Coast iliyo Kibaha ambaye ni mmoja wa walengwa wa programu hiyo, Bhoke Mukoji Mhini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




Mabalozi wa M-Pawa, Mpoki Mjuni na Dokii Wenceslaus wakichezesha droo ya pili ya M-pawa inayoendeshwa na Benki ya CBA pamoja na Vodacom iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya kusherehekea miaka mitano ya huduma hiyo nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

BIASHARA

## SH. MILIONI 101 MEZANI

# Halmashauri Musoma yawasambazia vijana, wanawake, wenye ulemavu mikopo bila riba

**Na Sabato Kasika**



Wana kikundi cha Kwikuba Carpenters wakiwa kazini.

UTOAJI mikopo kwa vikundi vya vijana, wanawake na walemavu ni utekeleaji wa agizo la serikali. Tayari Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, mkoani Mara, nao hawako nyuma katika hilo, wakitenga asilimia 10 ya mapato ya halmashauri kuviwezesha vikundi kujikwamua kiuchumi.

Katika mwaka wa fedha ulioisha, halmashauri hiyo ilitoa Sh. milioni 101 kwa vikundi 21 vya vijana, wanawake na walemavu vilivyopo Musoma Vijijini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Wilaya ya Musoma, John Kayombo, anasema katika mwaka wa fedha uliopita, halmashauri iliitengea zaidi ya Sh. milioni 109 za mkopo kwa makundi hayo matatu.

"Hadi sasa tumeshatoa mkopo wa Sh. milioni 101 na tunajiandaa kumalizia fedha zilizobakia ambazo ni zaidi ya Sh. milioni nane, tumepanga kufikia mwishoni mwa mwezi huu tuwe tumefanya hivyo," anasema Kayombo, huku akiwakumbusha wakopaji kuzingatia masharti, ikiwamo ya kurejesha deni kwa wakati.

"Serikali imeshaondoa riba kwenye mikopo ya wanawake, vijana na walemavu katika ngazi ya halmashauri. Serikali imedhamiria kuyasaidia makundi hayo, na kwamba jambo la msingi ni kuzingatia masharti ya mkopo."

Anawakumbusha kuwa, nia ya serikali kutoa mikopo ni kuwataka wanawake, vijana na walemavu kujikwamua kiuchumi, kupitia uanzishaji miradi kwa kuegemea nguvu ya mikopo wanayopewa.

**MIKOPO VIKUNDI 21**

Kayombo anasema katika vikundi 21 vilivyopata mikopo katika halmashauri yake, wanawake ni vikundi14, walemavu vitatu na vijana vitano, vyote vinajishughulisha na biashara.

Mkurugenzi huyo anataja vikundi vya vijana vilivyopata mkopo kuwa ni; Amani Group kilichopo Kijiji cha Tegeruka na cha Jenga na Sisi cha kijiji cha Mkirira. Vyote vimekopeshwa Sh. milioni tano kila kimoja. "Wengine ni vijana waendesha bodaboda wa kijiji cha Mkirira wamepata Sh. milioni 6.7, Kwikuba Carpenters wa kijiji cha Kwikubwa Sh. milioni sita na Jitahidi Ufaidike wa kijiji cha Kamguruki Sh. milioni nane," anasema.

Anafafanua kuwa, vikundi hivyo vimepata mkopo jumla Sh. milioni 30.7, kwa ajili ya kuendeshea biashara za useremala, ufugaji kuku, kusaga, uuzaji ng'ombe na kilimo cha bustani.

**WALEMAVU**

Katika vikundi vya wenye ulemavu, Kayombo anasema wamejitokeza Shivyawata Erusuri Group cha kijiji cha Bwai Kumsoma na kukopeshwa kimepata Sh. milioni mbili.

Anakijata kikundi kingine ni Mifunda Walemavu wa kijiji cha Chumwi, ambacho kimekopeshwa Sh. milioni 1.3 na kwamba jumla ya mkopo kwa watu hao wenye ulemavu ni Sh. milioni 3.3.

**VIKUNDI WANAWAKE**

Anavitaja vikundi hivyo ni; Upendo Women Group cha kijiji cha Bwai Kwitururu na Imani Chumwi, Mtakatifu Jema cha kijiji cha Maneke, Tumaini Group cha kijiji cha Kwikubwa, kila kimoja kimepatiwa shilingi milioni tano.

> **"Vikundi vingine ni Kinamama Vicoba cha kijiji cha Busungu, Upendo Group cha kijiji cha Chumwi na Tujikomboe Group cha kijiji cha Rukuba, ambavyo vyote kila kimoja kimepata mkopo wa Sh. milioni tano," anasema.**



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, John Kayombo. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

"Vikundi vingine ni Kinamama Vicoba cha kijiji cha Busungu, Upendo Group cha kijiji cha Chumwi na Tujikomboe Group cha kijiji cha Rukuba, ambavyo vyote kila kimoja kimepata mkopo wa Sh. milioni tano," anasema.

Mkurugenzi huyo anataja kikundi cha Bomafa cha kijiji cha Kinyang'erere na Kuludala cha kijiji cha Buraga, kila kimoja kimekopeshwa Sh.milioni tatu, Imuca Group cha kijiji cha Chumwi, shilingi milioni nne; na Upendo Group cha kijiji cha Chitare, kimekopeshwa shilingi milioni saba.

"Matumaini Group cha kijiji cha Tegeruka, Mkombozi Group cha kijiji cha Mkirira na Amani na Upendo cha kijiji cha Kigera Etuma, kila kimoja kimepata Sh. milioni tano," anasema.

Anafafanua kuwa, vikundi hivyo vimepata jumla ya shilingi milioni 67 kwa ajili ya kusaidia biashara ya uuzaji nafaka, kilimo cha bustani za mboga na matunda.

"Jumla yake ya vikundi ambavyo vitakuwa tayari vimekopeshwa ni Sh.101,000,000," anasema Kayombo, akijivuna halmashauri yake imefika hatua nzuri katika utoaji mkopo, kukidhi asilimia 92.6 ya mahitaji.

Anasema katika mwaka huo wa fedha, Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, ilipanga kutenga asilimia 10 ya bajeti kuwakopesha vijana, wanawake na walemavu.

**VIONGOZI VIKUNDI**

Katibu wa Kikundi cha Amani na Upendo cha kijiji cha Kigera Etuma, Nyapamba Chibure, anasema hatua ya serikali kuondoa riba katika mikopo, ni ishara kwao inavyowajali wanyonge.

"Kwa mara ya pili sasa kikundi chetu kinapata mkopo. Mwaka 2017/2018 tulikopoeshwa shilingi milioni mbili, riba ilikuwa ni shilingi 200,000, lakini mwaka huu tumeambiwa hakuna riba," anasema Chibure.

Anasema, katika mwaka uliopo wa fedha, kikundi chake chenye biashara ya uuzaji nafaka, pia kuweka na kukopa, kimepata shilingi milioni tano.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Vijana cha Kwikuba Carpenters wa kijiji cha Kwikuba, Kamunyiro Kubega, anasema unafuu walioupata wa kutotozwa riba, unawapa wajibu wa kuhakikisha wanarejesha mkopo kwa wakati.

"Zamani tulikuwa tukihangaika kutafuta riba na pia jinsi ya kurejesha mkopo kwa wakati, lakini sasa hilo la riba halipo tena, kilichobaki ni kuchakarika kuhakikisha tunarejesha mkopo ili wengine wakope," anasema Kubega.

Mwenyekiti huyo anasema, kikundi chake kimepata mkopo wa shilingi milioni tano zitakazotumika kununua malighafi ya mbao na mengine, kutengeneza samani za kuuza. "Mwaka wa fedha wa uliopita, tulikopeshwa shilingi milioni tatu ambayo riba yake ilikuwa Sh. 300,000 na tulikuwa tunarejesha Sh. 75,000 kila mwezi, lakini sasa tunashukuru kwani tumetoka katika kifungo cha riba," anasema.

Pia, Mwenyekiti wa kikundi cha walemavu Shivyawata Erusuri Group, cha kijiji cha Bwai Kumsoma, Yohana Magai, anasema ni mara ya kwanza kikundi chake chenye wanachama 15 kupata mkopo.

"Tuliomba mkopo wa shilingi milioni mbili na tumepewa, sasa kilichobaki ni kuimarisha mradi wetu wa kufuga kuku wa kienyeji kadri inavyowezekana ikiwa ni pamoja na kujenga mabanda na kuongeza wengine," anasema.

Magai anasema Shivyawata Erusuri kwa sasa inafuga kuku 24 na wanakusudia kuongeza wengine kadri inavyowezekana, hivyo matarajio mkopo utawasaidia na watarejesha kwa wakati.

UCHUMI

**NaYasmine Protace, Kibiti**



Zao la ufuta likiwa limevunwa shambani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# Baada ya korosho kukwama, Kibiti yahamishia mtego wa mapato ufuta

- DC: Marufuku kuuvusha nje ya wilaya
- Vitambulisho Machinga 5,000 vyauzwa

HIVI sasa ni msimu wa mavuno katika maeneo mengi nchini. Katika hilo inaeleweka kwamba, mikoa ya kusini, kama vile Mtwara, Lindi ni mahiri katika ulimaji zao la ufuta.

Pia, kuna baadhi ya mikoa jirani nao kusini, ikichukuliwa mathalan, katika mkoa wa Ruvuma, kupitia wilaya yake kama Tunduru, panaeleweka sio mbali sana na Masasi mkoa wa Mtwara, au Nachingwea mkoani Lindi.

Vivyo hivyo mkoa wa Pwani katika wilaya za Kibiti na Rufiji nazo ni majirani waliokingana na mkoa wa Lindi. Hali ya hewa na ardhi za maeneo hayo, pia utamaduni wa wakazi hao, kwa jumla zinafanana sana.

Hao wote kuiuchumi wanaangukia katika umahiri wa kuzalisha zao la ufuta, huku Mtwara na Lindi wakiwa vinara na ni moja ya zao kuu la kiuchumi kwa wakazi wake.

Hivyo, si msamiati mgeni kumwambia mkazi wa Kibiti na Rufiji, kuhusu kujikita katika kilimo cha ufuta, pia mihogo na mahindi kama mazao ya kula.

Kwa sasa Wilaya ya Kibiti, imeamua kujipanga kuhakikisha inadhibiti njia za panya ili kuhakikisha zao hilo halivushwi katika wilaya zingine. Hiyo ni mbinu ya kudhibiti uchumi wa wilaya.

Ufuta unadhibitiwa usifike katika wilaya zingine, ikiwa namna inayosaidia kudhibiti mapato yao, vinginevyo yanashuka na inaangukia kuwajengea wakazi maisha duni, kupitia bajeti goigoi ya halmashauri yao.

**DC Kibiti**

Akizungumza katika kikao cha robo tatu cha Baraza la Madiwani Kibiti, Mkuu wa Wilaya, Gulam Hussein, anasema mwaka huu ndio unaofanyika mnada wa kwanza kwa kuuza ufuta na unaendelea vizuri, hivyo anawataka wananchi kutouza ufuta kwa kutumia 'kangomba' au njia nyinginezo za panya.

"Wilaya imejipanga na imehakikisha mianya yote ya kutorosha korosho inadhibitiwa," anasema Hussein.

Pia, mkuu huyo wa wilaya anasema kunapaswa kuwapo ushirikiano kati ya madiwani na wananchi na watumishi wa halmashauri, ili kusiwapo aina yoyote ya mchezo mchafu unaohusiana na kutorosha zao hilo.

Akizungumzia suala la mifuko ya plastiki, Hussein anatumia fursa hiyo kusema wilaya imeishazuia matumizi yake, kama ilivyo kitaifa, hivyo jambo muhimu sasa ni jamii kuzingatia maelekezo hayo kwa usalama wao kimazingira na kisheria.

Katika hilo, mkuu wa wilaya anatoa angalizo maalum kwamba wazazi na walezi wahakikishe wanafanya utaratibu wa kuwanunulia watoto wao mifuko inayoruhusiwa na kamwe wasiangukie mifuko iliyopigwa marufuku katika kubebea madaftari shuleni.

**Mwenyekiti Halmashauri**

**"Wilaya imejipanga kusimamia mnada wa ufuta," anasema Mwenyekiti na kuongeza, kuwa katika kuboresha kilimo cha korosho, jumla ya miche 2575 imepandwa sasa, lakini bado haijachukuliwa. Mmoja unauzwa Sh. 300.**

Khatibu Chaulembo, ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti, anasema wilaya awali ilitegemea sana ushuru wa korosho, lakini mwaka huu dharura iliyotokea imepelekea kinyume, kwamba ushuru wa kupitia korosho haukupatikana, tegemeo likiegemea kwenye ufuta.

Pia, mwenyekiti anasema katika utendaji wao walifanikiwa kukamata kilo 400 za korosho zikisafirishwa kupelekwa wilaya jirani ya Rufiji, hivyo anatoa angalizo kwamba itakapotokea mtu akikamatwa anasafirisha ufuta kinyemela, bidhaa yake itataifishwa.

Mtazamo wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ni kwamba, asilimia 45 ya mapato yaliyokuwa yanapatikana kupitia korosho, sasa tegemeo limebebeshwa zao la ufuta.

"Wilaya imejipanga kusimamia mnada wa ufuta," anasema Mwenyekiti na kuongeza, kuwa katika kuboresha kilimo cha korosho, jumla ya miche 2575 imepandwa sasa, lakini bado haijachukuliwa. Mmoja unauzwa Sh. 300.

Pia, Chaurembo anasema, wananchi waliovamia msitu wa Ngumbuluni na kuufyeka, kisha kupanda mazao ya ufuta na korosho, wanatakiwa kuondoka mara moja, kabla ya hatua kuchukuliwa, ikielezwa hatua hiyo ni hatari ya kuupoteza msitu wenyewe.

**Ofisa Biashara**

Kaimu Ofisa Biashara wa Kibiti, Savio Mango, anasema katika kazi ya msimu wa kuuza ufuta, anasema tani 30 za awamu ya kwanza ndio zilitarajiwa kuuzwa.

Kuhsu vitambulisho vya wajasiriamali, Mango anasema wameshagawa vitambulisho 5,000 na kupatikana kiasi cha Sh. milioni 100.

"Awamu ya kwanza tuligawa vitambulisho 1,000 na awamu ya pili tuligawa vitambulisho 4,000," anasema, kwamba ni mkakati ulioweza kuwafikia

wafanyabiashara wa mjini na vijijini.



Wakulima wa korosho waliokusanyika katika soko la kuuza bidhaa zao, Muhoro, Rufiji.

UCHUMI




# Taharuki ya fedha bandia zaiumiza Kenya, Benki Kuu yakana 'si kweli'

SAFARI mpya zilizinduliwa kutimiza masharti ya katiba, kukabiliana na ufisadi na fedha ghushi.

Kumekuwapo na taarifa zinazoenea katika mitandao ya kujamii kwamba noti mpya za thamani kubwa zaidi Kenya tayari zimeghushiwa.

Noti hizo za shilingi 1,000 zilizinduliwa wakati wa sikukuu ya Madaraka pamoja na noti nyingine kutimiza masharti ya kikatiba, kukabiliana na ufisadi na ueneaji wa fedha za kughushi.

Ukurasa maarufu wa kijamii ulieneza ujumbe unaodai kwamba tayari kuna noti mpya bandia ambazo zinaenezwa.

Hata hivyo, hakuna ushahidi wowote kwamba taarifa hizo ni za kweli.

Taarifa hizi zilienezwa vipi?

Ukurasa maarufu wa kuhusu hali ya foleni au msongamano wa magari barabarani Kenya katika 'Twitter' wenye wafuasi milioni moja, ulieneza ujumbe na picha zilizokuwa zimepakiwa mtandaoni na mtu mwingine zikidai kwamba kulikuwa na noti bandia.

"Iwapo mtu anaweza kubaini chanzo cha picha hii, basi Wakenya wasio na hatia wataokolewa [kutoka kwa matapeli]. Hizi ndizo noti bandia zinazoenezwa," ujumbe huo wa Twitter ulisema.

Ujumbe huo uliashiria kwamba noti zilizokuwa kwenye picha hiyo zilikuwa bandia.

Hata hivyo, ilibanika si sahihi, huku ikielezwa noti zilizopigwa picha ni halali.

Inadaiwa, ujumbe huo ulichanganya kati ya upande mbele na nyuma wa noti mpya za shilingi 1,000 za Kenya. Upande mmoja, kuna picha ya Majengo ya Bunge na upande mwingine Jumba la Kimataifa la Mikutano la Kenyatta (KICC).

Picha zote mbili zinapatikana kwenye noti mpya ya shilingi 1,000.

Madai zaidi

Ujumbe mwingine ulioenezwa sana kwenye 'WhatsApp' na 'Twitter' unasema yupo mtu aliyetapeliwa Dola 170 (shilingi 17,000 za Kenya) baada ya kukabidhiwa noti bandia za shilingi 1,000. Inaambatanishwa na ujumbe unaowatahadharisha watu wawe "macho, kuna noti bandia."

Baadhi ya watu kwenye mitandao ya kijamii wanasema rangi kwenye picha ya noti iliyowekwa ina mkolezo tofauti wa rangi.

Msemaji wa Benki Kuu ya Kenya, aliiambia BBC kwamba ni vigumu kubaini uhalisia na uhalali wa noti kwa kutazama picha pekee.

Aidha, alisema kufikia sasa hawajapokea taarifa zozote za kuwapo kwa noti mpya bandia.

Kulikuwpo pia na taarifa kwamba mwanafunzi wa chuo kikuu kimoja jijini Nairobi, alikuwa amekamatwa na noti bandia za jumla ya shilingi 10 milioni.

Madai hayo yalichapishwa kwenye blogu kadhaa na kuenezwa na watu kupitia 'WhatsApp.' Ilidaiwa pesa hizo ghushi zilikuwa za noti za shilingi 1000 na 500.

Taarifa hizo zilidai kwamba, mtuhumiwa ambaye ana miaka 21 alikamatwa baada ya wadokezi kutoa taarifa polisi.

Lakini Benki Kuu ya Kenya inasema hakuna kisa kama hicho kilichoripotiwa. ***BBC***







# Serikali yawahakikishia wawekezaji ushirikiano

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imewahakikishia wawekezaji kuwa itaendelea kushirikiana nao na kuboresha mazingira ya uwekezaji kuhakikisha uwekezaji wao unakuwa endelevu na serikali kunufaika na kodi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, alipokuwa anafunga kongamano la kuhamasisha uwekezaji kwenye kilimo cha mboga na matunda katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Kairuki alisema serikali inathamini mchango wa sekta binafsi katika ukuaji wa uchumi, hivyo iko tayari kuwashika mkono, kuwasemea na kuwajengea mazingira mazuri ili uwekezaji wao uendelee kuwa na tija.

Alisema serikali inapata mapato ya kodi na yasiyokuwa ya kodi kupitia uwekezaji unaofanywa na sekta binafsi na kuyatumia katika shughuli mbalimbali ukiwamo uendeshaji wa serikali na shughuli za maendeleo.

"Fedha zinazopatikana pia zinatumika katika kujenga na kuboresha huduma za kijamii pamoja na miundombinu ya maendeleo, hivyo niwahakikishie wawekezaji wote mkiwamo mliowekeza kwenye hii sekta ndogo ya mboga na matunda tunawathamini sana," alisema Kairuki.

Alisisitiza kuwa serikali itahakikisha inawatafuta wawekezaji popote walipo na kuwaalika kuja kuwekeza nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji (TIC), Geofrey Mwambe, aliwahamasisha wananchi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kulitumia kongamano hilo kama chachu ya kujikita kwenye uwekezaji kwenye mboga na matunda.

Alisema mazao ya mboga, matunda na maua yanalimwa na kustawi vizuri katika maeneo ya uwanda wa juu kutokana na hali ya hewa ya maeneo hayo kuruhusu yastawi vizuri.

Aliitaja baadhi ya mikoa ya Tanzania ambayo inayoruhusu mazao hayo kustawi ni Tanga, Manyara, Kilimanjaro, Arusha na mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

"Jukumu letu kuu kama Kituo cha uwekezaji ni kuibua fursa za uwekezaji ili wananchi wazione na wale wanaoziona wanaohitaji kuwekeza kutoka ndani na nje ya nchi waweze kuzitumia hizo fursa," alisema Mwambe.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirikisho la wakulima wa mboga na matunda (Taha), Jacqueline Mkindi, alisema changamoto kubwa inayowakabili wakulima wa Tanzania ni ukosefu wa masoko ya uhakika.

Alisema wakulima wamekuwa wakihamasishwa kuzalisha mazao mbalimbali, lakini masoko yamekuwa sio ya uhakika na hivyo kusababisha wakulima kuingia hasara.

Vilevile aliiomba serikali kujenga majengo yenye ubaridi ili kuwawezesha wakulima kuhifadhi mazao yao ya mboga na matunda yasiharibike kabla ya kupelekwa kwenye masoko.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, akiangalia mtoto mchanga aliyezaliwa kwenye Kituo cha Afya Tinde, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, na kutoa wito kwa wajawazito kujenga tabia ya kujifungulia vituo vya afya mahali kwenye usalama, pamoja na kuwanyonyesha watoto wao maziwa ya mama ili wapate kukua kiafya na kiakili. **PICHA: MARCO MADUHU**

# DC aipa neno shule kuhusu miradi ujenzi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKUU wa Wilaya ya Chunya, Mhandisi Maryprisca Mahundi, ameitaka Bodi ya Shule ya Sekondari Lupatingatinga kuhakikisha inasimamia vizuri mradi wa ujenzi wa bwalo la shule hiyo linalojengwa ili thamani ya fedha ionekane.

Alitoa angalizo hilo alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya mradi huo unaotekelezwa kwa kutumia mfumo wa akaunti ya dharura unaotumia mafundi wa kawaida badala ya mkandarasi.

Taarifa ya mradi huo inaonyesha utagharimu Sh. milioni 153, ambapo Sh. milioni 53 zinatokana na nguvu za wananchi wa kata tatu za wilaya hiyo ambazo ni Lupatingatinga na Mamba.

Mahundi alisema lengo la serikali ni kutumia mfumo wa akaunti ya dharura (Force account) ni kupunguza gharama kwenye miradi, hivyo aliwataka wasimamizi kuhakikisha fedha hizo zinaokolewa na kufanya kazi zingine.

"Tusije tukawa tunatumia mfumo huu kwa lengo la kuokoa fedha, kumbe fedha hizo zinaingia tena kwenye mifuko ya wachache, naombeni muwe waaminifu na bwalo hili likamilike wakati uliopangwa," alisema Mahundi.

Alisema ukumbi huo utakuwa unatumika kwa ajili ya mitihani ya taifa pamoja na wanafunzi wa shule hiyo inayoanzia kidato cha kwanza mpaka cha sita kuutumia kwa ajili ya chakula.

# Kanisa lashtukia misaada yenye masharti magumu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KANISA la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde, limeanza mikakati ya kujiunga na makanisa mengine katika baadhi ya nchi za Afrika kubuni miradi ya kiuchumi ili kujitegemea na kuachana na misaada ya nchi za magharibi yenye masharti magumu.

Moja kati ya masharti yanayodaiwa kulikera kanisa hilo ni kuwalazimisha Waafrika kuzikubali ndoa za jinsia moja, kitu ambacho limesema ni kinyume cha maandiko matakatifu na maadili ya Kiafrika.

Askofu wa KKKT Dayosisi ya Konde, Dk. Edward Mwaikali, aliyasema hayo wakati wa kutia saini hati ya ushirikiano wa masuala ya kiuchumi kati ya vijana wa kanisa hilo na Kanisa Presberian Synod la Malawi. Alisema makubaliano hayo yanalenga kuimarisha ushirikiano kwenye sekta ya afya na elimu ambapo alisema wanatarajia kuandaa miradi mbalimbali ili kuinua uchumi.

Alisema lengo kuu la umoja huo ni kuhakikisha nchi za Afrika zinaungana na kujiwezesha kutatua changamoto zao wenyewe badala ya kutegemea misaada kutoka nchi za magharibi.

"Asilimia kubwa nchi za Afrika zinafanana kiutamaduni, lakini kwa kipindi kirefu tumetengana... sasa ni wakati wa kuwa kitu kimoja na tunatatua changamoto zetu za kiuchumi pasipo kutegemea misaada ya nchi za Magharibi," alisema Dk. Mwaikali na kuongeza:

"Kwa kipindi kirefu misaada ya wazungu imetutawala na kudumuza akili zetu na ndio maana wamefika hatua ya kutupatia misaada inayoambatana na masharti ya kishetani," aliongeza.

Katibu wa KKKT Dayosisi ya Konde, Mchungaji Ikupilika Mwakisimba, alisema huu ni wakati sahihi wa madhehebu ya dini kuungana na kupanga mikakati itakayosaidia kuinua uchumi wa kanisa, nchi na kwa jamii.

Alisema makanisa pamoja na serikali vinatakiwa kuungana katika kukemea masuala mbalimbali yanayokwenda kinyume cha maadili ya Kiafrika.

Akizungumzia ushirikiano huo, Katibu wa Kanisa la Presberian Synod la Malawi, Mchungaji Alex Maulana, aliwataka Waafrika kuungana na kuondoa tofauti za kidini, ukabila, utaifa na rangi ili kuwa na nguvu ya pamoja kukabili mambo mbalimbali.


Alisema Waafrika endapo wataungana wataweza kufikia malengo yao binafsi bila ya kushurutishwa na taifa lolote pamoja na kuziwezesha nchi zao kukua kiuchumi.

"Sipendi kuwa mnafiki, nimeshangazwa na utaratibu wa nchi ya Tanzania kwa viongozi wa serikali kuwa pamoja na viongozi wa dini na kutekeleza masuala mbalimbali ya maendeleo, nawaombeni Watanzania msikubali kudanganywa na mtu yoyote, endelezeni amani na upendo uliopo," alisema Maulana.

Alisema ushirikiano kati ya serikali na viongozi wa dini ni muhimu sana kwa kuwa unapelekea wananchi wote kuwa wamoja na kufanya kazi kwa ushirikiano.

Akizungumza kwa niaba ya Serikali ya Tanzania Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alipongeza ushirikiano huo wa makanisa kwa maelezo kuwa ni mwendelezo wa ushirikiano kati ya mataifa hayo mawili.

Alisema Tanzania na Malawi zimekuwa na ushirikiano wa muda mrefu na kwamba ndio maana baada ya Malawi kupata madhara ya kimbunga, Serikali ya Tanzania ilipeleka msaada wa chakula kwa ajili ya wananchi wa nchi hiyo.





# Wizara yatangaza nia kutokomeza mbung'o

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI ipo mbioni kuanza utekelezaji wa mradi maalum wa kuangamiza mbung'o, ili kuboresha sekta ya ufugaji sanjari na kuongeza uzalishaji na wingi wa ng'ombe bora wa nyama na maziwa.

Hayo yalibainishwa jijini Dodoma na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Luhaga Mpina, wakati akizungumza na wananchi katika maonyesho ya ng'ombe bora wa maziwa yaliyofanyika katika Viwanja vya Nanenane.

Mpina alisema fedha zinazohitajika ili kukamilika kwa mradi huo nchi nzima zimepatikana na zipo tayari zikisubiri kuanza utekelezaji.

"Serikali imejipanga kutatua changamoto mbalimbali za magonjwa ya wanyama ikiwamo kumteketeza mbung'o ambaye anasumbua mifugo na hivi karibuni tunatarajia kuzindua mradi mkubwa wa kutokomeza wadudu hao utakaoanzia wilayani Meatu," alisema Mpina.

Aliwaambia kuwa serikali imejipanga kuhakikisha wafugaji hawauziwi chanjo zilizopita muda wake, wala kuongezewa bei tofauti na bei elekezi. Pia kuondoa kero ya ukosefu wa chanjo, kupima magonjwa kila eneo hususani yale yanayotoka katika nchi jirani.

Alisema Wizara itaendelea kuboresha taasisi ya kuzalisha chanjo ya TVI iliyopo Kibaha mkoani Pwani, ili kuhakikisha uchunguzi wa magonjwa unafanyika muda wote na kuondoa changamoto hizo.

Kwa upande wa changamoto ya upungufu wa maofisa ugani alisema lipo tatizo la baadhi ya maeneo kuwa na maofisa ugani wengi na nyingine kuwa na upungufu, hivyo aliiomba serikali kuangalia na kuwahamisha waliozidi katika baadhi ya maeneo na kuwapeleka sehemu zenye upungufu.

Katika hatua nyingine Mpina alizitaka sekta binafsi pamoja na taasisi za fedha kuchangamkia fursa ya uzalishaji maziwa, huku akizitaka benki nchini kuanza kutoa mikopo kwa wakulima na wafugaji kwa kuwa uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita bilioni 2.2 na kufikia lita bilioni 2.7 kwa mwaka 2019.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Profesa Elisante Ole Gabriel, akizungumzia maonyesho hayo alisema yana lengo la kuwahamasisha wananchi wazidi kufuga kwa tija na kwa kutumia sayansi na teknolojia.

Aliongeza kuwa yote yanalenga kuunganisha uchumi wa viwanda katika sekta ya mifugo na kuwataka wafugaji kutambua umuhimu wa afya kwa mnyama na uboreshaji wa malisho.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi wa Taasisi ya Kimataifa ya Ufugaji (ILRI), Dk. Jimmy Smith, alisema licha ya maziwa kuendeleza sekta ya viwanda hapa nchini lakini pia yanaongeza ajira kwa vijana.

Katika maonyesho hayo yaliyohudhuliwa na viongozi mbalimbali kulikuwa na gwaride la ng'ombe lililohusisha ng'ombe bora 40 kutoka katika mikoa mbalimbali hapa nchini waliopita kwenye mchujo na baadhi yao kushinda na kupata zawadi mbalimbali ikiwamo fedha na ngao.



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akizungumza na Balozi wa Tanzania nchini Misri, Meja Jenerali Issa Suleiman Nassori, baada ya kupokelewa jana katika Uwanja wa Kimataifa wa Cairo nchini Misri. **PICHA: BUNGE**

# 'Watanzania waambiwa kunyweni maziwa'

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

BODI ya Maziwa Tanzania (TDB) imewataka wananchi kujenga tabia ya kunywa maziwa ili kuboresha afya zao.

Aidha, imewakumbusha kutumia maziwa ili kuwainua wafugaji kiuchumi, kuboresha sekta ya viwanda na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

Akizungumza na gazeti hili jana Ofisa Huduma na Usindikaji Maziwa wa (TDB), Shehemba Jumaa, alisema maziwa ndiyo chakula pekee ambacho mtu akinywa anakuwa na afya bora kuliko kingine chochote.

Aliongeza kuwa maziwa ndiyo kinywaji ambacho mtoto akizaliwa akiwa na kilo chache anatumia na baada ya muda mfupi anaongezeka uzito, hivyo kila mmoja anapaswa kutumia maziwa bila kujali ni mtoto au mkubwa.

"Nawaomba mjijengee tabia ya kunywa maziwa bila kujali ni aina gani," alisema Jumaa.

Alieleza kuwa TDB, inaendelea na programu maalum ya kuhamasisha wafugaji kuungana kwa pamoja katika vikundi ili kuboresha uzalishaji na kurahisisha masoko lakini pia kuzalisha kwa gharama ndogo.

Alisema, mpaka sasa tayari wamefikia mikoa zaidi ya mitano ikiwamo Tanga, Pwani, Mbeya, Iringa na Njombe na bado wanaendelea na programu hiyo ili kuifikia nchi nzima.

Akizungumzia Mkoa wa Dodoma ambao ndiyo maonyesho yanafanyika, alisema haujafanikiwa kuingiza hata ng'ombe mmoja katika shindano la kutafutwa ng'ombe bora wa maziwa.

Jumaa alisema mkoa huo una ng'ombe wengi, lakini siyo wa maziwa kwa kuwa wanafugwa kienyeji zaidi.

"Dodoma ni moja ya mkoa ambao unazalisha kienyeji zaidi. Tukiangalia kwa upande wa hali ya hewa hatuoni kama inasumbua kwa kuwa mkoa wa

Dodoma kipindi cha mvua kuna nyasi za kutosha hivyo kama bodi tutalichukulia hilo kwa umuhimu mkubwa ili kuhakikisha inapiga hatua," alisema Jumaa.

Alisema mazao ya mifugo yanakumbwa na misimu kwa kuwa wanazalisha kienyeji, hivyo aliwataka wafugaji wa Dodoma kupitia maonyesho hayo kujifunza ufugaji huo wa kisasa ili kuinua uchumi wa wafugaji mkoani humo.

Kwa upande wao wafugaji kutoka mkoani Dodoma, Thobias Lihamba na Seleman Mtyani walisema wamesikitishwa na maonyesho hayo kufanyika mkoani Dodoma, lakini mkoa huo haujaingiza fainali ng'ombe bora katika shindano hilo.

"Kilimanjaro imetoa ng'ombe wengi utasema wao ndio wenyeji wa mkoa, wafugaji wa Dodoma tutumie nafasi ya maonyesho haya ili mwakani nasi tufikie lengo la ng'ombe bora katika maonyesho haya," alisema Lihamba.

Aidha, alibainisha kuwa mkoa wa Dodoma ni moja ya mkoa ambao una kituo cha uhamilishaji wa ng'ombe wa maziwa kilichopo wilayani Mpwapwa na hivi karibuni kitaanza kufanya kazi, lakini wafugaji mkoani humo bado hawajaanza kunufaika na kituo hicho.

## Kanisa lahimiza kuombea uchaguzi

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

VIJANA wametakiwa kuombea uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji utakaofanyika Oktoba mwaka huu, ili kuwapatia Watanzania viongozi wenye kuwajali watu watakaojituma kuwaletea maendeleo.

Ushauri huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Vijana Taifa wa Kanisa la Pentecoste Holiness Association Mission (PHAM), Mchungaji Felix Mapesa, alipokuwa akizungumza na vijana kwenye semina iliyofanyika Makole jijini Dodoma.

Akizungumza na vijana hao waliotoka mikoa mbalimbali, aliwataka kuombea uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Oktoba, ili wapatikane viongozi ambao watakuwa na mzigo wa kuwatumikia Watanzania.

Alisema ili viongozi hao waweze kupatikana ni muhimu vijana kote nchini wakahamasika kuomba ili viongozi hao waongoze nchi kwa upendo.

Mwenyekiti huyo pia aliwataka vijana kufanya kazi kwa bidii ili waweze kujikwamua kiuchumi na kuondokana na utegemezi ambao umekuwa ikuwarudisha nyuma kimaendeleo.

"Ni wakati sasa kukataa hii kauli kuwa hali ni ngumu wakati vijana wana nguvu ya kufanya kazi ambazo zinazoweza kuwaletea mapato ya kiuchumi na hatimaye kuondokana na umaskini," alisema.

Aidha, aliwataka vijana kuepukana na migogoro ndani ya makanisa na kwenye vyama kwa kuwa wanadhoofisha huduma za kiroho na za kimwili na hata zile za kijamii pia.

Kwa upande wake Askofu wa Kanda ya Kati, Julius Bundala, akifungua semina hiyo aliwataka vijana kuwa na maono na dira kwa ajili ya kuwaelekeza wenzao wanaowaongoza ndani ya makanisa hayo.



Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Maulid (kulia), akizungumza na mwandishi wa habari, Khatib Suleiman nje ya ukumbi wa Baraza. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Nauli za daladala zapanda Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imetangaza rasmi kupandisha nauli ya magari yote ya abiria yanayotoa huduma mijini na vijijini kuanzia mwezi ujao.

Bei hizo zitatozwa kuanzia Julai mosi mwaka huu, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa wanahabari jana na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Dk. Sira Ubwa Mamboya.

Alisema kuwa nauli hiyo ya magari ya abiria kwa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja imepanda kutoka Sh. 300, iliyokuwa gharama ya zamani na kuanzia sasa abiria watatozwa Sh. 400.

Akifafanua zaidi alisema: "Umbali wa kilomita sifuri hadi 12 nauli itakuwa ni Sh. 400 badala ya 300. Kutoka kilometa 13 hadi 15 itakuwa Sh. 500 badala ya Sh. 400, wakati kilometa 16 hadi 18 watatozwa Sh. 600 badala ya Sh. 500 , kilometa 19 mpaka 21 nauli mpya zitakuwa Sh. 900 badala ya Sh. 800," alisema Waziri Mamboya.

Aidha, alieleza kuwa kwa usafiri wa vijijini nauli imeongezeka Sh. 100 ambayo inategemeana na eneo husika, kama nauli ya sasa ni Sh. 1,000 nauli mpya itakuwa Sh. 1,100.

Alisema kuwa ongezeko hilo la nauli kwa magari ya abiria linakusudia kupunguza gharama za uendeshaji kwa wamiliki wa magari ya abiria kutokana na kupanda kwa gharama mbalimbali za uendeshaji.

Lengo ni kuwasaidia wenye magari waendelee kutoa huduma kwa wananchi, kulinda ajira za madereva na utingo na kuwepo kwa usafiri endelevu kwa wananchi.

Alieleza kuwa ikiwa nauli zitaendelea kubaki kama ilivyo sasa wamiliki wa magari ya biashara wataendelea kupata hasara na hatimaye kushindwa kutoa huduma hali itakayopelekea matatizo ya usafiri na usafirishaji. "Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji inawajibu wa kisheria kuhakikisha kuwa pamoja na mambo mengine maslahi ya watumiaji na watoa huduma za usafiri yanalindwa. "Lengo ni kuhakikisha kuwa kunakuwapo na huduma endelevu ya usafiri ulio bora na wenye kukidhi mahitaji pamoja na kujenga, kulinda na kuendeleza mazingira ya kuvutia watoa huduma." Alisema Mamboya.

Alisema kuongeza nauli pia kunalenga kuimarisha huduma ya usafiri zinazotolewa ili ziwe katika kiwango na gharama zinazoendana na huduma hizo.

Alieleza kuwa kwa nauli za magari ya abiria zinazotoa huduma katika katika miji na vijiji kwa Unguja na Pemba zitaongezeka kwa wastani wa asilimia 3.5 mpaka asilimia 40 tofauti na nauli za zamani.

# Serikali yataja sababu za kufunga kiwanda

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KIWANDA cha kuzalisha soda za kampuni ya Coca - Cola Zanzibar, kimefungwa baada ya kushindwa kutekeleza masharti ya mkataba wa makubaliano ya uzalishaji.

Waziri wa Fedha na Mipango Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, alisema hayo wakati akitoa ufafanuzi na kujibu hoja mbali mbali za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliotaka kujua hatma ya kiwanda hicho.

Balozi Ramia alisema kiwanda hicho kimefunga uzalishaji baada ya kwenda kinyume na masharti ya awali yaliyokitaka kuzalisha bidhaa za soda.

Alisema kilichofanywa na uongozi wa kiwanda hicho ni kuondoka na kuhamishia uzalishaji wa soda sehemu nyingine. Aidha, alisema wamiliki wa kiwanda hicho walikigeuza ghala la kuwekea mizigo kinyume cha makubaliano na sheria.

"Napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tumekiagiza kuondoka nchini baada ya kushindwa kuzalisha soda badala yake wamegeuza kuwanda kuwa ghala la kuhifadhi mizigo," alisema.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Said Hassan Said, alisema uongozi wa kiwanda hicho umekwenda kinyume na sheria na makubaliano ya mkataba. Alisema serikali inachotaka kuona kiwanda kinazalisha bidhaa kama ilivyokubaliwa kisheria, kukusanya kodi na kutoa ajira kwa wananchi na si kufanya kile wanachotaka wenyewe.

"Masharti ya makubaliano ya mkataba na kiwanda cha soda cha Coca Cola ni kuzalisha bidhaa hiyo lakini kwa bahati mbaya kiwanda hakifanyi kazi hiyo kimekuwa ghala,"alisema.

# Kamati yaibua changamoto za bajeti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi inayohusika na majumuisho ya mjadala wa bajeti ya serikali kuu, imetaja mambo makubwa yaliyotikisa mijadala bajeti ya serikali.

Aidha, imeeleza kuwa kutopatikana au kutotumika kwa fedha za baadhi ya miradi zilizoidhinishwa na baraza hilo kuwa ni miongoni mwa mambo yaliyojitokeza muda wote wakati wa mjadala wa bajeti hiyo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Muhammed Said akiwasilisha hotoba ya kamati hiyo, alisema kamati imebaini kukosekana utekelezaji wa miradi kuwa ni changamoto kubwa.

Alisema baadhi ya taasisi za serikali licha ya kupatiwa fedha za miradi walizoidhinishiwa katika bajeti ya mwaka 2018/2019 zilishindwa kutekeleza miradi mbalimbali, tena hazikuwa na utayari wa kutumia fedha hizo.

Alisema kamati inaishauri serikali kuhakikisha kuwa wakati wa utekelezaji wa miradi, inazingatia muda wa kumaliza miradi ili malengo ya miradi hiyo yafikiwe kwa wakati.

"Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake imebaini kuwepo na changamoto katika kifungu cha 52(2) cha sheria ya fedha ya mwaka 2016 kuhusu fedha zilizopitiwa na mwaka wa fedha bila ya kutumika ambapo katika sheria iliyoandikwa kwa Kiswahili kifungu hicho kinaelekeza kuwa fedha yoyote iliyopitiwa na mwaka bila ya kutumika irudishwe katika mfuko mkuu wa hazina,"alisema Saidi.

Alieleza kuwa jambo jingine lililojitokeza wakati wa mjadala wa bajeti ni kwa baadhi ya miradi kutokuanza hasa kwa upande wa kazi za ujenzi, licha ya kuwa miradi hiyo ni ya siku nyingi na inaidhinishiwa fedha , hata hivyo inashindwa kutekelezwa.

Alisema mifano ya miradi hiyo ni ule wa ujenzi wa Mahakama Kuu huko Tunguu ambao ni takriban mwaka wa tatu sasa lakini kwa mara nyingine umeshindwa kuanza hatua za mwanzo za ujenzi.

"Suala la kujiuliza ni kwamba miaka yote hiyo ambayo fedha zinaidhinishwa ni nini kinachokwamisha mradi huo kutekelezwa?"Alihoji.

Aidha, alitaja jambo jingine lililojitokeza ni baadhi ya wajumbe kutopatiwa ufafanuzi wa kuridhisha kwa baadhi ya fedha za miradi ikiwamo mradi wa kuendeleza vijana na ule wa kuendeleza maeneo ya kihistoria ya Mkamandume na Fukuchani.

## Kioo Limited yakwaa tuzo mwajiri bora

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Kioo Limited kwa mara nyingine imefanikiwa kutwaa tuzo ya mwajiri bora inayotolewa na Chama cha Wafanyakazi wa Sekta ya Viwanda na Biashara (Tuico), Mkoa wa Temeke.

Tuzo hizo zilitolewa juzi jioni jijini Dar es Salaam na Naibu Katibu Mkuu wa Tuico Taifa, Tamim Salehe, kwenye sherehe ya kutathmini utendaji wa chama hicho uliofanyika jijini hapa.

Mbali na kutwaa tuzo hiyo ya mwajiri bora wa mwaka, tawi bora la wafanyakazi la Tuico lilitoka kwenye kampuni hiyo ya Kioo Limited.

Tamimu aliipongeza kampuni ya Kioo kwa kuwa mshindi wa kwanza kwenye tuzo hizo na kuitaka iendelee kuwa mfano kwa waajiri wengine mwaka hadi mwaka.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo, Meneja Rasilimali Watu wa Kampuni ya Kioo Limited, Jacob Msuya, alisema ushindi huo unatokana na namna wanavyowajali wafanyakazi wao na kuthamini maslahi yao.

Alisema kuzingatia maslahi ya wafanyakazi na kuwawekea mazingira mazuri ya kazi watumishi wake imekuwa chanzo kikubwa cha kampuni hiyo kushika nafasi hiyo ya kwanza kwa mwaka wa pili mfululizo.

Msuya alisema kampuni hiyo imekuwa na uwezo mkubwa wa kutatua changamoto za ndani za wafanyakazi na menejimenti imekuwa na uhusiano mzuri na wafanyakazi wake.

"Tunathamini sana wafanyakazi na tumewawekea mazingira rafiki na salama ya kufanyakazi wafanyakazi wetu na tunafanya haya kuunga mkono juhudi za rais wetu mpendwa Dk. John Magufuli ya kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi ya viwanda," alisema Msuya.

Salehe aliusifu Mkoa wa Temeke kwa namna ambavyo umekuwa ukiongoza kitaifa kwa kujitahidi kukusanya michango na kuongeza idadi ya wanachama kila mwaka.

# Wanunuzi pamba mbaroni tuhuma kuchezea mizani

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

WAKALA wa Vipimo (WMA) umewakamata viongozi watatu wa Kampuni ya ICK inayojishughulisha na ununuzi wa pamba wilayani Kwimba mkoani Mwanza wakidaiwa kutumia mizani ambayo haijasajiliwa kwa matumizi ya vipimo tangu mwaka 2016.

Meneja wa WMA Mkoa wa Mwanza, Albogasti Kajungu, alisema watuhumiwa hao wakazi wa Kijiji cha Chakalawi, Kata ya Kapamwa Tarafa ya Mwamashimba wilayani Kwimba walikamatwa baada ya kupata taarifa kutoka kwa raia wema kwamba wanatumia mizani iliyochakachuliwa.

Walipofuatilia walikuta mizani miwili ambapo mmoja kati yake haujathibitishwa na serikali kupitia WMA.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa juzi katika operesheni ya WMA inayoendelea katika wilaya hiyo, ambapo walibaini udanganyifu unaofanywa na viongozi wa vyama vya msingi waliopewa dhamana na kijiji kusimamia mauzo ya pamba.

Alisema mizani iliyokamatwa ilikuwa inapunja kilo tatu kwa kila kilo 20.

Alisema watuhumiwa hao, wamekabidhiwa polisi na taratibu zingine za kisheria zinafuata.

"Hii ina maana kuwa mkulima akileta kilo 100 ataibiwa si chini ya kilo 13, hivyo watu kama hawa lazima wachukuliwe hatua kali za kisheria na kuwa fundisho kwa wengine.

Aidha, Kajungu alitoa tahadhari kwa viongozi wa vyama vya msingi wanaosimamia ununuzi wa zao la pamba kutenda haki kwani kinyume chake faini kali zisizopungua milioni 20 na kifungo kisichopungua miaka mitatu au vyote kwa pamoja hawataviepuka.

Mkurugenzi wa Ufundi wa WMA, Stella Kahwa, alisema ukaguzi kama huo wa kushtukiza unaendeshwa kwa mikoa yote inayolima pamba, ufuta, kahawa na tumbaku ili kuhakikisha mkulima hadhulumiwi wakati wa kuuza mazao yake na apate faida kulingana na jasho lake.

"Sasa hivi tupo katika operesheni kuangalia mizani ya pamba, ufuta, kahawa na tumbaku kama inatumika kwa usahihi, tulianza kwa kuhakiki mizani na sasa kuelekea msimu wa ununuzi wa pamba, ufuta, kahawa na tumbaku tunafuatilia kuangalia kama mizani hiyo iliyohakikiwa kweli inatumiwa vilivyo na wahusika.

"Niendelee kusisitiza kwamba wale wanaodhani kwamba hatuwezi kuwafikia wanajidanganya kwa sababu serikali imetuwezesha kufika kila mahali kwa kutumia magari makubwa naya kisasa kufanya kazi hii, wote waliozoea kuchezea vipimo vyote vya mazao tutawafikia na sheria kali dhidi yao itachukua mkondo wake," alisema Stella.

Mmoja wa viongozi wa Kampuni ya ICK, Shija Gimbisha, alikiri kuwa na mzani mmoja ingawa alisema hawautumii kupima pamba.

"Tulikuwa na mizani miwili, mmoja tulitaka tuupeleke ukagongwe muhuli kwanza ndiyo tuanze kuutumia, si tatizo kuwa na mizani miwili, huu mmoja tulikuwa hatujaanza kuutumia," alisema Gimbisha.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Songas Tanzania, Nigel Whitaker (watatu kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 108, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Sea Sense, Joana Trindade (watatu kulia), kwa ajili ya kuchangia Sh. milioni 108 kudhamini programu ya mafunzo ya mwaka mmoja kuwawezesha wananchi katika kisiwa cha Kilwa kupata elimu ya utunzaji wa fukwe na uvuaji salama. Msaada huo ni jitihada za kudumisha viumbe hai na kuchochea ukuaji wa sekta ya uvuvi nchini. Wa mwisho kulia ni Ofisa Mkuu wa Biashara na Ufuatiliaji, Sebastian Kastuli na Mshauri wa masuala ya kiufundi, Bi. Lindsey West. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafugaji wadogo wapewa mbinu za kujiinua kiuchumi

**Na Yasmine Protace**

WAFUGAJI wadogo hapa nchini wametakiwa kuchangamkia ufugaji wa kuku ili waweze kujiinua kiuchumi.

Wito huo, umetolewa na Dk. Furaha Mramba, Mtendaji Mkuu wa Maabara ya Vetenali Tanzania. Dk. Mramba ambaye alikuwa mgeni rasmi katika maonyesho ya kuku jijini, Dar es Salaam, alisema kuwa kwa sasa chanjo inapatikana na mfugaji akifuga kuku atainuka kiuchumi kutokana na kupata idadi kubwa ya kuku. "Leo tunapitia mradi huu, ambao umeanzishwa miaka minne... nimeona aina mbalimbali za kuku na kupata maelekezo jinsi wanavyouza kuku bei ndogo na kuku hao huzaliana kwa wingi," alisema.

Dk. Ezekiel Ngolomela, mtafiti kiongozi katika mradi huo, alisema mradi ulianza mwaka 2015 mpaka mwaka huu.

Alisema mradi huo ambao wa uendelezaji wa kuku Tanzania, umelenga jinsi kuku wanavyoweza kustahimili hali ya hewa.

Alisema mradi umeendeshwa katika mikoa 10, na kuwa walifanya utafiti katika maeneo ya vijijini.

Alisema wamebaini kuwa kuku aina ya kroille na sasso wanahimili mazingira ya Tanzania na kwa mwaka wana uwezo wa kutaga mayai 180 , wakati kuku wa kienyeji wana uwezo wa kutaga mayai 40 kwa mwaka.

Aliwashauri wananchi kujikita katika ufugaji hasa kinamama ambao wamekuwa wakijishughulisha katika ujasiriamali, lakini uzalishaji kukosa mzunguko mzuri.

# Iran yatungua ndege ya Marekani isiyokuwa na rubani

**TEHRAN, Iran**

IRAN imetungua ndege ya Marekani isiyokuwa na rubani katika tukio ambalo maofisa wake wanasema ndege hiyo ilikuwa katika anga ya nchi hiyo, lakini maofisa wa Marekani wamesema ilikuwa katika anga za kimataifa.

Kwa maelezo ya Iran, ndege hiyo aina ya RQ-4 Global Hawk ilitunguliwa na majeshi yake ya Revolutionary Guard katika eneo la anga la Kaskazini ya Jimbo la Hormozgan nchini humo karibu na njia kuu ya meli za kimataifa eneo la Hormuz.

Ofisa wa Marekani ameitambua ndege iliyotunguliwa kuwa ni MQ-4C Triton ambayo ilikuwa inaruka katika eneo hilo la Hormuz.

Msemaji wa Jeshi la Majini la Kikosi cha Central Command cha Marekani, Bill Urban ameiambia VOA kuwa: "Hakuna ndege ya Marekani iliyokuwa inaruka katika anga la Iran hivi karibuni."

Hata hivyo, alisita kutoa maoni yoyote zaidi juu ya tukio hilo.

Jeshi la Marekani limesema kuwa Iran ilijaribu kutungua ndege ya Marekani isiyokuwa na rubani wiki iliyopita, na mvutano huo kati ya nchi hizo mbili umeongezeka kutokana na shambulizi la meli za mafuta katika eneo hilo ambalo Marekani inailaumu Iran, wakati Iran ikikanusha kuhusika na shambulizi hilo.

Uhusiano umezidi kuwa mbaya tangu Rais wa Marekani, Donald Trump alipojitoa mwaka 2018 kutoka katika mkataba wa kimataifa uliyokuwa unaidhibiti programu ya Iran ya nyuklia kwa kupunguziwa vikwazo.

Vikwazo vipya vilivyotolewa na Marekani vimeathiri uchumi wa Iran, na Iran imetangaza kuendeleza kuzalisha uranium kwa wingi wakati ikiendelea kutafuta msaada kutoka mataifa ya Ulaya kuzuia hatua hiyo ya vikwazo vya Marekani.

***VOA***



Rais wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un (kulia), akiwa na Rais wa China, Xi Jinping, walipokutana kwa mazungumzo ya nyuklia mjini Pyongyang. **PICHA: ALLIANCE**

# Xi Jinping ziarani Korea Kaskazini

**PYONGYANG, Korea Kaskazini**

VIONGOZI wa China na Korea Kaskazini wamekuwa na mazungumzo katika Mji Mkuu wa Korea Kaskazini Pyongyang, huku ajenda kubwa inayotajwa ikiwa ni mazungumzo ya nyuklia yaliokwama na Marekani.

Shirika la Habari la China Xinhua limesema Rais Xi Jinping na kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un wamekutana kwa mazungumzo mjini Pyongyang.

Awali Xi na mke wake, Peng Liyuan na maofisa waandamizi wa China walikaribishwa kwa kupigiwa mizinga 21, katika gwaride kubwa la heshima lililofanyika katika Uwanja wa Ndege wa Pyongyang.

Takribani watu 10,000 walijipanga vyema, huku wakipunga maua hewani na kuimba kwa sauti karibu Xi, karibu Xi.

Kim na mkewe Ri Sol Ju, walikutana na ujumbe wa wapokeaji kwenye uwanja wa ndege huo.

Xi yupo katika ziara ya kikazi ya siku mbili nchini Korea Kaskazini, ambapo inaelezwa kuwa ni ziara ya kwanza kwa kiongozi wa China kuwasili nchini humo katika kipindi cha miaka 14.

Mkutano huo unafanyika wakati Xi na Kim wanakabiliwa na migogoro tofauti na Marekani.

Xi anakabiliwa na mgogoro wa kibiashara na Kim kuhusu silaha za nyuklia.

Kwa mujibu wa Xinhua, China inaweza kucheza karata ya kipekee ya kujijenga kwa kuondosha hali ya kutoaminiana kati ya Korea Kaskazini na Marekani ili waweze kufanya kazi pamoja kufanikisha jitihada za kuondosha matumizi ya nyuklia.

Marekani inaitaka Korea Kaskazini kuachana na kuendeleza silaha za nyuklia kabla ya kuondolewa vikwazo vya kimataifa ilivyowekewa taifa hilo.

Lakini Korea Kaskazini imetaka muda wa hatua kwa hatua katika kulitekeleza hilo, huku ikihimiza kupata unafuu wa vikwazo vya kiuchumi ilivyowekewa.

Katika suala hilo, China inataka uwiano sawa wa kila upande na si kuwapo kwa shinikizo la upande mmoja na matakwa yasio akisi hali halisi.

Mwanadiplomasia wa zamani wa Korea Kaskazini, Thae Yong Ho aliyetoroka mwaka 2016 alisema anadhani Kim anataka kumpa ujumbe Xi wa kuuwakilisha kwa Rais Trump, pale ambapo viongozi hao wawili watakapokutana katika mkutano wa kilele wa mataifa ya nchi za G20 wiki ijayo unaotarajiwa kufanyika Japan.

Mazungumzo ya Marekani na Korea Kaskazini yamekwama tangu Kim na Rais Trump wafanye mkutano wao wa kilele wa mara ya pili uliofanyika Februari mjini Hanoi, Vietnam.

***DW***

## Marekani yatoa tahadhari ya ugaidi Uganda

**KAMPALA, Uganda**

UBALOZI wa Marekani nchini Uganda umetoa tahadhari nyingine ya kutokea kwa shambulio la kigaidi nchini humo.

Kulingana na tahadhari hiyo iliochapishwa katika ukurasa rasmi wa mtandao wa kijamii wa balozi hiyo, kuna uvumi wa mipango ya mashambulizi katika maeneo yanayopendwa sana na raia wa kigeni katika Afrika Mashariki ikiwamo Uganda.

Ubalozi huo umesema kuwa ijapokuwa hauna ushahidi wa kutosha kuhusu tishio hilo ama habari kuhusu wakati ambapo mashambulizi hayo yatafanyika umewaonya wakazi kuchukua tahadhari. "Ubalozi hauna ushahidi wa moja kwa moja wa tishio hilo ama taarifa za muda gani mashambulizi yatatokea, hata hivyo unawaonya wananchi kuchukua tahadhari," Ilieleza taarifa hiyo. Ubalozi huo umewataka raia kuwa macho wakati wowote katika maeneo wanayozuru, kuwa na tahadhari dhidi ya makundi ya watu wengi.

Aidha, umewataka raia kuwa macho katika maeneo yanayopendelewa sana na watalii hususani wale wa mataifa ya magharibi.

**BBC**

## Misri yageuka mbogo kisa kauli ya Rais wa Uturuki

**CAIRO, Misri**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Misri, Sameh Shoukry, amelaani kauli iliyotolewa na Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan kuwa Rais wa nchi hiyo, Abdel Fattah al-Sisi alihusika na kifo cha Rais wa zamani Mohamed Morsi.

Shoukry amesema kauli ya Erdogan haikubali na imetolewa kwa nia mbaya.

"Morsi alikuwa mwenye maumivu, akiwa kwenye sakafu kwa dakika 20 na kwa bahati mbaya, hakuna kilichofanyika kumsaidia, Morsi aliuawa," alisema Erdogan.

Morsi alifariki dunia baada ya kuzirai akiwa mahakamani siku ya Jumatatu, na kuzikwa jijini Cairo juzi, mazishi yaliyohudhuriwa na familia yake peke yake. Rais Erdogan alikuwa mshirika wa karibu wa Morsi kwa kipindi cha mwaka mmoja alipokuwa madarakani kabla ya kuondolewa madarakani mwaka 2013. Tangu kipindi hicho, uhusiano wa kidiplomasia kati ya Cairo na Ankara ukaanza kuyumba.

***RFI***

# Wengine waibuka washindi M-Pawa

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara ya Afrika (CBA) na kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom, zimefanya droo yao ya pili ya promosheni ya kukopa na kuwekeza na M-Pawa inayoendelea katika kusherehekea miaka mitano ya huduma hiyo nchini.

Droo hiyo ambayo ni ya pili, ilifanyika katika ofisi za makao makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam na washindi walitangazwa mbele ya mwakilishi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Jehud Ngolo, ambaye ofisa mwandamizi wa ukaguzi, wafanyakazi wa CBA na wachekeshaji maarufu Silvery Mujuni 'Mpoki' na Ummy Wenceslaus maarufu kama 'Dokii'.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na CBA, washindi hao walichaguliwa kutoka makundi matatu ambayo ni kuweka akiba, kulipa mkopo mapema pamoja na 'Savings challenge'.

Aidha, washindi hao walipata mara mbili ya akiba iliyoko kwenye akaunti zao ambayo ina kianzio cha kati ya Sh. 1,000 na Sh. 200,000 na wengine wenye fedha zaidi ya Sh. 200,000 walipata mara mbili ya kiasi hicho.

Pia washindi wengine wa marejesho ya mkopo na 'Savings challenge' walizawadiwa simu pamoja na muda wa maongezi.

"Huduma ya M-Pawa inalenga zaidi kuwajali wateja wake na itaendelea kutoa zawadi mbalimbali katika kipindi hiki cha promosheni, huku tukijizatiti kuboresha huduma zetu za kifedha na kujumuisha wateja wetu," alisema Zainabu Mushi mwakilishi wa CBA wakati wa kuendesha droo hiyo.

"Tunawahimiza watumiaji wote wa huduma ya M-Pawa washiriki kwenye promosheni hii kwa kuweka akiba, kukopa na kurudisha mikopo yao mapema, ili kujiweka kwenye nafasi ya kushinda na kuwahimiza watu wengine wasiotumia M-Pawa kuanza kutumia huduma hii," aliongeza.

Promosheni hiyo itaendelea kila wiki kwa muda wa wiki nne na mwisho wa promosheni kutakuwa na mshindi mkubwa atakayeibuka na zawadi ya fedha taslimu Sh. milioni 15.

# Prof. Ndalichako afagilia mabaraza ya ujuzi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi Stadi, Prof. Joyce Ndalichako, amesema Mabaraza ya Ujuzi ya kisekta (SSCs), yatasaidia kupunguza tatizo la ujuzi katika nyanja mbalimbali za maendeleo.

Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) wamezindua mabaraza hayo ili kujengea uwezo wanavyuo kwenye soko la ajira.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mabaraza hayo jana jijini Dar es Salaam, Prof. Ndalichako, alisema mabaraza hayo yana nafasi nzuri ya kufanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano kuifikisha Tanzania katika uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Napenda kutoa ombi kwa sekta binafsi kuendelea kuwapokea vijana au wanachuo wanaokuja kufanya mafunzo kwa vitendo (internship) ili kuwajengea uwezo na utayari wa kuingia kwenye soko la ajira," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa TPSF, Salum Shamte, alisema mabaraza yatakuwa ni fursa pekee ya kuunganisha taasisi binafsi, serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo kutoka nje ya nchi katika kuleta ufanisi katika maendeleo.

"Tumefikia hatua nzuri mpaka kuyazindua mabaraza haya ambayo yatakuwa chachu katika kuongeza ujuzi zaidi kwa wahitimu wa vyuo mbambali," alisema Shamte.

Shamte alisema TPSF imekuwa ikitoa ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa serikali kupitia Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) katika ngazi ya wilaya, mkoa, wizara na hata taifa ili yafanyiwe kazi.

"Huu ni mwendelezo wa mambo ambayo serikali imekuwa ikiyafanya kwa kushirikiana na TPSF kwani huko nyuma tumekuwa na majadiliano mengi yenye tija kwa mustakabali wa ustawi wa uchumi wa Tanzania," alisema.

Aidha, katika hatua nyingine Bwana Shamte alisema mabaraza hayo yatajikita katika sekta kuu sita ambazo ni Kilimo, Utalii, Tehama, Uchukuzi, Ujenzi na Nishati, hali ambayo itaongeza ushirikishwaji mpana kwa wadau katika kukuza ujuzi nchini.

Kuanzishwa kwa mabaraza hayo kumeungwa mkono na wadau mbalimbali, huku wakieleza ni kwa namna gani yataenda kusaidia katika mnyororo mzima wa kukuza ujuzi nchini.

Mjumbe wa Sekta ya Kilimo, Fabian Mwakatuma, alisema mpango mkakati wa ubia wa serikali na TPSF utasaidia sana kupunguza changamoto ya wajuzi katika sekta mbalimbali.

"Watu wanaohitimu stashahada na shahada ni wengi kwa sasa nchini... lakini wengi wao hawana ujuzi na kushindwa kuleta ushindaji katika soko la ajiri, hivyo uwapo wa mabaraza haya utawaongezea thamani wahitimu wa vyuo mbalimbali," alisema Mwakatuma.

Prof. Preksedis Ndomba kwa upande wake alisema huu ni mpango wa pili wa serikali wa kuhakikisha kunakuwa na viwanda na rasilimali yenye weledi katika sekta mbalimbali.

"Ujuzi ni jambo mtambuka kwani linagusa maeneo mengi ya kisekta, hivyo mabaraza haya yanaenda kuiweka Tanzania katika ramani nzuri kiuchumi na viwanda," alisema Prof. Ndomba.

Serikali na TPSF wamekuwa na majadiliano ya mara kwa mara katika kuhakikisha baadhi ya changamoto zilizopo zinapatiwa ufumbuzi ili kuimarisha mazingira rafiki kwa upande wa uwekezaji hali ambayo imeleta mafanikio makubwa.



Meneja Rasilimali Watu wa Kioo Ltd, Jacob Msuya (kushoto), akipokea cheti cha mwajiri bora kutoka kwa Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda na Biashara (Tuico), Salehe Tamim katika hafla ya kutunuku waajiri bora iliyofanyika jijini Dar es Salaam, ambapo Kioo iliibuka mshindi wa jumla. Kulia ni Katibu wa Tuico Temeke, Magwe Muyaga na Mwenyekiti wa Tuico Temeke, Peter Mkumbi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Japan, Tanzania kutoa mafunzo ya uvuvi

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Kimataifa na Ushirikiano la Japan (JICA) kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania, zitaendesha mafunzo ya uvuvi kwa raia wa Somalia yatakayofanyika nchini kwa siku nne kwenye Chuo cha Wakala na Elimu ya Uvuvi (FETA), Mbegani, wilayani Bagamoyo.

Mafunzo hayo ya wiki tano yatakayoanza Juni 24, yatawalenga vijana kwa lengo la kuwapatia ajira, kujenga amani na kuondoa migogoro. JICA ambayo ni mtekelezaji wa Misaada ya Kimaendeleo (ODA), imeweka mkazo kwenye sekta tatu za uvuvi, ujenzi na utengenezaji (magari), ili kuongeza ajira kwa vijana wa nchi ya Somalia, ambayo kwa sasa iko kwenye mgogoro.

FETA ni kati ya taasisi zinazoaminika kwa mafunzo katika sekta ya uvuvi kwenye nchi za Afrika Mashariki.

"Hali ya eneo la maji katika nchi za Tanzania na Somalia zinafanana na FETA ina uzoefu wa mafunzo hayo kwa nchi zilizo kwenye ukanda wa Jangwa la Sahara," ilisema taarifa iliyotolewa na JICA, jana.

Taarifa hiyo ilisema kwa kipindi cha wiki tano za mafunzo, wanafunzi wa Somalia watajifunza njia za uvuvi ikiwamo matumizi ya vifaa vya uvuvi (FAD's) kutoka kwa wataalamu wa nchini Marekani.

Washiriki wa mafunzo hayo pia watapata nafasi ya kutembelea Soko la Kimataifa la Samaki, Kampuni ya Chakula Bahari, Mamlaka ya Bandari Zanzibar na Soko la Kariakoo, Dar es Salaam.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,

2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.

**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**

## NAFASI ZA KAZI

**TANGAZO LA KAZI ,** Mtu wa IT diploma anahitajika na Mesenger form six. Mawasiliano: 0715 885533

## ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

## GOROFA INAUZWA




**BOKO KAMWANGA STR**
**LOW DENSITY AREA**
**BLOC "C",**
**PLOT NO. 65**

**SIMU:** 0754 226 687 / 0756 410 345.

115258902

## VYETI VIMEPOTEA



**BAHATI ELIAS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.4060-0060** kilichotolewa na KETUMBEINE SEKONDARI mwaka 2009. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0334-0528** kilichotolewa na MWENGE SEKONDARI mwaka 2012. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **CD/IR/RB/3679/2019.**

115280902


## KUPOTEA KWA CHETI



**Valentine Heriel Minja** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.388/69** kilichotolewa na baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1983 katika shule ya Sekondari Marangu. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MOS/RB/3821/05**

115286102

## KUPOTEA KWA CHETI



**Pascal N.Mlinda** anatangaza kupotea kwa cheti cha Kidato cha nne chenye index namba **S.2456/0051** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2017 katika shule ya Sekondari Buleja. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **NBE 67171 2019**

115286302

## KUPOTEA KWA PASSPORT/ HATI YA KUSAFIRIA



**Cleverence Kombe** anatangaza kupotelewa na pasipoti ya kusafiria yenye nambari **AB819542,** iliyotolewa na Ofisi za Uhamiaji Dar es Salaam mwaka 2016. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya polisi ni **KJN/RB/772/2018.**

215286902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI/TRAILLER

**NAHDI FADHILI RAMADHANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 252 CSV VOLVO.** Kadi ya Trailler yenye namba za usajili **T 923 AJH.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PWA/BAG/RB/70884/2019.**

115286602

## KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**KHALIFA YAHAYA YUSUF** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 714 ASG.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.Taarifa Polisi. **MUH/RB/126/2019.**

115286702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA SUMBAWANGA MKOA WA RUKWA**

**SHAURI LA MAOMBI YA ARDHI NA; 15 LA MWAKA 2019**

**SIMON PETER KIMITI .............MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**JOSEPH BALTAZAR KAMEKA .............MJIBU MAOMBI**

**TANGAZO LA WITO WA KUITWA SHAURINI**

Wito huu unatolewa kwa Ndugu **JOSEPH BALTAZAR KAMEKA** wa S.L.P 147, Sumbawanga, Rukwa kuhudhuria shauri la Maombi ya Ardhi Na. 15 la mwaka 2019 katika Baraza la Ardhi na Nyumba, Wilaya ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa, siku ya tarehe 30 Julai, 2019 saa 3.00 kamili Asubuhi bila kukosa ambapo shauri hilo limepangwa kusikilizwa mbele ya Mwenyekiti wa Baraza

Kutofika kwako siku ya tarehe 30 Julai, 2019 saa 3.00 kamili Asubuhi kutapelekea shauri hilo kuendekea kusikilizwa upande mmoja

**Imetolewa na:**
**Justina Rwezaura**
**Mwenyekiti**
**Baraza la Ardhi na Nyumba, Wilaya ya Sumbawanga**
**Mkoa wa Rukwa**



215286402

**IN THE DELEGATE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.37 OF 2019**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE DEVOTA PAULIN CHIGALULA -PETITIONER**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION FRANCIS GODWIN IJENGO**


**GENERAL CITATION**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of probate for letters of administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 3th day of July , 2019.

The will if any of the said deceased to be deposited and open for inspection of the Court.

Dated 19th This day of June,2019.



115287702

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 49 OF 2019**

**In the matter of the Estate of the late ALBERT SAMWEL MOSHI of Dodoma City**

**AND**

**In the matter of an application for letters of Administration by MATILDA HENRY MTENGA**


**GENERAL CITATION**

***(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 1963)***

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filled on or before the 2 Day of July 2019.

Dated at Dodoma this 12 day of 6 2019



115286502

## Uza,

## Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza

## Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223 311

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# LIVERPOOL
## KUTOMUUZA ORIGI

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL haipo tayari kumuuza Divock Origi kipindi hiki cha majira ya joto hata kama watakuwa wamejiweka kwenye mazingira ya kumkosa kwani anaweza kuondoka akiwa huru kipindi kijacho cha majira ya joto, ESPN FC imeripoti.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji amebakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake, lakini wawakilishi wake wamekuwa katika mazungumzo ya kuongeza mkataba mpya na klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amefunga mabao kadhaa muhimu kwa Liverpool msimu uliopita na kuwasaidia kutoa changamoto kwenye Ligi Kuu ya England na kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wakati akiwa bado hajafanya maamuzi yoyote kuhusu majaliwa yake, pande zote mbili zinaonekana kutokuwa na hofu yoyote.

Origi ana furaha kubakia hapo Merseyside msimu ujao, huku Liverpool watakuwa na muda hadi Januari kuweza kumshawishi yeye kuongeza mkataba mpya.

Kama akiamua kutia saini mkataba mpya, unaweza kuwa wenye maslahi makubwa zaidi kwani yeye mwenyewe hajaonyesha nia ya kulazimisha mkataba huo usainiwe haraka.

Liverpool walimsainisha kwa pauni milioni 10 akitokea Lille ya Ufaransa mwaka 2014, huku pia akicheza kwa mkopo katika Klabu ya Wolfsburg.

"Sifikirii kwa sasa kutumia fedha nyingi kwa ajili ya usajili wa wachezaji wapya, njia bora ni kubaki na kundi la wachezaji waliopo," alisema Klopp Machi mwaka huu wakati alipoulizwa kama atafanya usajili wa wachezaji wapya kipindi cha majira ya joto.






# MESSI:
## TUNAJIAMINI, TUTAIFUNGA QATAR

**SAO PAULO, Brazil**

LIONEL Messi amesema, Argentina wana uhakika wanaweza kuifunga Qatar kwenye mchezo wao wa mwisho wa kundi kwenye michuano ya mataifa ya Amerika Kusini, Copa America.

Kikosi hicho cha kocha, Lionel Scaloni kinakabiliwa na kuondolewa kwenye hatua ya makundi katika michuano hiyo baada ya kulazimishwa sare ya kufungana bao 1-1 kwenye mchezo wao wa pili wa Kundi B dhidi ya Paraguay juzi, Jumatano.

Messi alifunga kwa mkwaju wa penalti kipindi cha pili kusawazisha bao la Richard Sanchez kwenye mchezo huo uliopigwa pale Belo Horizonte, huku Argentina wakilazimika kumshukuru golikipa wao, Franco Armani aliyeokoa penalti ya Derlis Gonzalez ili kuweza kupata pointi moja kwenye mashindano hayo.

Hata ushindi dhidi ya Qatar unaweza usitoshe kwa Argentina, lakini Messi amesema kwamba wanajiamini watapata ushindi kwenye mchezo huo.

"Nikiiangalia timu, nainona kwamba itashinda mchezo ujao," alisema akiwaambia waandishi wa habari. Messi aliongeza: "Tunaangalia uwezekano wa timu kuimarika zaidi na nina imani tutakuwa kwenye ubora."

Argentina ilikuwa kwenye wakati mgumu katika kipindi chote cha kwanza na wakafungwa bao dakika ya 37 lililofungwa na Sanchez, kabla ya Messi kusawazisha baada ya kupewa penalti iliyoamliwa na teknolojia ya maamuvi ya video, VAR.

Armani aliokoa penalti ya dakika ya 63 iliyopigwa na Gonzalez na hivyo kuwawezesha kupata pointi hiyo moja.

Argentina ipo mkiani mwa kundi lake ikiwa na pointi moja, nyuma ya Colombia yenye pointi sita, Paraguay pointi mbili na Qatar moja.

# Coutinho hajui kesho yake Barca

**SAO PAULO, Brazil**

PHILIPPE Coutinho amesema hana uhakika wapi atacheza msimu ujao wakati uvumi wake ukienea kwamba majaliwa yake ya kuendelea kuwapo Barcelona yako shakani.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alikuwa na msimu wa kuridhisha katika kipindi chake cha kwanza kucheza pale Camp Nou, kabla ya mambo kwenda ndivyo sivyo msimu huu.

Coutinho alibainisha mapema wiki hii kwamba anahitaji kujiimarisha zaidi ili kuonyesha thamani yake, ambapo Barcelona watataka kuongeza fedha zaidi kutoka pauni milioni 142 walizoilipa Liverpool wakati akisaini kuichezea Januari mwaka 2018.

Manchester United na Paris Saint-Germain zinatajwa kwamba zinamuwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, lakini kwa sasa akili yake ni kuisaidia kwanza Brazil kushinda taji la Mataifa ya Amerika Kusini, Copa America, michuano inayochezwa kwenye ardhi yao.

"Sijui majaliwa yangu, hakuna yeyote anayejua," alisema Coutinho wakati akiwaambia waandishi wa habari wakati alipoulizwa kama ataondoka Barcelona.

"Kwa sasa akili yangu inaiwazia zaidi timu ya taifa, hivyo sifikiri chochote kingine."

Coutinho alifunga mara mbili wakati Brazil ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Bolivia kwenye mchezo wa ufunguzi wa Copa America, lakini katika mchezo wao wa pili walilazimisha sare ya bila kufungana na Venezuela.

## HABARI MICHEZO



# ENRIQUE
## ABWAGA MANYANGA HISPANIA

**MADRID, Hispania**

LUIS Enrique amejiuzulu nafasi ya ukocha katika timu ya Taifa ya Hispania, huku akitoa sababu ya kuwa na matatizo ya kifamilia.

Rais wa Shirikisho la Soka nchini Hispania (RFEF), Luis Rubiales ametangaza kwamba kocha huyo ameamua kuachana na kikosi hicho.

Enrique kocha wa zamani wa Klabu ya Barcelona, aliukosa mchezo dhidi ya Malta Machi mwaka huu, pamoja na ule dhidi ya San Marino na Sweden mwezi huu.

Kocha msaidizi, Robert Moreno ndiyo amechukua nafasi ya kuinoa timu hiyo hadi pale kocha mpya atakapotangazwa.

Vyombo vya habari za michezo nchini Hispania vimeombwa kumpa heshima yake, Enrique kutokana na alichokifanya tangu alipoteuliwa ndani ya timu ya taifa.

Katika taarifa yake rais wa 'TFF' ya Hispania, Rubiales amesema, "vyombo vya habari Hispania lazima viheshimu hii hali ilivyo na tunaomba kuendelea kufanya hivyo. Tunamwamini Robert kuendelea na kazi hiyo ya kutupeleka kwenye Euro 2020."

## MATA ASAINI MIAKA MIWILI MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

JUAN Mata amesaini mkataba mpya na Manchester United, klabu hiyo imethibitisha.

Kiungo huyo ambaye mkataba wake ulikuwa unamalizika Juni 30, mwaka huu, amesaini kuongeza miaka miwili ya kuendelea kukaa hapo Old Trafford hadi mwaka 2021, huku kukiwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja.

"Ni heshima kubwa kuendelea kuiwakilisha klabu kubwa kama hii na yenye mashabiki wa aina yake," alisema Mata. "Nimekuwa hapa Manchester United kwa kipindi cha miaka mitano na najisikia fahari kubakia hapa Old Trafford kwani ni nyumbani.


"Nasubiria kuendelea kufanya kazi na Ole pamoja na benchi lote la ufundi; mtazamo walionao unaifanya klabu kuwa na matarajio makubwa zaidi na nina furaha kubwa kuwa sehemu yao."

Mazungumzo kati ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 na United yalisimama na klabu hiyo haikuwa tayari kuongeza mkataba wa zaidi ya mwaka mmoja.

Makubaliano zaidi yamefikiwa baada ya Solskjaer kuonyesha kumhitaji Mata na hivyo maamuzi ya kuongezwa mkataba yakafanyika.

"Juan ni mchezaji wa aina yake na ni mmoja wa wachezaji niliofanya nao kazi," alisema Solskjaer. "Yeye ni mfano mzuri kwa wachezaji wetu vijana kwani ndiye atakuwa chachu.

"Anaelewa nini maana ya kuwa mchezaji wa Manchester United na amekumbatia kila kitu kuhusu klabu hii."



# Giampaolo kocha mpya AC Milan

**MILAN, Italia**

AC Milan imemteua Marco Giampaolo kuwa kocha wao mpya juzi na amepewa kazi ya kujaribu kumaliza ukame wa miaka nane bila taji na kuwarudisha kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kuwa nje kwa misimu sita.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 51, awali aliinoa Sampdoria kwa misimu mitatu, na sasa ana changamoto kubwa ya kurudisha heshima ya Milan ambayo ni kama imepotea.

Anachukua nafasi ya Gennaro Gattuso ambaye aliachana na klabu hiyo Mei mwaka huu akiwa amebakiwa na miaka miwili kwenye mkataba wake baada ya Milan kushindwa kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, ikiwa imemaliza nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Italia, Serie A.

Milan ilisema katika taarifa yake kwamba wamempa Giampaolo mkataba wa miaka miwili, huku kukiwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja zaidi.



Milan, mabingwa mara saba wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na mabingwa mara 18 wa Serie A, wamekuwa kwenye kiwango duni kwa kipindi cha misimu michache iliyopita, huku wakiwa hawajatwaa taji lolote kwa kipindi cha misimu nane.

Kwa mara ya mwisho kutwaa taji la Serie A, ilikuwa ni mwaka 2011 na haijafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu msimu wa 2013-14 wakati walipoishia kwenye hatua ya mtoano wa timu 16.

Bilionea wa Italia na Waziri Mkuu wa zamani, Silvio Berlusconi ambaye alikuwa mmliki wa klabu hiyo aliiuza kwa Kampuni ya China kwa euro milioni 740 Aprili mwaka 2017.

Na mwaka uliofuata klabu hiyo ikachukuliwa na Kampuni ya Marekani ya Elliott Management.

Giampaolo alitumia kipindi chake cha uchezaji soka katika ligi daraja la tatu na la pili kabla ya kuumia kifundo cha mguu kilichomstaafisha soka akiwa na umri wa miaka 30.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA MOYO UPO JUVE, REAL YAHAHA

**Hali ilivyo itakuwa ni vema United kumruhusu mchezaji huyo aliyesajiliwa kwa rekodi ya klabu kuondoka...**

**Manchester, England**

WAKATI Paul Pogba akitaka kuondoka Manchester United huku miamba hiyo ya Old Trafford ikimthaminisha na pauni milioni 150, imefahamika moyo wa kiungo huyo bado upo Juventus zaidi ya Real Madrid ambayo nayo imekuwa ikihaha kupata saini yake majira haya ya joto, kwa mujibu wa Sky Italia.

Mabingwa hao wa Italia wapo tayari kumrejesha Pogba hapo Turin na inaaminika inajaribu kutafuta njia ya kufika kiasi cha mshahara anachohitaji kabla ya kuketi katika meza ya mazungumzo na United.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 26, kwa sasa anataka kuondoka Old Trafford na Jumapili alisema "unaweza kuwa muda muafaka kupata changamoto mpya kwingineko."

Pogba hataki kuongeza mkataba mpya United, wakati huu akiwa amebakiza miaka miwili katika ule wa awali, ingawa pia klabu ina uamuzi wa kuongeza miezi 12 moja kwa moja.

Sky Sports News inatambua kwamba United inatarajia Pogba atabaki Old Trafford majira haya ya joto, lakini inakiri kwamba kutokana na hali ilivyo itakuwa ni vema kumruhusu mchezaji huyo aliyesajiliwa kwa rekodi ya klabu kuondoka.

Wakati wakitaka kumbakisha mshindi huyo wa Kombe la Dunia, baadhi hapo United wanaeleweka kuwa na wasiwasi juu ya tabia ya Pogba na ushawishi wake mbaya juu ya idadi ya vijana kikosini.

Pogba ameitumikia Juventus kwa kipindi cha miaka minne baada ya kukataa mkataba mpya United mwaka 2012, na kuiwezesha kushinda ubingwa wa Serie A mara nne na makombe mawili ya Italia kabla ya kurejea tena Old Trafford mwaka 2016.

Mkurugenzi wa Michezo wa Juventus, Fabio Paratici alisafiri kwenda United wiki iliyopita kufanya mazungumzo kuhusu kuipata saini ya Pogba, ingawa kiungo Adrien Rabiot, ambaye anaondoka PSG, na nyota wa Lazio, Sergej Milinkovic-Savic pia wakieleweka kuwa katika rada zao.

Sky Italia inatambua kuwa Joao Cancelo, beki wa kulia wa Juventus ambaye inawezekana akaondoka majira haya ya joto, anaweza kuwa sehemu ya dili la kumnasa Pogba.

Real Madrid pia inavutiwa na kuipata saini ya kiungo huyo raia wa Ufaransa, ambaye aliomba kuondoka United majira ya joto yaliyopita, huku pia Barcelona nayo ikivutiwa naye.

Hata hivyo, miamba hiyo ya Hispania tayari imeshatumia zaidi ya pauni milioni 250 kwa ajili ya kuwasainisha wachezaji wapya na kuna wasiwasi wa kuweza kukidhi sheria ya kununua wachezaji kulingana na mapato ya klabu.

## KWA UFUPI

**LAMPARD KULA MITATU CHELSEA**
Chelsea inatumaini ya kumteua Kocha wa Derby, Frank Lampard kuwa kocha wao mpya kwa mkataba wa miaka mitatu wiki hii. ***(Standard)***

**WAN-BISSAKA SAFARI YAIVA UNITED**
Manchester United imekubali ada ya pauni milioni 55 kumsaini beki wa Crystal Palace na England U-21, Aaron Wan-Bissaka. ***(Record)***

**NEYMAR ASAKA NYUMBA BARCA**
MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Neymar, 27, ameanza kutafuta nyumba ya kuishi Barcelona, suala ambalo limeongeza tetesi kwa nyota huyo wa kimataifa wa Brazil kujiandaa kurudi Nou Camp. ***(Sport)***

**RODRIGUEZ, BALE WAGEUZWA CHAMBO**
Real Madrid imetoa ofa ya pauni milioni 115 kwa mshambuliaji wa PSG, Neymar na itaongeza aidha mshambuliaji raia wa Wales, Gareth Bale, 29, ama kiungo Mcolombia James Rodriguez, 27, kwa dili lolote. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**ARSENAL YAELEKEA KWA TIERNEY**
Arsenal imeelekeza mipango yake katika kumsajili beki wa pembeni wa Celtic, Mscotland Kieran Tierney, 22, majira haya ya joto. ***(Mail)***

**BAYERN, CITY VITANI KWA RODRI**
Bayern Munich inajiandaa kutoa upinzani kwa Manchester City katika mbio za kuisaka saini ya kiungo Mhispania Rodri, 22, kutoka Atletico Madrid. ***(AS - in Spanish)***

**JORGINHO KUMFUATA SARRI JUVE**
Jorginho, 27, yupo tayari kuitema Chelsea na kumfuata Maurizio Sarri katika klabu ya Juventus ikiwa ni mwaka mmoja baada ya kiungo huyo kujiunga na klabu hiyo akitokea Napoli kwa pauni milioni 50. ***(Mirror)***

**INTER, ATLETICO ZAMTAKA BERTRAND**
Inter Milan na Atletico Madrid zinavutiwa kuipata saini ya beki wa pembeni wa Southampton, Muingereza Ryan Bertrand, 29. ***(Mail)***

**CITY, UNITED ZAKWAMA KWA RICE**
West Ham imeiambia Manchester United na Manchester City kwamba haina lengo la kumuuza kiungo wa kimataifa wa England, Declan Rice, 20, katika dirisha la majira haya ya joto. (Sky Sports).

**SOLSKJAER AITAKA SAINI YA BROOKS**
KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer yupo tayari kuisaka saini ya kiungo wa Bournemouth na Wales, David Brooks, 21. ***(Sun)***

**SALIBA KUVUTWA ARSENAL WIKI HII**
ARSENAL itatoa ofa wiki hii kwa beki wa Saint-Etienne, Mfaransa William Saliba, 18. ***(Yahoo Sport France, via Express)***

**DIAME KUACHANA NA NEWCASTLE**
KIUNGO wa Newcastle United, Mohamed Diame, 32, anatarajiwa kujiunga na Al-Gharafa ya Qatar wakati mkataba wa nyota huyo wa kimataifa wa Senegal utakapomalizika hapo na miamba hiyo ya Tyneside mwishoni mwa Juni. ***(Chronicle)***

**CAMACHO KUNG'OLEWA LIVERPOOL**
Sporting Lisbon ipo katika mazungumzo na Liverpool kuhusu uwezekano wa kuipata saini ya winga Mreno Rafael Camacho. ***(Standard)***



HABARI MICHEZO

# WAKUTEMWA YANGA SASA MGUU SAWA

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Yanga unatarajia kutangaza majina ya wachezaji wote ambao watawaacha ndani ya kikosi chao kuelekea msimu ujao ili waanze kujitafutia timu mapema kabla ya dirisha la usajili kufungwa, imefahamika.

Akizungumza na mwandishi wetu jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Dk. Mshindo Msolla, alisema kwa sasa hawezi kutaja majina hayo mpaka hapo kila kitu kitakapokamilika huku akisema mchakato huo wa kuwatangaza unafanyiwa kazi na kwamba watawatangazia wanachama wao ili wajue kinachoendelea.

"Wiki ijayo tutatangaza majina ya wachezaji wote ambao hatutakuwa nao tena katika msimu ujao wa Ligi Kuu ili waanze taratibu za kutafuta maisha mengine kabla dirisha la usajili halijafungwa," alisema Msolla.

Aidha, mwenyekiti huyo aliendelea kueleza kuwa uwanja waliopewa Kigamboni na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda watauboresha kwa kuhakikisha wanatimiza malengo yao waliyojiwekea kwa kuifikisha mbali zaidi klabu yao.

"Uwanja tuliopewa Kigamboni tutaufanyia kazi kuhakikisha tunaufanya uwe wenye ubora ambao utatusaidia sisi kama klabu pamoja na wachezaji wetu kuwa na uwanja wenye hadhi nzuri," alisema.




Mkuu wa Huduma na Bidhaa wa Tigo, David Umoh (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa ushirikiano na Dstv utakaowawezesha wateja wa kampuni hizo, kushuhudia michuano ya fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, kwa vifurushi vya gharama nafuu. Kulia ni Mkuu wa Idara ya Masoko wa Dstv, Baraka Shelukindo na Mtaalamu wa Huduma za Intaneti wa Tigo, Allen Salaita. **MPIGAPICHA WETU**

# Afcon mubashara kiganjani mwako kupitia Tigo, DStv

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, zikitarajiwa kuanza leo kwa wenyeji Misri kukata utepe dhidi ya Zimbabwe huku timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars' yenyewe ikitarajiwa kushuka dimbani Jumapili kuvaana na Senegal, wateja wa Kampuni ya simu ya tiGO na DStv, wameletewa fursa ya kushuhudia michuano hiyo mubashara kiganjani mwao wakiwa sehemu yoyote na kwa muda wowote, imeelezwa.

Furaha hiyo imekuja kufuatia kampuni hizo mbili kuzindua ushirikiano maalum na mahususi wa huduma ya DStv itakayowapa wateja wake fursa ya kutazama mechi hizo kupitia "DStv Now mobile App" kwa gharama nafuu.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa ushirikiano huo jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Bidhaa na Huduma wa Tigo, David Umoh alisema ushirikiano huo na DStv unaendana sambamba na lengo la kampuni hiyo kukuza maisha ya kidijitali kwa kila Mtanzania.

"Tunayofuraha ya kuzindua huduma hii maalum ya DStv itakayowapa wateja wetu wa Tigo katika msimu huu wa michuano ya Afrika kupata fursa nzuri ya kutazama mechi mtandaoni na kushuhudia timu yao pendwa ya Taifa Stars na timu nyingine zinazoshiriki mashindano haya makubwa barani Afrika," alisema Umoh.

Aliongeza: "Kupitia mtandao wetu bora wa 4G, tunaweza kuwahakikishia wateja wetu wanaotumia DStv fursa ya uhakika ya kuunganishwa mubashara na bila usumbufu wowote kuangalia Kombe la Mataifa ya Afrika, kutoka sehemu yoyote na muda wowote kupitia DStv Now App katika vifaa walivyonavyo. Hii ni fursa nzuri pia kwa wale wateja ambao kwa sababu mbalimbali hawatakuwa na nafasi ya kutazama kupitia televisheni zao."

Kwa mujibu wa Umoh, Tigo inawapa wateja wake waliounganishwa na DStv nafasi ya kuchagua vifurushi vitatu. Cha kwanza ni kifurushi cha GB 1.5 kwa gharama ya Sh. 2,000 kwa saa 24, cha pili ni cha GB sita kwa gharama ya Sh. 7,000 kwa siku saba, na kifurushi cha tatu ni GB 16 kwa Sh. 20,000 kwa mwezi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Masoko Multichoice Tanzania, Ronald Shelukindo, alisema uzuri wa DStv Mobile App ni kwamba inaweza ikafanya kazi katika vifaa aina nne bila nyongeza ya gharama yoyote.

"Hakutakuwa na gharama ya ziada kutazama DStv kupitia vifaa mbalimbali, kwa sababu gharama zote zinakuwa zimeshalipiwa katika kifurushi cha mwezi cha DStv. Ili kuweza kuangalia mechi za Afcon, wateja wa DStv wanachohitaji kufanya ni kupakua DStv App katika simu janja zao, kompyuta mpakato, tablet au vifaa janja vingine," alisema Shelukindo.

Alifafanua kuwa uzuri mwingine wa kipekee ambao mteja anaweza kuupata kupitia huduma hii ni kwamba wateja wa DStv wanapewa uwezo wa kuunganisha hadi vifaa vinne tofauti kwa wakati mmoja kutazama vipindi vya DStv wakati huo televisheni nayo ikiwa nayo imeunganishwa na kuendelea kutumika kuangalia vipindi.

Shelukindo aliongeza kuwa, mechi za Afcon zitakuwa zinaonyeshwa kupitia vifurushi vyote vya DStv kuanzia kifurushi cha bei ya chini kabisa mpaka kifurushi cha DStv Premium, ambapo watakuwa na uwezo wa kufurahia mechi zote 52 za mashindano hayo.

Stars ambayo inashiriki fainali hizo kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 39, ipo Kundi C pamoja na Algeria, Senegal na jirani zao, Kenya.

## Mwenge yarejeshwa Ligi Kuu Z'bar 2019/20

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

HATIMAYE Klabu ya Mwenge imerudi tena Ligi Kuu ya Zanzibar msimu ujao baada ya kukubaliwa rufaa yake na Kamati ya Rufaa na Usuluhisho ya ZFF kufuatia Chama cha Soka (ZFA) wakati huo kushindwa kutekeleza kanuni yake ya mashindano na kuishusha klabu hiyo kinyume cha utaratibu wa kikanuni za 2018/19.

Kwa mujibu wa barua iliotelewa na Kamati ya Rufaa kwenda kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar yenye namba ya Kumbukumbu ZFF/NV/96/VOL41/262 2019, ilisema kamati ya rufaa na usuluhisho imeirejesha Klabu ya Mwenge Ligi Kuu ya Zanzibar baada ya kusikiliza maombi ya klabu hiyo.

Katika maelezo yake Klabu ya Mwenge ililalamiki Kamati ya Rufaa na Usulihisi kuwa ZFA wakati huo ilishindwa kutaja kifungu cha kanuni kilichoishusha klabu hiyo Daraja la Kwanza, na kwamba ilishindwa kusimamia kanuni ya mashindano inayosema ligi itachezwa na klabu 20 badala yake Ligi Kuu Zanzibar imechezwa ikishirikisha klabu 19 bila ya muongozo wa ZFA.

Kwa upande wake Kamati ya Rufaa na Usulihisi chini ya Mwenyekiti wake, Taki Abdulla Habibu wamekubali ombi la rufaa la Klabu ya Mwenge na kutupilia mbali uamuzi uliotolewa na ZFA kupitia kamati ya maridhiano sasa klabu hiyo itacheza tena Ligi Kuu ya Zanzibar msimu huu 2019/2020.

## Mtibwa yatangaza siku ya 'fujo' sokoni

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Mtibwa Sugar, umesema unatarajia kuanza kufanya usajili wa wachezaji na kutangaza majina ya wachezaji watakaowaacha mwanzoni mwa Julai mwaka huu kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Zuberi Katwila, alisema kwa sasa bado wanashauriana kuwa ni aina gani ya wachezaji ambao wanawahitaji kwa ajili ya msimu huo ambao unaonekana utakuwa na ushindani mkubwa kutokana na maandalizi yanayofanywa na timu.

"Sasa hivi bado tunajadiliana kupata wachezaji wazuri ambao watatusaidia kufanya vizuri msimu ujao, lengo ni kusainisha vifaa ambavyo vitaleta ushindani ndani ya timu yetu,"alisema Katwila.

Kocha huyo alisema msimu uliopita ulikuwa mgumu na kwamba msimu ujao atafanya vizuri ili ashike nafasi ya juu zaidi katika msimamo wa Ligi Kuu na kuwataka mashabiki wao waendelee kuwapa ushirikiano kama walivyofanyia msimu uliopita.

Michezo
Ijumaa Juni 21, 2019
Nipashe



Pogba moyo upo Juve, Real yahaha

HABARI UK 30

AMETUA...




Mmoja kati ya Wakurugenzi wa Klabu ya Simba, Salum Abdallah 'Try Again' (kulia), akimkabidhi hati ya mkataba wakala wa mchezaji, Sharaf Eldin Shiboub Ali Abdalrahman (katikati), baada ya kutia saini ya kuitumikia miamba hiyo kwa mkataba wa mwaka mmoja jana.
**PICHA: SIMBA**

# SIMBA YANASA KIUNGO BORA 'KATILI' WA SUDAN

●●● Ni fundi wa kukaba, vichwa na mipira iliyokufa, ameicheza timu ya taifa tangu akiwa kinda, sasa...

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa soka Ligi Kuu Bara, Simba, wamedhihirisha hawataki kufanya makosa msimu ujao kwenye ligi hiyo na michuano ya kimataifa kufuatia kuendelea kujiimarisha kwa kuinasa saini ya kiungo wa kimataifa wa Sudan, Sharaf Eldin Shiboub Ali Abdalrahman, aliyekuwa akikipiga Klabu ya Al Hilal ya nchini humo.

Shiboub ambaye anajulikana kwa shughuli yake pevu katika idara ya kiungo mkabaji wengi wakimuona kama 'kiungo katili' kutokana na ubora wake katika ukabaji, amekuwa kiungo bora mara mbili mfululizo wa Ligi Kuu ya Sudan.

Aidha, Shiboub amekuwa akiichezea timu ya Taifa ya Sudan tangu akiwa na umri wa miaka 17, na sasa amesaini mkataba wa mwaka mmoja wa kuitumikia Simba.

Miongoni mwa mambo ambayo yanamfanya Shiboub kuwa bora dimbani, inaelezwa ni pamoja na pasi zake za uhakika, huku akimudu kutumia nguvu zake vema katika ukabaji, lakini pia akielezwa kuwa fundi mzuri wa mipira 'iliyokufa' (faulo) pamoja na mipira ya kichwa.

Mchezaji huyo alitambulishwa rasmi jana na picha zake akisaini mkataba zikipostiwa kwenye ukurasa rasmi wa Instagram wa Simba SC akiwa na mmoja wa wakurugenzi wa klabu hiyo, Salum Abdallah 'Try Again'.

"Kiungo bora mara mbili mfululizo wa Ligi Kuu ya Sudan na mchezaji wa timu ya Taifa ya Sudan tangu akiwa na miaka 17, akitokea kwa mabingwa mara tatu mfululizo wa Ligi Kuu ya Sudan Klabu ya Al Hilal, Sharaf Eldin Shiboub Ali Abdalrahman amejiunga na mabingwa wa nchi kwa mkataba wa mwaka mmoja. Karibu Msimbazi Sharaf," ilisomeka taarifa hiyo katika ukurasa rasmi wa Instagram wa Simba. Shiboub anakuwa mchezaji mpya wa tatu kusaini kuichezea Simba, baada ya kipa Beno Kakolanya kutoka Yanga na beki wa kati, Kennedy Juma kutoka Singida United wote Watanzania.

Hata hivyo, kuna taarifa za klabu hiyo kuwapo kwenye mazungumzo na mawakala wa wachezaji kadhaa na wengine wameripotiwa kuwa njiani kutua nchini.

Miongoni mwao ni beki wa kati, Mbrazil Gerson Fraga Vieira kutoka ATK ya India na mshambuliaji Ryan Moon kutoka Kaizer Chiefs ya kwao, Afrika Kusini.

Katika hatua nyingine, kikosi cha Simba kiliondoka jijini Dar es Salaam jana asubuhi kwa ndege kuelekea Misungwi kupitia jijini Mwanza kwa ajili ya mchezo wa kirafiki dhidi ya wenyeji wao, Gwambina FC.

Mechi hiyo ni maalum kwa ajili ya ufunguzi wa uwanja wa Klabu ya Gwambina inayoshiriki Ligi Daraja la Pili Tanzania Bara.

Baadhi ya wachezaji wa kikosi hicho waliokwenda ni pamoja na beki mpya, Kennedy Juma, Yusufu Mlipili, Hassan Dilunga na Said Ndemla.

# Rais Caf aletewa Fatma wa Fifa

**CAIRO, Misri**

Shirikisho la Soka duniani (Fifa), limethibitisha kumteua Katibu Mkuu wake, Fatma Samoura kuwa 'Mjumbe Mkuu wa Fifa kwa Afrika' katika jitihada ya kuimarisha utawala kwenye soka barani Afrika.

Kwa kipindi cha hivi karibuni, Shirikisho la Soka barani Afrika (Caf), limekuwa likichunguzwa kwenye masuala mbalimbali yanayohusu uongozi na utawala.

Fatma ambaye ni raia wa Senegal atashika uongozi huo kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Agosti Mosi, mwaka huu, huku kukiwa na uwezekano wa 'kuongezewa muda katika wadhifa huo kwa makubaliano ya taasisi zote mbili'.

"Pia wamekubaliana kuwa Fifa na Caf watafanya ukaguzi wa uchunguzi wa hesabu za Caf haraka iwezekanavyo," taarifa hiyo iliongeza.

Samoura, 56, atasalia kuwa Katibu Mkuu wa Fifa, lakini ataelekeza baadhi ya majukumu mbalimbali kwa wengine katika shirikisho hilo.

Uamuzi huo una maana gani?

Fifa limeutaja uamuzi huu kama 'hatua ya kipekee na ya muda mfupi' kama ilivyoelezea wazi majukumu atakayokuwa nayo ofisa huyo wa zamani wa Umoja wa Mataifa.

Wakati Fifa imezoea kuziteua kamati za kawaida ambazo zinaendesha muungano wa wanachama wake wanaohitaji kusaidiwa, si kawaida yake kusaidia shirikisho katika matatizo kama hayo.

Rais wa Caf Ahmad amekuwa akichunguzwa hivi karibuni katika nyanja mbalimbali, ikiwamo kuhojiwa na maofisa wa Ufaransa mjini Paris mapema mwezi huu kabla ya kuachiliwa huru pasi kushtakiwa, hiyo ikiwa ni sehemu ya uchunguzi kuhusu tuhuma za ufisadi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >